# Nipashe

Jumatano Februari 26, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580164

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




## Mzee wa miaka 85 afungiwa mahubusu siku 3 bila chakula

UKURASA 3



Takukuru inavyopambana na rushwa makao makuu — Ukurasa 14

Uchaguzi serikali za mitaa DRC wapigwa tena kalenda — Ukurasa 17

siasa — JUMATANO FEBRUARI 26, 2020 — Nipashe — HABARI BORA NA KAMILIFU

Ni Agathon Rwasa dhidi ya kipenzi cha Nkurunziza — Ukurasa 19

Huyu ndiye Mashinji aliyeondoka

• Ameitumikia Chadema miezi 46
• Kaacha msururu wa ahadi zake

Na Mwandishi Wetu

ILIKUWA Machi 13 mwaka 2016 siku ya kumbukumbu isiyosahaulika kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji, baada ya kutangazwa kushika nafasi hiyo baada ya kupata baraka za Baraza Kuu la chama hicho kwa asilimia 100.

Wajumbe wa Baraza Kuu walikutana jijini Mwanza ikiwa ni miezi kadhaa tangu aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa, kujiunga na chama hicho na kubeba jukumu la kupeperusha bendera ya uliokuwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) kupitia Chadema katika nafasi ya urais, kwenye uchaguzi mkuu wa 2015.

Hata hivyo, Lowassa hakushinda nafasi hiyo kwa kuwa alipata kura milioni 6.07 sawa na asilimia 39.97 na mshindi akawa Rais John Magufuli, aliyeshinda kwa kura milioni 8.88 akijikusanyia asilimia 58.46.

Katika kikao cha Mwanza jina la Mashinji lililetwa mbele ya Baraza na Mwenyekiti wa Chadema Taifa.

INAENDELEA UK.16

Dk. Vincent Mashinji. PICHA: MTANDAO

Baada ya miongo kadhaa, al Bashir sasa kutinga ICC — Ukurasa 20

Mapito ya Katibu Mkuu Dk. Vincent Mashinji na nyayo zake Ukurasa 18

UKURASA 13

# Mabilioni ya benki yalivyoibwa kiajabu

**WATUHUMIWA** wakutwa na mabilioni nyumbani, wanunua magari, nyumba na viwanja, polisi 9 waingia matatani...*Endelea ukurasa wa 2*



UKURASA 3

## WATUMISHI WA SERIKALI MBARONI MADAI YA RUSHWA

UKURASA 3

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, akiwaonyesha wanahabari jana, fedha walizozikamata kutoka kwa walinzi wa kampuni ya ulinzi ya G4S. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store


## Raia China watuhumiwa kumpa Kamishna TRA mlungula mil. 11/-

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA, YANGA ZAITIWA MWAMNYETO COASTAL UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Msamaria mwema akimsaidia mwendesha pikipiki, baada ya kuanguka huku akiwa amepakia magunia ya mkaa katika eneo la Chanika, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Raia China watuhumiwa kumpa Kamishna TRA mlungula mil. 11/-

**Na Hellen Mwango**

RAIA wawili wa China wanaodaiwa kuwa mke na mume, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na tuhuma za kutoa rushwa ya Sh. milioni 11.5 kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Edwin Mhede.

Washtakiwa hao, Zheng Rongnan (50) na Ou Ya (47), wote wakazi wa Kinyambo, Mafinga C, Iringa wamefikishwa mahakamani hapo jana na kusomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huduma Shaidi.

Wakili wa Serikali, Mwakatobe Mshana, alidai kuwa Februari 24, mwaka huu, washtakiwa wote wakiwa katika Makao Makuu ya TRA yaliyopo Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, walitoa rushwa ya Dola za Marekani 5,000 (Sh. milioni 11.5) kwa Kamishna Mkuu Dk. Mhede, kama kishawishi cha kuwasaidia kampuni yao isilipe kodi ya Sh. bilioni 1.3 kiasi ambacho kilipaswa kuilipa mamlaka hiyo.

Baada ya kusomewa mashtaka, washtakiwa hao walikiri kutenda kosa hilo.

Hakimu Shaidi alisema kufuatia washtakiwa kukiri kosa hilo, kesi hiyo italetwa leo kwa ajili ya maelezo ya awali na upande wa mashtaka umlete mkalimani kwa ajili ya mshtakiwa wa kwanza ambaye hajui Kiingereza.

# Mabilioni ya benki yalivyoibwa kiajabu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia watu wanne waliokuwa wafanyakazi wa Kampuni ya Ulinzi ya G4S Security kwa tuhuma za wizi wa mabilioni ya shilingi kutoka benki na kuyatumia kununua magari, nyumba na viwanja ndani ya siku chache.

Vilevile, jeshi hilo linawashikiliwa askari wake tisa wa kanda hiyo akiwamo Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, aliyeongoza kikosi cha ukaguzi dhidi ya watuhumiwa, kwa kukiuka masharti na taratibu za kimaadili.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliwaambia waandishi wa habari jijini jana kuwa tukio hilo lilitokea Februari 7 mwaka huu na fedha zilizoibwa ni Sh. bilioni 1.28, Dola za Marekani 402,000 (Sh. milioni 923.782) na Euro 27,700 (Sh. milioni 68.967).

Mambosasa aliwataja watuhumiwa hao wanne kuwa ni Christopher Rugemarila (34), dereva wa kampuni hiyo ya ulinzi mkazi wa Chanika, Mohamed Ramadhani (40), mlinzi mkazi wa Mtoni Kijichi, Ibrahimu Maunga (49), mlinzi na mkazi wa Kiluvya na Salim Shamte (45), mkazi wa Mbagala Kizuiani.

Akisimulia kuhusu tukio hilo, Kamanda Mambosasa alisema Februari 7 mwaka huu, watuhumiwa watatu ambao ni Rugemarila, Ramadhan na Maunga walikuwa na gari lenye namba za usajili T 728 BAN, Nisan Hard Body, mali ya Kampuni ya Ulinzi ya G4S, ambalo ni mahususi kwa usafirishaji wa fedha.

"Walinzi hawa walikabidhiwa fedha kutoka tawi la Kariakoo la Benki ya NBC na NBC Samora ili wazipeleke makao mkuu ya benki hiyo yaliyoko Posta ya Zamani pale Sokoine Drive, lakini hawakufanya hivyo.

"Matokeo yake walipanga njama na kuelekea maeneo ya Temeke Maduka Mawili karibu na Kituo cha Mafuta cha Camel na kuchukua fedha zote na kuzipakia kwenye gari dogo lenye namba za usajili T134 DHY lililokuwa likiendeshwa na Salum Shamte," alidai.

Kamanda Mambosasa alisema kuwa baada ya kufanikisha uhalifu huo, watuhumiwa hao walitelekeza gari, silaha mbili aina ya Pump Action na bastola moja, mali ya Kampuni ya Ulinzi ya G4S.

"Vingine walivyovitelekeza ni mashine ya kuhesabia fedha na mihuri ya Benki ya CBA kisha waliondoka na kwenda kusikojulikana," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema katika ufuatiliaji wa tukio hilo, mchana wa Februari 17 mwaka huu, huko Mongo la Ndege jijini, mtuhumiwa wa kwanza, Rugemarila, alikamatwa na alipopekuliwa, alikutwa na Sh. milioni 110, Dola za Marekani 19,000 (Sh. milioni 43.661) zikiwa ndani ya gari lake lenye namba za usajili T 691 DSU.

"Mtuhumiwa Rugemarila alikutwa na magari ambayo ni T 691 DSU la Sh. milioni 15, T 909 DSU Toyota Rumx la Sh. milioni 13, T 627 DSU Toyota IST la Sh. milioni 11, T 653 DSU Toyota IST la Sh. milioni 11 na T 857 Toyota IST la Sh. milioni 11," alisema.

Alisema baada ya kuhojiwa, mtuhumiwa huyo alikiri kununua nyumba mbili na kiwanja kimoja vyenye thamani ya Sh. milioni 107 na samani za ndani kwa Sh. milioni tano.

Kamanda Mambosasa alisema mtuhumiwa huyo alikutwa na mali zenye thamani ya Sh. milioni 297.1 huku akikutwa pia na fedha za kigeni Dola za Marekani 21,000 (Sh. milioni 48.257).

Pia, alisema kuwa siku tano kabla ya kumkamata mtuhumiwa huyo, Jeshi la Polisi liliwakamata watuhumiwa wengine wawili ambao ni Ramadhan na Maunga.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alidai watuhumiwa hao walikamatwa maeneo ya Mbagala na walipopekuliwa, walikutwa na Sh. milioni 332, Dola za Marekani 50,000 (Sh. milioni 114.898) na Euro 5,010 (Sh. milioni 11.513.

Mambosasa alisema watuhumiwa hao pia walikutwa na gari lenye namba za usajili T 134 DHY aina ya Toyota IST ambalo lilitumika kubeba fedha hizo wakati zikihamishwa kutoka kwenye gari la Kampuni ya G4S.

Baada ya mahojiano, alisema wawili hao walikiri kununua viwanja viwili maeneo ya Kisemvule na Kivule vyenye thamani ya Sh. milioni 25.

Kamanda Mambosasa alisema jumla ya mali na fedha taslimu walizokutwa nazo watuhumiwa ni Sh. milioni 357, Dola za Marekani 50,000 na Euro 5,010.

"Upelelezi uliendelea na juzi (Februari 24) mtuhumiwa Ibrahimu alikamatwa na baada ya kupekuliwa, alikutwa na Sh. milioni 195.2, Dola za Marekani 70,600 (Sh. milioni 162,236)," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema mtuhumiwa huyo pia tayari alikuwa amenunua nyumba ya Sh. milioni 30 Kibaha mkoani Pwani na samani za ndani zenye thamani ya Sh. milioni 10, akitumia fedha hizo za wizi.

Alisema jumla kuu ya mali na fedha alizokuwa nazo ni Sh. milioni 253 na kubainisha kuwa wamefanikiwa kuwakamata watuhumiwa wakuu wote watatu na mmoja aliyesaidia kukamilisha wizi huo.

"Tunawashikilia askari polisi tisa kwa kukiuka maadili ya kazi wakati wa ufuatiliaji na upekuzi wa tukio hili," alisema Kamanda Mambosasa.

Aliongeza kuwa askari hao wakati wa ukamataji, hawakuzingatia maadili na maelekezo waliyopewa na Mkuu wa Operesheni ya Ukamataji, Mrakibu wa Polisi Fadhili.

"Walipewa maelekezo wasubiri na kiongozi wa operesheni atakapofika, ndiye ataelekeza namna ya kufanya ukaguzi, lakini walianza upekuzi ambao siyo kwa mujibu wa utaratibu.

"Baadaye hicho kilichowasababisha wasisubiri kikaungwa mkono na mtuhumiwa wa kwanza, aliwalalamikia kwamba wamechukua baadhi ya fedha.

"Kwa kuwa kazi yetu ni kulinda maisha ya watu na mali, hatujali ni nani na anafanya nini, awe ni mtuhumiwa wa ndani, ofisa wa polisi, atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria, awe raia, hivyo hivyo," alionya.

Kamanda Mambosasa aliwashukuru waandishi wa habari kwa kuwa na subira kuhusu tukio hilo, akieleza kuwa angetoa taarifa hizo mapema bila kukamilisha ukamataji, angetoa nafasi kwa wahusika kujificha zaidi.

"Fedha hizi za Watanzania zisingerudi, ninazionya kampuni za ulinzi kuhusu ajira holela zinazofanyika, zinatusababishia haya, inasemekana mtuhumiwa wa kwanza alikuwa kwenye kampuni nyingine na alifanikisha hili.

"Haiwezekani kiwango kikubwa cha fedha kikasindikizwa na askari wawili na dereva na silaha mbili zibebe mzigo huu wa fedha, haya ni masihara na haiwezekani, hii ni njama na maandalizi yalianzia huko.

"Kwenye ile mitambo, wana uwezo wa kuona mwenendo wa gari linatoka benki hiyo jirani kwenda hapo, inawezekanaje? Mfuatiliaji wa mwenendo wa gari anaachaje na kukaa kimya? Gari likahama jirani tu hapo, likaenda hadi Temeke akakaa kimya?" Alihoji.

Kamanda Mambosasa alitamba kuwa Jeshi la Polisi halitamwacha yeyote aliyehusika kwenye wizi huo wa fedha na kwamba watawakomba wa ndani na nje ili wizi wa aina hiyo usijirudie tena.

Alisema fedha hizo ni za umma na zinapaswa kuwekwa mahali salama, akiahidi kutoa zawadi kwa askari polisi waliowezesha kukamatwa kwa mshtakiwa wa pili, watatu na wanne.

HABARI KITAIFA

# Mzee wa miaka 85 afungiwa mahubusu siku 3 bila chakula

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

MZEE wa miaka 85, Masanja Mahubi, anadaiwa kufungiwa kwa siku tatu katika ofisi ya serikali ya mtaa bila kupewa chakula na Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, Msoba Mligo.

Akizungumza kwa shida baada ya Jeshi la Polisi likiongozwa na Mkuu wa Jeshi hilo wilayani Igunga, Ally Mkalipa, kuuvunja mlango wa ofisi hiyo na kumtoa nje, Mahundi alisema alikuwa amechoka sana kutokana na kutokula chakula kwa muda wa siku tatu.

Alidai kuwa Februari 18 alikuwa ametoka Kijiji cha Iyogelo, Kata ya Kining'inila, alikokuwa amefuata ng'ombe wake waliokuwa kwa ndugu yake na alipofika mtaa wa Mwamaganga maeneo ya Mwanzugi, saa tatu usiku aliamua kulala.

Alisema katika harakati za kutafuta nyumba ya kulala alikutana na mwenyekiti huyo akiwa na vijana watatu ambao walimuhoji alikotokea na anakokwenda.

Mahundi alisema, licha ya kuwajibu walimchukua na kumfikisha ofisi ya serikali ya mtaa wa Mwamaganga, ambako alifungiwa ndani ya ofisi hiyo.

Alidai kuwa Februari 19, saa nne asubuhi akiwa amefungiwa kwenye ofisi hiyo alipewa kikombe cha chai na chapati mbili na alipomwomba mwenyekiti huyo amwachie, alimpa masharti kuwa kama anataka kutolewa nje atoe kitu kidogo.

Anaeleza kuwa Februari 20, saa nne asubuhi akiwa mahabusu ya ofisi hiyo, alisikia sauti za wananchi waliokuwa wanamtaka mwenyekiti huyo amfungulie kwa kuwa ilikuwa siku tatu akiwa mahabusu.

Mahundi alidai mlango wa ofisi hiyo ulivunjwa na polisi na yeye kutolewa nje.

"Mimi nilikamatwa na mwenyekiti na kisha kufungiwa ofisini kwa muda wa siku tatu bila kutoka nje wala chakula, bali kikombe kimoja cha chai na chapati mbili, namshukuru Mkuu wa Polisi Mkalipa kwa kuwa ilikuwa nifie humo, ameniokoa," alidai huku akibubujikwa na machozi.

Alipotakiwa kuzungumzia tuhuma hiyo, mwenyekiti huyo alikiri kumfungia mzee huyo ofisini kwa muda wa siku tatu.

Alidai kuwa hakuwa na funguo za ofisi hiyo ndiyo maana hakuweza kumfungulia haraka na kushindwa kueleza kisa cha kumkamata na kutompa chakula.

Baadhi ya wananchi wa mtaa huo, Kimwaga Juma, Issa Abihudi na Asia Clement, walidai mwenyekiti wao alikuwa na tabia ya kuwafungia ofisini wazee mpaka watoe kitu kidogo na kwamba hivi sasa hawana imani naye.

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Igunga, Ally Mkalipa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba polisi walipata taarifa kutoka kwa raia wema.

"Sisi tulipokea taarifa kutoka kwa raia wema na tulipofika tulimkuta mzee huyo akiwa amefungiwa ofisini na tulivunja mlango na kumtoa nje," alisema.

Jeshi la Polisi wilayani Igunga, lilimsafirisha mzee huyo kwenda nyumbani kwake.



Mwenyekiti wa Kamati ya Mikakati, Usimamizi na Ufuatiliaji ya Chama cha ACT-Wazalendo, Ismail Jusa (kulia), akipokea fomu kugombea nafasi ya kiongozi mkuu wa chama hicho, kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Omary Shaaban katika ofisi ndogo za chama hicho, Vuga mjini Zanzibar jana. **PICHA: ACT - WAZALENDO**

# Watumishi serikali watiwa mbaroni tuhuma za rushwa

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Mwanza, inatarajia kuwafikisha mahakamani watumishi wa nne wa serikali kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Mmoja wa watumishi hao ni kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) huku wengine watatu wakiwa watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (Mwauwasa).

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Stenga, alisema ofisa huyo wa TRA, Boniface Mwasamboma, alikamatwa na taasisi hiyo kwa tuhuma za kuomba rushwa ya Sh. milioni moja na kupokea Sh. 400,000 kati ya kiasi aliochoomba. Alisema kitendo hicho na kinyume cha kifungu 15 (1) (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

"Ofisa huyo wa TRA alichukua TIN (Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi) ya mfanyabiashara kisha akamwambia ili asimfungulie kesi, ampatie kiasi hicho cha fedha. Baada ya Takukuru kupata taarifa, tuliweka mitego yetu na kumkamata. Uchunguzi wa tuhuma hiyo umekamilika na tutamfikisha mahakamani mtuhumiwa," alisema Stenga.

Katika tukio lingine, alisema maofisa watatu wa Mwauwasa, wametiwa mikononi mwa Takukuru kwa tuhuma za matumizi ya nyaraka kwa lengo la kumdanganya mwajiri wao kinyume cha kifungu cha 22 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Thobias Kabwalo, aliyekuwa Meneja wa Fedha, Gadeni Chegele aliyekuwa Meneja Ufundi na Marco Mkungu aliyekuwa Mhasibu Msaidizi.

Mkuu huyo wa Takukuru alisema watuhumiwa hao walitumia nyaraka hizo na kujipatia zaidi ya Sh. milioni 26 fedha isivyo halali.

## Zitto apata wapinzani ACT

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Kamati ya Mikakati, Usimamizi na Ufuatiliaji ya Chama cha ACT-Wazalendo, Ismail Jusa, amechukua fomu kugombea nafasi ya Kiongozi Mkuu wa chama hicho.

Nafasi hiyo kwa sasa inashikiliwa na Mbunge wa Kigoma Mjini na mmoja wa waasisi wa chama hicho, Zitto Kabwe.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Ofisa Habari wa chama hicho, Suphian Juma, Jusa amekuwa mwanachama wa tatu kuchukua fomu kuwania nafasi hiyo, akitanguliwa na Zitto na Katibu wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Katavi, Joseph Mona.

Jusa ni mmoja wa makada waliojiunga na ACT-Wazalendo wakitoka Chama cha Wananchi (CUF), kutokana na kile walichoeleza kumuunga mkono aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad.

Maalim Seif aliihama CUF Machi 2018 na kujiunga na ACT baada ya kutofautiana na Mwenyekiti wa chama hicho, Profesa Ibrahim Lipumba.

Jusa (48), aliwahi kuwa mwakilishi katika Bunge la Wawikilishi Zanzibar na pia mbunge katika Bunge la Tanzania, alipoteuliwa na Rais wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete.

Mwanasiasa huyo pia aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa (CUF), ikidokezwa na wachambuzi wa masuala ya siasa nchini kwamba ni 'mwanafunzi mzuri wa Maalim Seif'.

Uchaguzi wa viongozi wakuu wa ACT-Wazalendo unatarajiwa kufanyika Machi 14 mwaka huu baada ya kukamilika kwa uchaguzi wa ngome za wanawake, vijana na wazee za chama hicho.



# Mkemia Mkuu ageukia wajasiriamali wadogo

**Na Mary Geofrey**

MAABARA ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) inatarajia kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo(Sido) kutoa elimu ya matumizi sahihi ya kemikali kwa wanafunzi wa ujasiriamali nchini ili kuwaepusha na madhara yanayosababishwa na kukosa elimu.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza katika warsha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kuhusu madhara ya kemikali na kuzifahamu sheria na kanuni zinazosimamia matumizi salama ya kemikali.

Warsha hiyo iliandaliwa kwa ushirikiano kati ya GCLA, Mamlaka ya Kupambana na Kuzuia Dawa za Kulevya (DCEA) na Sido.

Alisema kutokana na kuwapo kwa maoni ya wajasiriamali kuwa wanachelewa kupata mafunzo hayo ya matumizi salama ya kemikali kuna umuhimu wa kushirikiana kuanza kutoa elimu kuanzia wanapokuwa wakijifunza ujasiriamali.

"Suala hili ni zuri na tunaweza kushirikiana na Sido tukaona namna ya kuanza kutoa elimu ya usalama wa matumizi ya kemikali kabla kuanza kutumia bila tahadhari na kusababisha madhara kwao na jamii kwa ujumla," alisema Dk. Mafumo.

Alisema wana mpango wa kuanza kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara wanaouza kemikali ili kuwaeleza madhara ya kuuza bidhaa zilizomalizika muda wake.

Dk. Mafumiko pia aliwataka wafanyabiashara hao kujifunza namna ya kuzitambua bidhaa feki za zilizoisha muda wake ili kuwaepusha na madhara yatokanayo na matumizi mabaya ya kemikali.

Alitaja madhara ya kemikali zikitumiwa isivyokusudiwa ni kuwa sumu, kusababisha ajali, ulemavu, matatizo ya uzazi na saratani.

Awali wajasiriamali hao, waliishukuru GCLA kwa kuandaa mafunzo hayo na kuwataka yaanzie ngazi ya chini kwa wanafunzi ambao wanajifunza kufanya shughuli za ujasiriamali ili wajikinge mapema badala ya kusubiri hadi wapate madhara.

"Tunaishukuru GCLA mafunzo mazuri sana lakini changamoto iliyopo mafunzo yanachelewa kutufikia wakati ukiwa tushatumia kemikali na tukapata madhara ni muhimu yakaanzia vyuoni ili tuchukue tahadhari mapema," alisema mtengenezaji wa sabuni, Mary Lukas.

Alisema pia wanaomba kuwapo na ukaguzi wa kutosha kwenye maduka ya kuuza kemikali ili kuepuka kuuziwa bidhaa zilizoisha muda wake.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa jamii umuhimu wa kupata mafunzo kutoka Sido ili kuzalisha bidhaa zenye ubora na zinazokidhi viwango.




Kaimu Mkurugenzi wa Kampuni ya Mawasiliano (TTCL), Kezia Katamboi (kulia), akibadilishana mkataba na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kudhibiti Visumbufu katika Ukanda wa Kitropiki (TPRI), Dk. Margaret Mollel, baada ya kusaini mkataba wa huduma ya simu za mkononi ya T-HAKIKI kwa ajili ya wakulima kuhakiki viuatilifu vilivyosajiliwa jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Kigogo mwingine wa Chadema atua CCM

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo(Chadema) Jimbo la Bunda, Makina Josephat, amekihama chama hicho na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Amesema amechukua uamuzi huo kutokana na kuvutiwa na utendaji wa Rais John Magufuli.

Makina ambaye pia alikuwa Diwani wa Unyali wilayani Bunda, alipokewa katika ofisi za CCM mkoani Dodoma na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama hicho, Ismail Jama, kwa niaba ya Katibu Mkuu, Dk. Bashiru Ali.

Kiongozi huyo alisema amefikia uamuzi huo ili kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali chini ya Rais Magufuli, akidai alikuwa akifanya kazi kwenye mazingira magumu akiwa Chadema.

Makina alisema amehamasika kuungana na wapambanaji wazalendo wa nchi kuipigania nchi kwa kuwa alichokuwa anakipigania, amekiona kinafanyika CCM.

"Nimeona kwa nguvu zangu sina sababu ya kubaki upinzani, nikaona nijiunge na chama tawala nitumie nguvu zangu katika maendeleo ya nchi, Rais Magufuli amenivutia sana na kazi anayofanya kwa kuwa anakubalika na Watanzania tunamkubali," alisema.

Akizungumza baada ya kumpokea kiongozi huyo, Jama alisema hatua ya kupokea wanaohamia CCM ni mwendelezo kwa kuwa wanaunga jitihada za zinazofanywa na serikali katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

Juzi, Katibu Mkuu alipokea madiwani 11 wa Chadema wakiongozwa na Meya wa Jiji la Mbeya, David Mwashilindi, sababu ikitajwa kuwa kuunga mkono jitihada za Rais Magufuli.

# Wataalamu SADC wajadili umeme

**Na Gwamaka Alipipi**

WATAALAMU na makamishna wa masuala ya nishati kutoka nchi 12 za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc), wamekutana jijini Dar es Salaam kujadiliana namna na kuboresha nishati jadidifu kwa nchi wanachama hususani upatikanaji wa umeme wa uhakika maeneo ya vijijini.

Vilevile, watajadiliana kuhusu uanzishaji wa kituo cha umahiri cha kuendeleza nishati na matumizi bora ya nishati, matumizi ya gesi asilia kwa nchi hizo.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao hicho, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Zena Saidi, alisema mkutano huo ni sehemu ya mwendelezo wa vikao vya Sadc nchini, unahusisha wataalamu, wakurugenzi, makamishna kutoka nchi 12 ya jumuiya hiyo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa uamuzi uliopitishwa na mawaziri wanaohusika na masuala ya nishati na wakuu wa nchi.

Pia watajadiliana kuhusu kuboresha vyanzo vya umeme kama mabwawa ili kuwapo na upatikanaji wa umeme wa uhakika katika ukanda wa Sadc.

"Kwa mfano kwa sasa Tanzania inatengeneza mradi wa kuzalisha umeme wa Nyerere, utakapokamilika tunaweza kuuza umeme wa ziada katika nchi za Sadc, tunataka bei ya umeme ipungue, tunataka matumizi ya mkaa yapungue, tunataka uhifadhi wa mazingira uboreshwe," alisema Saidi. Kuhusu upatikanaji wa umeme katika nchi za Sadc hasa vijijini, alisema upo chini ya asilimia tano, hivyo kuna haja ya kuongeza upatikanaji wa umeme katika maeneo hayo.

Naye Kamishna wa Nishati na Gesi wa Wizara ya Nishati Tanzania, Adam Zuber, alisema wataalamu hao pia watajadiliana masuala ya nyuklia, kufanya mapitio, kujadiliana utekelezaji wa miradi mbalimbali kama vile uanzishaji wa kituo cha umahiri cha kuendeleza nishati jadidifu na matumizi bora ya nishati kwa nchi hizo.

"Kamati ya Nishati ya Sadc, wamekutana ikiwa ni utekelezaji wa maamuzi ya marais, wanachama 12 wamehudhuria, na kituo hicho kitaanzishwa baada ya kupata uhalali wa wanachama 11 kati ya 16 wa jumuiya hiyo, kwa sasa ni nchi nane ambazo zimeshasaini uanzishwaji wa kituo hicho," alisema Zuber.

Mkurugenzi wa Miundombinu wa Sadc, Mapolao Makoena, alisema mojawapo ya agenda itakayojadiliwa kwa undani ni mabadiliko ya protokali ya nishati, kwamba maamuzi yake yatapelekwa kwa mawaziri ambao nao watayawasilisha kwa marais wa nchi.

Mkutano wa 39 wa Jumuiya ya Sadc, ulifanyika Agosti mwaka jana jijini Dar es Salaam pamoja na mambo mengine Rais John Magufuli alikabidhiwa uenyekiti wa jumuiya hiyo baada ya Rais wa Namibia, Hage Geingob kumaliza muda wake.

HABARI KITAIFA

# Mhagama afunguka kuhusu mkandarasi Daraja Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amesema mkandarasi anayejenga kipande cha barabara katika Daraja la Nyerere, atawasilisha mpango kazi wake serikalini.

Waziri alisema hayo alipofanya ziara ya kushtukiza katika kipande cha barabara kilichopo katika Daraja la Nyerere lililopo Kigamboni, Dar es Salaam, kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Rais John Magufuli, aliyeagiza kipande cha barabara hiyo yenye urefu wa kilomita mbili kikamilike.

Kipande hicho cha barabara kinajengwa na kampuni ya ujenzi ya China Railway Construction Engineer Group.

Waziri Mhagama alisema kazi inayoendelea sasa katika eneo hilo ni ya kufanya mapitio ya ujenzi ambayo mkandarasi anaikamilisha.

"Mkandarasi atawasilisha mpango kazi wake ili sasa mshauri mwelekezi wetu ambaye ni Tanroads (Wakala wa Barabara Tanzania), kuiangalia na kuidhinisha ili kama kweli huo mpango kazi uko sawa sawa kwa kuzingatia kazi zilizobakia," alisema.

Alisema watahakikisha maagizo hayo ya Rais ya kukamilisha kipande hicho cha barabara chenye urefu wa kilomita mbili yanatekelezwa kwa gharama ileile.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), William Erio, alisisitiza kuwa lengo la ziara hiyo ni kuangalia nini kinachoendelea.

Alisema walipata taarifa ambazo sio rasmi kwamba kuna hali ya kusuasua, hivyo waliona ni vema kwenda kujionea utekelezaji wa maagizo hayo.



Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya NMB, Mkoa wa Dodoma, wakiwa kwenye kampeni ya upandaji miti eneo la Area C, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Miti 500 ilipandwa ili kuunga mkono kampeni ya serikali ya kutunza mazingira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwakilishi wa Chansela Ujerumani atembelea Makumbusho ya Taifa

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKILISHI wa Chansela wa Ujerumani anayeshughulikia Afrika, Guenter Nooke, ametembelea Makumbusho ya Taifa jijini Dar es Salaam na kufurahishwa na maonyesho yaliyopo katika Makumbusho hiyo.

Nooke alikuwa ameongozana na Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regine Hess, na Dk. Rainer Hoening, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Batteri ya Ujerumani.

Makumbusho ya Taifa walikutana na Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho, Dk. Noel Lwoga, Mkurugenzi wa Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni, Achiles Bufure pamoja na Mhifadhi Mkuu wa Makumbusho, Dk. Amandus Kweka.

Mwakilishi huyo anayeshughulikia Afrika, alitembelea ukumbi wa Chimbuko la Mwanadamu, Ukumbi wa Historia, pamoja na Onyesho la Mchango wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika ukombozi wa Afrika ambalo limepangwa katika ukumbi wa muda.

Akizungumza baada ya kutembelea kumbi hizo, Nooke alisema maonyesho ni mazuri na ameyafurahia.

## Uhakiki viuatilifu sasa kielektroniki

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Mawasiliano Tanzania (TTCL Corporation) na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Ukanda wa Tropiki (TPRI), zimeingia makubaliano ya maandalizi ya uzinduzi wa mfumo wa kuhakiki viuatilifu kwa kutumia teknolojia ya kielektroniki.

Mfumo huo uliopewa jina la 'T-Hakiki' ni huduma ya simu ya mkononi ambayo itamwezesha mkulima kupata taarifa ya kiuatilifu kilichosajiliwa na kwa matumizi sahihi ili kuleta tija katika kilimo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam katika hafla ya kusaini mkataba wa makubaliano, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TTCL Corporation, Kezia Katamboi, alisema baada ya makubaliano hayo, utoaji wa huduma hiyo unatarajiwa kuanza mwezi ujao ikiwa ni baada ya kukamilisha baadhi ya taratibu zinazotakiwa.

Alisema makubaliano hayo ni muhimu kwa maendeleo ya sekta ya kilimo, ufugaji na viwanda.

Alisema hii ni hatua kubwa katika kulinda bidhaa za kilimo na ufugaji kwani itahakikisha wakulima na wafugaji wanapata mavuno yanayostahili.

"Kwa kupitia mfumo huu ambao utatumia mawasiliano ya TTCL Corporation utakuwa suluhisho la kuondoa viuatilifu feki sokoni na kuongeza kasi ya matumizi ya viuatilifu sahihi vya kilimo na ufugaji kwa kuwa mtandao wa TTCL Corporation umeenea nchi nzima hivyo wakulima wote nchi nzima watanufaika na mradi huu.

Aidha, Mkurugenzi wa Biashara Quincewood ambayo inasimamia mfumo huo wa kuhakiki viuatilifu kwa kutumia teknolojia ya kielektroniki, Fatma Fernandes, alisema sekta ya kilimo ni muhimili wa maendeleo ya uchumi.

"Sekta hii inachangia kiasi cha nusu ya pato la Taifa, robo tatu ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi na chanzo cha chakula pamoja na utoaji wa fursa za ajira zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania.

"Kilimo kina uhusiano na sekta zisizo kuwa za kilimo kupitia uhusiano wa usafishaji kwenda kwenye usindikaji wa mazao ya kilimo, matumizi ya ndani, uuzaji nje ya nchi na uzalishaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu."

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti na Udhibiti wa Viuatilifu katika Ukanda wa Kitropikia, Dk. Margaret Mollel, alifafanua kuwa huduma hiyo ya "T-Hakiki" itamwezesha mkulima kupata taarifa kuhusu viuatilifu vilivyosajiliwa na vyenye ubora unaotakiwa kwa kutumia hapo alipo kwenye sehemu yake ya kilimo.

"Pia itamwezesha kujua matumizi sahihi ya viuatilifu kulingana na visumbufu lengwa kwa kuwasiliana na mamlaka ya TPRI pamoja na wamiliki wa viuatilifu na kutoa taarifa sahihi kwa TPRI kuhusu viuatilifu ambavyo havina ubora kwa ajili ya ufuatiliaji na kuchukua hatua," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Usajili utaleta mazingira rafiki shughuli za udalali*

SERIKALI imesema kuanzia sasa hakuna dalali atakayeendesha shughuli hizo bila kujisajili na kuwa na leseni.

Hatua hiyo ilitangazwa juzi jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, alipokuwa akizindua mfumo wa utoaji leseni za udalali na uendeshaji minada kwa njia ya kielektroniki.

Alisema tayari shughuli hizo ni rasmi na wanaotakiwa kuziendesha ni waliosajiliwa pekee, na kwamba wamejipanga kuanza kufanya opareshini katika kila mtaa maeneo mbalimbali nchini kuwakamata madalali ambao hawajajisajili

Pia alisema madalali feki wote watakaokuwa wanakamatwa kufanya shughuli hizo bila kuwa na leseni, watakuwa wanatangazwa kwenye vyombo vya habari.

James alisema kama mtu anajiita ni dalali na anafanya shughuli hizo bila kujisajili, mwisho wake umefika na kwamba serikali ina mbinu mbalimbali za kufanya shughuli zake.

Katibu Mkuu huyo alisema watapita mitaani wanapofanyia shughuli hizo bila kujisajili na kuwakamata watakaokutana nao bila huruma kisha kuwafikisha mahakamani.

Alifafanua kuwa madalali hao feki wamekuwa wakiwatapeli watu kwa muda mrefu, hivyo kusababisha madalali halali waliojisajili kulipa kodi serikalini nao waonekane ni matapeli.

Watu wengi wanaofanya shughuli za udalali katika meneo mengi nchini bila kusajiliwa bila shaka hawatafurahishwa na hatua hii, ingawa sisi tunaona kwamba ni hatua yenye malengo mazuri.

Miongoni mwa malengo hayo ni serikali kuwatambua madalali, shughuli zao na mahali wanapofanyia kazi zao. Pili ni kuweka mazingira mazuri ya shughuli za udalali kwao na watu wanaohitaji huduma hizo ikiwamo kudhibiti vitendo vya utapeli.

Tatu, kuwasajili kutawafanya madalali nao wachangie kuingizia mapato serikali kupitia kodi stahiki ambayo mamlaka husika zitawapangia.

Kimsingi, kazi za udalali kwa muda mrefu zimekuwa zikifanyika kiholela bila kuwapo usimamizi wa serikali, hivyo wengi wa madalali kuzigeuza kuwa kichaka cha kufanya utapeli na kutochangia katika mapato ya serikali.

Madalali wengi hawatambuliki rasmi kutokana na kutokuwa na maeneo rasmi ya kufanyia kazi, badala yake wamekuwa wakikaa mitaani na kwenye vijiwe, hali inayosababisha iwe vigumu kuwafuatilia hata inapotokea wakawatapeli watu.

Licha ya kutojulikana wala kulipa kodi, ukweli unabaki pale pale kuwa madalali ni wengi na wanapata kipato kizuri kutoka kwa wateja wanaohitaji huduma muhimu kama nyumba, vyumba, viwanja, mashamba, kwa kutaja baadhi.


Madalali wamekuwa wakijipatia asilimia kumi kwa wateja wao baada ya kufanikisha mahitaji yao, hivyo kudai kuwa sekta hiyo haina fedha ni uongo.

Tunaona kwamba serikali imefanya jambo jema sana kuibua chanzo hicho kipya cha mapato sambamba na kutaka watoa huduma hao kusajiliwa ili watambulike kwa lengo la kuiwekea mazingira bora kulinganisha na huko nyuma.

Tunasema hivyo kwa kuwa huko nyuma madalali na watu wao wa karibu pamoja na familia zao walionekana ni matapeli kutokana na shughuli zao kutokuwa na uwazi.

Tunatarajia kuwa watu wote wanaojihusisha na kazi za udalali wataitikia wito wa serikali wa kujisajili kwa ajili ya kutoa huduma hizo katika mazingira rafiki na ya uwazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



### Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Siku Wanawake Duniani ichochee usawa wa kijinsia

**MACHI** 8 kila mwaka, huwa ni siku ya kimataifa ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani inayoangazia masuala yanayohusu wanawake katika harakati mbalimbali, hasa za masuala ya usawa wa kijinsia.

Wiki mbili zijazo, Tanzania itaungana na nchi nyingine wanachama wa Umoja wa Mataifa, katika maadhimisho hayo yenye kaulimbiu usemayo: "Kizazi cha Usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya Sasa na Baadaye"

Serikali imetoa maelekezo kuwa maadhimisho yafanyike ngazi ya mkoa, kutoa wigo kwa wanawake, wadau wengine kutathmini hatua ambazo taifa limefikia katika masuala ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake na wasichana.

Kimsingi usawa wa kijinsia ni moja ya mambo muhimu na unahamasishwa, ili kuhakikisha hakuna ubaguzi kwenye jamii katika kushiriki shughuli mbalimbali za maendeleo zikiwamo za uzalishaji mali.

Kutokana na umuhimu wa usawa wa kijinsia, baadhi ya nchi zimekuwa zikifanya juhudi za kuwapa wanawake nyadhifa kubwa za uongozi ili kwamba waweze kutoa mchango wao katika kuongoza.

Tanzania inatajwa kuwa ni miongoni mwa za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), ambayo imewezesha wanawake kujikita zaidi katika kujiwezesha kukuza mitaji na kuinua uchumi wao.

Hii ni kwa mujibu wa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kwamba Tanzania imepiga hatua kubwa katika kutambua sheria za usawa wa kijinsia.

Ni katika moja ya hotuba zake wakati akizindua machapisho ya kuimarisha usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake kwa nchi za SADC, kwamba masuala ya kuwawezesha wanawake katika sekta mbalimbali yanaonekana.

Anasisitiza kuwa serikali inatambua uwepo wa usawa wa kijinsia na uendelezwaji wanawake nchini na kwamba hilo limetambuliwa katika Katiba ya nchi kama suala muhimu kwa haki za binadamu.

Wakati huu ambao dunia inaelekea katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ni muhimu kutambua kuwa haiwezekani kuwa na mafanikio katika jamii iwapo baadhi ya makundi yataachwa nyuma, hasa wanawake.

Ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi na uongozi ni suala muhimu, lengo likiwa ni kuhakikisha maendeleo yanaletwa na Watanzania wote bila kubagua ikiwa ni njia mojawapo ya kufikia usawa wa kijinsia.

Ni kweli kwamba wanawake nchini, wamekuwa wakiwezeshwa kielimu na kushirikishwa katika ngazi za maamuzi na uongozi, siyo vibaya kasi hiyo ikaongezeka ili kupata wanawake wengi zaidi katika ngazi za maamuzi.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu iwe ni chachu ya kufikia kile ambacho serikali imekusudia kwa ajili ya usawa wa jinsia nchini na pia kumaliza ukatili wa kijinsia unaoendelea kwenye baadhi ya jamii.

Serikali ilishaandaa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto kwa lengo la kupunguza kiwango cha ukatili kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

Hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia (2005); Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008); Sheria ya Makosa ya Kujamiiana -(1998).

Serikali inaamini utekelezaji wa mpango huo utachangia katika utekelezaji wa mipango na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake na wasichana pamoja na haki na ustawi wa mtoto.

Kwa kawaida binadamu huzaliwa na jinsi ya kike au kiume, na jinsi hizo ni tofauti ya kibaologia, lakini hazihusiani na nani kati ya mwanamke au mwanamume ni wa hali ya juu zaidi ya mwingine.

Kwa hiyo serikali inapochukua hatua mbalimbali za kuhakikisha usawa wa kijinsia unakuwapo na pia kutokomeza vitendo vya ukatili wa jinsia, jamii haina budi kuunga mkono hatua hizo.

Ninasema hivyo, kwa sababu uhusiano uliyopo umejengwa na jamii yenyewe (wanaume na wanawake), lakini unaweza kubadilishwa na ukaleta usawa wa kijisia iwapo jamii itabadilika.

Ikumbukwe kwamba udhalilishaji kijinsia hutokea pale tafsiri za jamii kuhusu haki, wajibu na majukumu inapoashiria kujenga tabaka au 'mapengo' kati ya mwanamke na mwanamume katika ngazi mbalimbali.

## BARUA/MJADALA

# Ninaomba mwongozo wa serikali

**Ndugu Mhariri,**

*NAMI nitoe pongezi zangu kwa Gazeti la Nipashe kwa kazi kubwa inayofanyika ya kuielimisha jamii kupitia habari na taarifa mbalimbali zinazovuta wasomaji.*

*|Ninapenda kulalamika kuwa kuna jambo ambalo serikali hulipuuza sana licha ya kwamba linatukera, nalo ni wenye magari na pikipiki kufungua mabomba ya kutolea moshi (muffler) na kusababisha kelele ambazo zinatukera mno.*

*Naamini wanamazingira wanafahamu kuwa sauti za juu ni moja ya kero ambazo zinachafua mazingira kwa hiyo tunaziomba mamlaka zinazohusika kupiga marufuku kelele hizo ambazo pamoja na kuchafua mazingira zinatukera na kustua watu wengi.*

*Pengine ni vyema hata Wakala wa Barabara (Tanroads) na Mamlaka ya Usafirishaji Ardhi (Latra), wakaingilia kati kukomesha kero hii.*

***Mwananchi mwathirika***
***Ubungo , DSM.***

# Tunaomba msaada Breakdown hizi barabarani ni aibu

*WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi pamoja na wa Mambo ya Ndani tuna heshima kubwa kuwaeleza kuwa sisi wenye magari tunakerwa na huduma mbovu na ya kizamani na iliyopitwa na wakati ya breakdown.*


*Ni kero kuona minyororo na magurudumu yaliyochakaa yakikokota magari yetu ya thamani . Hivi viongozi wetu pamoja na polisi na wadau wengine wanaohusika na breakdown hawaoni kuwa magari haya tena mabovu hayafai kutumika kwenye barabara zetu, licha ya kutumiwa kukokota magari?*

*Tunaomba serikali iliangalie hili na ichukue hatua kwa kuondoa magari hayo na kuagiza wafanyabiashara kuleta huduma za kisasa za breakdown na hizo gari mbovu zipelekwe Makumbusho ya Taifa.*

***Sudi Nassoro Mpogole***
***Iringa.***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Kusajili daftari la kudumu kutaleta pia viongozi bora

**Na Mwandishi Wetu**

OKTOBA 25 miezi tisa kuanzia sasa Watanzania watapiga kura kwenye uchaguzi mkuu, utakaowapatia madiwani, wabunge na marais wa Jamhuri ya Muungano na wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hivyo kwa sababu maalumu labda uwe ugonjwa au safari nje ya nchi ni muhimu mwenye sifa ya kupiga kura akajiandikishe hivyo ni vyema kujitokeza kujiorodhesha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura linalotumia mashine za kielektroniki za BVR.

Wananchi wanatakiwa kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huo ili kujipatia viongozi watakaoleta mabadiliko na maendeleo si kisiasa pekee bali kwenye Nyanja na sekta zote muhimu, ikiwamo kusaidia kupunguza kama si kumaliza umaskini .

Wananchi wakumbuke kuwa ni wajibu wao tena haki ya msingi kuwachagua viongozi ambao watapatikana miongoni mwa wagombea wote watakaopendekezwa na vyama vyao, kisha waone ni yupi akikaa madarakani anaweza kuliongoza taifa kwa maslahi ya umma na wote wakanufaika badala ya kulihudumia tumbo lake au chama chake na au hata kundi fulani la wapambe wake.

Kushiriki kwenye uchaguzi kutawezekana tu kama watu wamejiandikisha kwanza kwenye daftari la kudumu la kupiga kura.

Vyama vya siasa navyo visiwakwaze wananchi viweke wagombea ambao wapigakura watakapowachagua wawe wataalamu na mahiri watakapowaweka kuwa viongozi madarakani waongze nchi kwa haki, amani na weledi.

Wawe tayari kutetea haki na maslahi ya umma na kuunga mkono haki za binadamu, kuheshimu makundi yote kuanzia wenye ulemavu, wazee, watoto, vijana , wanawake na raia wote.

Ni vyema wale wenye nia ya kugombea uongozi wakaingia kwenye uchaguzi huku wakiwa na unafahamu kuwa Tanzania inaongozwa na katiba hivyo kuheshimu sheria na katiba liwe suala muhimu katika kuchagua kiongozi na kuliongoza taifa.

Viongozi watakaochaguliwa wajue wana kazi ya kufanya kwa kuwa kila Mtanzania analo la kuzungumza kuhusu vile anataka serikali atakayoichagua ifanye nah ii ni kutokana na ukweli kuwa awamu ya tano imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa umakini na uadilifu ili kuondokana na mazoea ya kuendesha nchi huku wachache wakinufaika na wengi wakibakia kuwa maskini.

Kujiandika kwenye daftari kuhakikishe kuwa hakuna kuchagua viongozi wanaohonga. Wanaotoa pesa za umma ili kupata madaraka.

Tunawasikia wadau mbalimbali wakiliombea taifa liwe na uchaguzi bora na kupata watendaji waadilifu, ni vyema pia kuomba Mungu azuie viongozi wabovu wanaopata uongozi kwa njia ya rushwa na matendo maovu.

Ikumbukwe kuwa anayetoa rushwa ili achaguliwe hatakuwa na mamlaka au maadili ya kukemea rushwa, ubadhirifu , upendeleo na kulindana. Atakuwa daima wa kulinda uovu ili adumu katika nafasi aliyojiwekea kwa kuhonga.

Viongozi wanaochaguliwa wakumbuke kuwa na nia safi kwa watu waliowachagua na lengo lao liwe kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania kwani hilo linawezekana.

Hapa ni lazima ashiriki kuwapatia wapiga kura wake kazi ili wapate riziki, awe mjasiriamali wa kubuni na kuwawezesha wananchi kumudu maisha yao kwa kuwashirikisha kwenye mambo mbali hasa kwa kutumia rasilimali walizo nazo.

Viongozi wanaotarajia kugombea na kuchaguliwa baada ya wananchi kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la kupiga kura wasaidie kuwa na ujasiriamali na viwanda ili baada ya miaka mitano kilo moja ya sukari inunuliwe kwa Shilingi 500 badala ya 3,000 za sasa.

Hii itawezekana iwapo viongozi watakaochaguliwa baada ya wananchi kujiandikisha kwenye daftari la kupiga kura watakuwa wabunifu wa kushiriki kazi za uzalishaji mali na kujenga viwanda vikiwamo vidogo na vikubwa vijijini ili kuzalisha bidhaa za aina mbalimbali.

Ninachotaka kusema hapa ni kwamba uadilifu wa mtu ni muhimu na uchapakazi nao ni lazima ili kutatua matatizo ya wapiga kura.

Ieleweke wazi kwamba Watanzania wa kawaida ambao hawapendi kuishi chini ya dola moja ( Shilingi 2,300) kwa siku wanalazimika kufanya hivyo kwa sababu viongozi wao hawajawasaidia kikamilifu kuondoka kwenye matumizi hayo ya ya chini.

Tena ni vyema ikumbukwe kuwa wapiga kura wenu hawafurahii kununua sukari na sembe kwa pesa nyingi ndiyo maana wanaishia kwenye kununua nusu na robo.

Kwa hiyo viongozi wanaotaka kuchaguliwa 2020 , waamke na kujituma ili kuwaondolea na kumaliza tatizo la kununua bidhaa kwa kipimo cha robo kilo kwa kila kitu kuanzia sukari, maharage, nyama na unga.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Makonda kuwamaliza matapeli wa ardhi

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameahidi kuwamaliza matapeli wa ardhi mkoani kwake kabla ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, mwaka huu.

Makonda alitoa ahadi hiyo jana jijini Dar es Salaam katika kikao cha Kamati ya Ushauri Mkoa.

Alisema watu hao wamefanya utapeli wa kuwapimia wananchi viwanja na kudai kuwa na vibali vyote na wananchi wametoa fedha zao ili wapate hati.

"Kumbe ni matapeli na hawana uhusiano na mkoa, wilaya wala wizara, mchakato wa kuwakamata umeanza tangu jana (juzi), tuna matumaini ya kwamba matapeli wa aina hii wanaohusika katika sekta ya ardhi tunaweza kuwamaliza kabla ya uchaguzi mwaka 2020," alisema.

Alisema mkoa unataka wananchi wamiliki ardhi zao kwa utaratibu na pasipo shaka badala ya mtu kujenga kesho anabomolewa kwa kuambiwa amejenga kiwanja cha mtu mwingine.

Kadhalika, alisema ofisi yake imeendelea kupokea malalamiko ambayo mpaka sasa yamefikia 8,548 yanayohusu ardhi, mirathi, utapeli wa magari na baadhi yake kesi zipo mahakamani.

Katika hatua nyingine Makonda alisema ufanyaji wa biashara saa 24 katika soko la Kariakoo, utaanza wakati wowote kuanzia sasa.

"Ninapendekeza suala hili lianze wakati wa Ramadhani ili tutumie wakati huo kuzindua Kariakoo ya usiku na mchana, kwa hiyo mamlaka zinazohusika kuanzia polisi, Wilaya ya Ilala mmeshiriki na mnakazi ya kukamilisha ikiwa ni pamoja na ufungaji kamera," alisema.

Pia aliwataka wafanyabiashara waanze mkakati wa kujiongezea ulinzi kwa kufunga taa na kamera za kutosha katika biashara zao.



Watoto wanaolelewa katika kituo cha Amazing Steps, kilichoko wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani, wakiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wa Taasisi ya Time to Help ya Uholanzi na viongozi wa shule za Feza, waliokarabati kituo hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatoa wiki 2 kampuni simu kuchunguzwa vifurushi

**Na Futuna Seleman**

SERIKALI imetoa wiki mbili kwa Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA), kuzichunguza baadhi ya kampuni za simu nchini zinazoshutumiwa kukata ovyo bando za vifurushi vya muda wa maongezi kabla ya muda wa matumizi ili hatua stahiki zichukuliwe.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, alipohojiwa na vyombo mbalimbali vya habari baada ya kuzindua mnara wa mawasiliano uliojengwa na Kampuni ya simu ya Tigo, kijiji cha Mavuji, wilayani Kilwa, mkoani Lindi na mnara wa simu uliojengwa na Kampuni ya Halotel, katika kijiji cha Mbunju, Mvuleni kata ya Mkongo, wilayani Rufiji, mkoani Pwani baada ya kupokea ruzuku kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa wote.

Alikuwa akitoa ufafanuzi kuhusu ya malalamiko aliyoyapokea kutoka makundi mbalimbali manung'uniko ya matumizi ya mawasiliano ya baadhi ya kampuni za mitandao ya simu nchini kuwadhulumu na kuwaibia wananchi.

"Naagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ndani ya wiki mbili mniletee ripoti ya uchunguzi wenu kwanini hiyo kampuni (bila kuitaja) inashutumiwa kuanzia bungeni, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya kumi na moja, wananchi wote wanalalamika kuwa wakiweka hela kidogo zinaisha tatizo la muda mrefu," alisema na kuongeza;

"Lazma mfuate matumizi yakoje, vigezo na masharti yakoje, muone kama vinakidhi sheria na matumizi yenu ya TCRA, lakini pia muweze kuchukua hatua stahiki, tunahitaji wananchi wawasiliane vizuri bila matatizo yoyote ili mawasiliano yawaletee maendeleo na ulinzi wa maisha yao badala ya kuwaongezea gharama za matumizi."

Mhandisi Nditiye alisema suala la mabando kampuni nyingi zinatoa hapa na pale, watu wanajaribu kuhoji kama mtu amenunua bando la wiki inakuwaje wiki moja liishe halafu hilohilo ananunua wiki nzima hajatumia anapokea ujumbe limeisha, jambo ambalo alisema TCRA inapaswa kulishughulikia.

"Moja ya kazi ya TCRA ni kuwadhibiti hao watu 'wa regulate' (wadhibiti) kuhakikisha wanawatendea haki Watanzania, tunahitaji wa hali ya chini watumie mawasiliano kwa faida na bei nafuu na yanayopatikana kwa uhakika zaidi, hatuhitaji blah blah za kampuni za simu katika hilo, TCRA ndani ya wiki mbili mniletee ripoti ya uchunguzi wenu," alisema Nditiye.

Aliitaka TCRA CC kujitangaza vya kutosha ili wananchi wajue mahala pa kukimbilia kama hawatendewi haki katika mawasiliano.

Hata hivyo, alisema inawezekana wananchi ambao ndio watumaiji wa huduma za mawasiliano, hawajui namba ya TCRA CC, kwavile bado TCRA haijajitangaza vyema kwa wananchi wajue wakalalamikie wapi.

"TCRA CC haijajitangaza vya kutosha kwa wananchi ili wajue kumbe mtetezi wao kuhusu matumizi ya mawasiliano ni yeye TCRA CC kwasababu haiwezekani wananchi walalamike kwa waziri kuwa wanaibiwa na wanadhulumiwa na kuibiwa fedha zao wakati mtetezi wao yupo," alisema.

"Lakini pia hili jambo niwaambie TCRA sio la kuwaachia TCRA CC peke yao, TCRA inatakiwa kuingilia kati haiwezekani mtu ajiunge bando la shilingi elfumbili hata kabla hajapiga aambiwe ame download (pakua) vitu, haiwezekani lazima vigezo na masharti ya kampuni mbalimbali za simu za mkononi ziainishwe ziwe wazi ili wananchi wachague vigezo gani na masharti ya kampuni ipi ajiunge naa akikubali ajue consequence (matokeo) za kutumia, lakini TCRA lazima iwadhibiti hao watu," alisema.

Pia, alisema tayari serikali imetoa vitabu vya miongozo kwa watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano kwa wabunge, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya zote, madiwani na wana mpango wa kuvisambaza kwa watendaji wote wa kata ili wananchi wavitumie kudai haki zao.

## Aiangukia serikali udhibiti viwavi jeshi

**Na Faustine Feliciane, MOROGORO**

MENEJA shamba wa Shirika la Kuendeleza Kilimo Hai Tanzania (SAT), Frank Maro, ameishauri serikali kuongeza nguvu ya kukabiliana na wadudu waharibifu mashambani kama vile viwavi jeshi kwa kutoa mafunzo maalum kwa maofisa ugani ili kudhibiti makundi ya wadudu hao.

Wadudu hao ambao ni kero kwa wakulima wengi nchini, wamekuwa wakivamia mazao mbalimbali hususani mahindi na kusababisha hasara kwa wakulima, akieleza kuwa inakadiriwa hupunguza uzalishaji wa mazao kwa wastani wa asilimia 87.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye mafunzo ya waandishi wa habari za kilimo hai, meneja huyo alisema baadhi ya maofisa ugani wanashindwa kuwadhibiti viwavi jeshi kwa kuwa hawana uelewa wa kutosha kuhusu wadudu hao.

"Ili kukabiliana na kitu chochote, lazima kwanza kukielewa hicho kitu, kuwadhibiti mapema viwavi jeshi na wadudu wengine kwanza ni muhimu kufahamu tabia zao na namna wanavyoanza kushambulia mazao kabla hawajaanza kukomaa. Viwavi jeshi wanapitia hatua nne za ukuaji," alisema.

Maro alibainisha kuwa hatua ya kwanza ni kutaga mayai kuanzia 2,400 hadi 8,000 kwa wiki na huyataga chini ya majani la mmea, hivyo ni vigumu mkulima kugundua kwa haraka.

Aliendelea kufafanua kuwa viwavi jeshi wakishataga mayai hayo, huyagandisha kwa ute wanaoutoa mdomoni kuyafanya mayai kuganda chini ya jani la mmea kuyawezesha kutoanguka pindi mvua inaponyesha.

"Hatua ya pili mayai hugeuka kuwa lava ambapo huanza kushambulia mahindi juu kwenye mbelewele kisha kuingia ndani ya mche," alisema.

Mtaalamu huyo alisema katika kipindi hicho mahindi hushambuliwa kwa kasi na ni ngumu kuwadhibiti kwa sababu katika hatua hiyo wameshaanza kukomaa kwa kuwa na ngozi ngumu.

"Hatua hiyo hata mpulizie dawa, ni vigumu kufa kwa sababu ngozi yake imeshakuwa ngumu na anaelekea kugeuka kuwa buu ambalo linakuwa na gamba gumu ili kwenda hatua ya tatu ya ukuaji kisha baada ya hapo hugeuka kuwa kipepeo ambayo ni hatua ya nne," alisema.

Aliongeza kuwa madhara ya wadudu hao shambani yamekuwa makubwa hivyo kuna haja maofisa ugani kupewa elimu ya kutosha kuwatambua na namna ya kuwadhibiti wadudu hao.

Alisema njia rahisi kuwadhibiti viwavi jeshi shambani ni wakiwa kwenye hatua ya kwanza na ya pili kwenye ukuaji, lakini baada ya hapo wanakuwa sugu na ni ngumu kufa kwa kupuliziwa dawa.

Maro alieleza kwa njia za asili ambazo mkulima anaweza kutumia kuwadhibiti ni kutumia maji yaliyotokana na mchanganyiko wa unga wa majani ya mwarobaini, pilipili, arovela, mafuta ya kupikia ya alizeti na maji hayo yanyunyuziwe shambani kabla ya mbelewele za mahindi hazijaanza kuchomoza.

Alisema wadudu hao vamizi kwa mara ya kwanza waliingia nchini miaka ya 2000 wakitokea mataifa ya Amerika Kusini na wamesababisha madhara makubwa kwa wakulima, wakishambulia mahindi, ngano, ulezi, pamba, mtama, tumbaku, viazi na mpunga.

# Polepole sasa aagiza umeme, maji Pemba

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

SHIRIKA la Umeme Zanzibar tawi la Pemba limetakiwa kuweka transfoma nyingine mpya katika Kisiwa cha Kojani Wilaya ya Wete ili wananchi wa kisiwa hicho waweze kunufaika na nishati hiyo muhimu.

Wito huo ulitolewa na Katibu wa Itikadi na Uenezi Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, alipokuwa akizungumza na wana-CCM na wananchi wa kisiwa hicho, baada ya kukagua Shule ya Sekondari ya Kojani, ukiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa ilani ya CCM kisiwani Pemba.

Polepole alilitaka shirika hilo kuhakikisha ndani ya siku 36 kuanzia sasa transfoma hiyo iwe imeshafungwa ili kuondoa tatizo lililopo hivi sasa.

Alisema lengo la Serikali ya CCM ni kuwasogezea wananchi wake popote walipo wananufaika na matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Ninaliagiza Shirika la Umeme tawi la Pemba kuanzia tarehe ya leo hadi ifikapo mwishoni mwa mwezi wa tatu transfoma nyingine iwe imeshawekwa hapa Kojani," alisema Polepole.

Polepole aliwataka viongozi wa jimbo hilo kufuatilia kwa karibu agizo hilo na kuhakikisha transfoma hiyo inafungwa kwa wakati.

"Dhamira ya chama chetu ni kuwasogezea huduma muhimu wananchi wetu, hivyo ole wao watumishi ambao wamepewa majukumu ya kuwahudumia wananchi, lakini wanafanya uzembe, nitakula nao sahani moja," alieleza katibu huyo.

Wakati huo huo, Polepole aliiagiza Mamlaka ya Maji (ZAWA) Kisiwani Pemba kuweka pampu nyingine katika kisima kilichopo Kwale ndani ya siku tatu ili kiweze kutoa huduma kwa wananchi kama kilivyokusudiwa.

Akizungumza na wananchi wa Shehia ya Taifu baada ya kukagua kisima hicho, Polepole aliwahakikishia wananchi hao kuwa tatizo la ukosefu wa maji katika kijiji chao litaisha muda wowote kuanzia sasa.

Alieleza kuwa Serikali ya CCM awamu ya tano imedhamiria kuwapelekea wananchi wake maendeleo, hivyo ni wajibu wa watumishi wa umma waliokabidhiwa dhamana kufanya kazi kwa umakini sana.

"Maendeleo hayana chama, dini na hata kabila bali kila mwananchi wa nchi hii ana haki ya huduma zote muhimu kama wanavyopata wananchi wengine wa maeneo tofauti," alisema.

Mapema akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Daya Mtambwe Wilaya ya Wete baada ya kukagua ujenzi wa Chuo cha Amali ambacho kinajengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, aliwataka wanafunzi hao kusoma kwa bidii ili kufanikisha malengo yao.

# THRDC yampongeza JPM uteuzi makamishna THBUB

**Na Mbaraka Kambona**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), umepongeza hatua ya Rais John Magufuli ya kuwateua Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB).

Pongezi hizo zimetolewa na Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao huo, Onesmo Olengurumwa, alipokutana na Mwenyekiti wa THBUB, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu jijini Dodoma juzi.

Alisema uteuzi huo umefurahiwa na wadau wengi wa haki za binadamu kwani utaiwezesha tume kufanya kazi zake kama inavyopaswa.

Alisema kuwa THBUB ni chombo cha kitaifa ambacho kimeundwa kikatiba na kupewa mamlaka ya kuhamasisha na kulinda haki za binadamu nchini na wananchi wengi wanakitegemea chombo hicho kwa ajili ya kuwasaidia kutetea haki zao.

Aliongeza kuwa THBUB kukaa muda mrefu bila makamishna kulikwamisha mambo mengi kwa kuwa wao ndio wenye kufanya maamuzi mbalimbali katika taasisi hiyo.

Olengurumwa alisema pia kukosekana kwa makamishna hao kulipelekea kudorora kwa ushirikiano baina ya wadau wa haki za binadamu na taasisi hiyo, lakini sasa anaamini kwa kuwapo wao katika uongozi huduma za tume kwa wananchi zitatolewa kama inavyotegemewa.

Aidha, Olengurumwa alimhakikishia Mwenyekiti wa THBUB ushirikiano wa karibu na kumweleza kuwa watakaa kuona maeneo gani wanaweza kushirikiana, lakini kwa kuanzia alimwahidi Jaji Mwaimu kuwa THRDC itatoa mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa wa tume kuhusu namna bora ya kufanya utetezi wa haki za binadamu kwa wananchi.

Akizungumza wakati akimkaribisha mratibu huyo, Jaji Mwaimu alimweleza kwa ufupi kuhusu majukumu ya THBUB na mipango ya taasisi hiyo kwa mwaka huu.

Aliahidi kuendelea kushirikiana na wadau wote wakiwamo THRDC akisema kuwa tume peke yake bila kushirikiana na wadau wengine haitaweza kutimiza majukumu yake ipasavyo.

Rais alifanya uteuzi wa makamishna hao mwishoni mwa mwaka jana baada ya THBUB kukaa bila makamishna kwa takriban miaka mitatu.



Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa (kulia), akizungumza na Mwenyekiti wa THBUB, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu (kushoto), alipomtembelea ofisini kwake jijini Dodoma juzi. **PICHA: THBUB**

# Tanzania, Finland zajadili usawa kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo na Biashara ya Kimataifa wa Finland, Ville Skinnari, amefanya mazungumzo na Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Mendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu kuhusu maendeleo na usawa wa jinsia nchini.

Akizungumzia masuala ya jinsia, Jingu amesema serikali imechukua hatua madhubuti kuboresha usawa wa kijinsia na haki ya mtoto wa kike.

Amesema serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imewekeza katika kuwawezesha wanawake kiuchumi na masuala ya uongozi.

Ameongeza kuwa serikali imeweka mkakati kukabiliana na mimba katika umri mdogo na kupinga mila zilizopitwa na wakati ikiwamo ukeketaji.

Aidha, ameongeza kuwa sera ya Taifa ni kushirikisha wananchi katika jitihada za kukabiliana na vikwazo vilivyopo.

Dk. Jingu alisema serikali katika ngazi mbalimbali za uongozi imeunda kamati maalum za kulinda na kuhakikisha haki za mtoto zinalindwa.

Kwa upande wake, Waziri Skinnari alisema nchi yake inaunga mkono juhudi za Tanzania kupambana na changamoto zilizopo.

## Vyuo vyatakiwa kuboresha ujuzi

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

SERIKALI imevitaka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Ufundi nchini kuandaa programu za kuboresha ujuzi kwa wanafunzi ili kuwawezesha wahitimu kukidhi mahitaji ya soko la ajira ikiwamo kujiajiri wenyewe.

Hayo yalisemwa jijini Mwanza jana na Mkurugenzi na Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali, Vickness Mayao, aliyemwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika kongamano la wadau la namna ya kujadili utekelezaji wa dhana ya uanagenzi Kanda ya Ziwa ili kuimarisha ujuzi katika vyuo.

Mayao alisema kutokana na wahitimu wa vyuo hivyo kutokuwa na stadi za kutosha kukidhi mahitaji ya soko la ajira ikiwamo kujiajiri wenyewe, hali hiyo imesababisha ukosefu wa stadi hizo zinazohitajika kwenye soko la ajira, hivyo wataalamu wengi nchini kushindwa kuajiriwa na kujiajiri wenyewe.

Alisema, ili kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025, serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuwawezesha wahitimu wa vyuo vya maendeleo ya jamii nchini waweze kujiajiri na kuendana na ushindani wa soko la ajira kwa kuwa wakati umefika wa mitaala ya vyuo nchini kuboreshwa ili kukidhi mahitaji ya soko hilo.

"Tukaona tupate fursa ya kukaa na waajiri kwa sababu wanafunzi hawa tunatarajia waende kuajiriwa na kujiajiri ili kutekeleza adhima ya serikali ya kufikia uchumi wa kati wa viwanda ifikapo 2025," alisema Mayao.

Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Neema Ndoboka, alisema katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto idara hiyo imeandaa kongamano la namna ya kutekeleza dhana ya kuboresha ujuzi wa wahitimu wa vyuo vya maendeleo ya jamii na maendeleo ya ufundi, hivyo wameamua kujadili pamoja na waajiri namna ya kuboresha dhana ya wanagenzi ili kuboresha ujuzi wa wahitimu ambao watakidhi matakwa ya ajira.

Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare Musoma, Paschal Mahinyika na Mkurugenzi wa Shirika la Kivulini, Yassin Ally ni baadhi ya wadau waliozungumza kwenye kongamano hilo, kwa kuiomba serikali kuweka mifumo ya kielektroniki itakayosaidia kuendana na kasi ya ushindani ili waweze kupata uwezo wa kujiajiri kwa sababu wahitimu wengi wa vyuo wakienda mitaani hawana uwezo wa kujiajiri kutokana na kutopatiwa elimu hiyo.

"Mahitaji sasa hivi miradi yote ya maendeleo ya jamii yanatakiwa kuwa na mifumo ya kielektroniki inayoweza kupima na kuonyesha matokeo, utakuta wahitimu wengi wanafundishwa kwa nadharia kwa sababu wafundishaji hawana hizo nyenzo," alisema Ally na kuendelea:

"Hivi sasa tunatumia mifumo ya kisasa mfano, sisi tumepata shida kuwapata maofisa ufuatiliaji na tathmini mpaka tumewatafuta nje."

# Kairuki apigia debe uwekezaji Mara

**Na Mwandishi Wetu, MUSOMA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amesema kukamilika kwa mwongozo wa uwekezaji wa Mkoa wa Mara utasaidia kuibua na kuzitangaza fursa mbalimbali za biashara na uwekezaji zilizopo mkoani humo na hatimaye kuvutia wawekezaji wengi.

Akizungumza katika mkutano wa majadiliano kati ya sekta ya umma, wawekezaji na wafanyabiashara wa Mkoa wa Mara wenye lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kukuza uwekezaji katika mkoa huo, Waziri Kairuki alipongeza mkakati wa mkoa kuandaa mwongozo kwani utakuwa dira kwa sekta za uwekezaji na biashara.

"Nimefurahishwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Mkoa wa Mara kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kufanikisha azma ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025," alisema Waziri Kairuki ambaye aliambatana na Manaibu Waziri, Dk. Ashatu Kijaji (Fedha na Mipango) na Stella Manyanya (Viwanda na Biashara).

Aidha, Waziri Kairuki alikiagiza Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) chenye dhamana ya kutangaza vivutio uwekezaji kutumia tovuti ya mkoa wa Mara kuzitangaza fursa zote zilizopo mkoani humo ili kuchochea uwekezaji zaidi.

"Mwongozo wa uwekezaji wa mkoa utakapokamilika utakuwa ndiyo dira yenu katika kuzitangaza fursa za biashara na uwekezaji zilizopo hapa. Hii itachochea na kuvutia mitaji mingi ya uwekezaji katika mkoa wa Mara," alisisitiza.

"Naipongeza serikali ya mkoa kwa kuanzisha tovuti yake ambayo itakuwa sehemu ya kuzitangaza fursa zilizopo ili kuchochea na kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza katika mkoa wa Mara," alisema Kairuki.

Alisema Mkoa wa Mara una fursa nyingi katika sekta za uvuvi, kilimo cha pamba, miwa, kahawa, uzalishaji wa vifaranga, viwanda vya kuchakata samaki na nyinginezo nyingi ambazo zitahitaji kubadilisha maisha ya watu.

Manyanya amesema mkoa wa Mara una nafasi kubwa ya kuanzisha viwanda vikiwamo vya mifuko ya ngozi kwani soko lake ni kubwa ndani na nje ya nchi.

"Tumieni fursa hiyo kuwekezeka katika kiwanda cha kutengeneza mifuko ya ngozi ambayo inatumika migodini kubebea malighafi kutokana na uimara wake," alisema Manyanya.

Nayei Kijaji alisema serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini ikiwa ni pamoja na kupunguza utitiri wa kodi, tozo na ada mbalimbali ili kumrahisishia mfanyabiashara kufanya shughuli zake.

"Kwa mwaka mmoja uliopita kodi na tozo 54 zimefutwa ili kumwondolea adha mfanyabiashara na mwekezaji katika kufanya shughuli zake lengo likiwa ni kufikia azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025," alisema Kijaji.



Mwanasheria wa kituo cha taarifa kwa wananchi (TCIB), Neema Kimambo, akitoa somo la utekelezaji na ufanikishaji wa mikataba wazi kwenye manunuzi ya umma na mwongozo kwa wabunge wa Bunge la Tanzania, kwa washiriki wa mkutano kutoka asasi za kiraia (AZAKI), mkoa wa Mwanza juzi. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Kampeni kuudhibiti ukatili kijinsia Kisarawe

**Na Julieth Mkireri, KISARAWE**

DAWATI la Jinsia Polisi Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, limeratibu kampeni ya 'Ukatili wa Kijinsia Kisarawe Sasa Basi'.

Lengo la kampeni hiyo ni kukomesha vitendo hivyo ambavyo vinaelezwa kuwa kikwazo kwa watoto wa kike kufikia malengo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo iliyozinduliwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya hiyo, Jokate Mwegelo, Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kisarawe, Eva Stesheni, alisema kampeni hiyo imeratibiwa na dawati hilo kwa kushirikiana na watoto.

Eva alisema matukio ya ubakaji katika wilaya hiyo yanaendelea kuripotiwa mara kwa mara, ambapo kwa mujibu wa takwimu, kesi 55 za vitendo vya ubakaji viliripotiwa katika wilaya hiyo mwaka 2019.

Aidha, alisema kwa kipindi cha Januari 10 hadi Februari 22, kesi za ubakaji 20 zimeripotiwa, hali iliyosababisha jeshi hilo kuanza kutoa elimu ili kukomesha hali hiyo.

"Lengo la kampeni ni kupaza sauti, kuhamasisha utoaji wa taarifa za ukatili wa kijinsia hasa ubakaji kwenye vituo vya Polisi ili wahalifu wakamatwe na kutoa huduma stahiki kwa waathirika wa ukatili," alisema.

Alisema elimu ya ukatili wa kijinsia itaendelea kutolewa katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo, ili kusaidia wananchi kushiriki kikamilifu kupinga vitendo vya ukatili.

Kadhalika, katika kampeni hiyo wananchi na wanafunzi watapata fursa ya kupata elimu ya namna ya kuripoti matukio hayo, na mambo ya kufanya baada ya kufanyiwa vitendo vya ubakaji ili wasipoteze ushahidi wa tukio.

Eva aliwaomba wananchi kushirikiana kikamilifu na Jeshi la Polisi ili kumpa nafasi mtoto wa kike kutimiza malengo yake katika nyanja ya elimu.

Alibainisha kuwa kutokana na vitendo vya ubakaji, watu wawili waliokuwa wakikabiliwa na tuhuma za ubakaji, kesi zao zilimalizika Januari mwaka huu katika Mahakama ya Wilaya ya Kisarawe, ambapo mtuhumiwa Abdul Mkude alihukumiwa kifungo cha maisha jela na mtuhumiwa Samwel Abraham alihukumiwa miaka 30 jela.

# Wajasiriamali mbegu sasa waanza mkakati

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAJASIRIAMALI wa mbegu nchini wameanza mkakati wa kuzalisha mbegu zinazokabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi na zinazohimili ukame na kuleta mazao mengi, ili kumsaidia mkulima kupata uhakika wa chakula na kipato.

Akizungumza jana katika maonyesho ya kilimo teknolojia yaliyofanyika katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tari Seliani, Meneja Mauzo wa Kampuni ya Seedco, Daniel Ulimboka, alisema, kuwa kwa sasa wamefanya utafiti na kuja na mbegu bora ambazo zinahimili hali ya ukame, licha ya uhaba wa mvua, bado zinaleta mavuno ya kutosha kwa mkulima.

"Tuna mbegu aina ya tumbili 419 ambayo inafanya vizuri sana hasa katika kipindi ambacho hakuna mvua za kutosha, wakulima bado wamekuwa wakipata mavuno na kufurahia kilimo licha ya kukosa mvua," alisema Daniel.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Melchiory Temu, aliwataka watafiti kubuni teknolojia zinazoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi, ili wakulima wapate mazao badala ya kupata hasara kutokana na mabadiliko hayo ambayo yamekuwa yakileta athari na kusababisha kushuka kwa uzalishaji.

Aidha, aliwataka wakulima kuondokana na kilimo cha mazoea na kufanya kilimo chenye tija na kuwaletea manufaa wakulima na taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi wa Baraza la Nafaka Afrika Mashariki, Gerald Masila, alisema wanafanya juhudi za kuwaunganisha wakulima na masoko, ili wapate faida ya kilimo chao na kujikwamua kiuchumi.

"Tunafahamu juhudi zetu zitazaa matunda, kwani wakulima wamepata masoko, hivyo watakuwa na uhakika wa kujivunia kiuchumi," alisema.

> **"Tuna mbegu aina ya tumbili 419 ambayo inafanya vizuri sana hasa katika kipindi ambacho hakuna mvua za kutosha, wakulima bado wamekuwa wakipata mavuno na kufurahia kilimo licha ya kukosa mvua," alisema Daniel.**

# Wabunge wa EALA wataka naibu spika

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WABUNGE wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) juzi wamesema ipo haja ya kupelekea mapendekezo kwenye kikao cha Marais wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya kuongeza kipengele cha kuruhusu nafasi ya Naibu Spika, ili kuondoa mkanganyiko unaojitokeza pale spika anapopata udhuru.

Akizungumza jana kwenye kikao cha nne cha Bunge hilo, Mbunge kutoka Kenya, Abdulkadir Aden, alisema kikao cha juzi kilipoteza muda wa saa zaidi ya mbili kwa sababu ya kupitia sheria na kanuni ili kuona zinasemaje juu ya kumpata naibu spika wa muda, jambo ambalo ni upotevu wa muda.

"Sisi tumeona bora kupeleka mapendekezo yetu kwenye kikao cha marais wetu, ili kuomba waangalie mkataba wa uanzishaji wa EAC upoje na waingize kipengele cha kuruhusu nafasi ya naibu spika," alisema.

Alisema katika vikao vinne walivyokaa, vikao vitatu imejitokeza shida ya kumpata Naibu Spika, jambo ambalo linaleta shida katika vikao vyao pale spika anapopata udhuru.

"Kama jana saa mbili zimepotea tukibishana kumpata naibu spika wa kutuendeshea kikao chetu kwa siku mbili ambazo Spika wetu, Martin Ngoga hayupo, maana ana udhuru," alisema.

Naye Mbunge kutoka Tanzania, Habib Mnyaa, alisema mapendekezo watapendekeza na kupeleka kwa marais wa nchi wanachama, ili waone haja ya kubadilisha mkataba wa uanzishaji wa EAC.

"Lakini mimi kwa maoni yangu sioni haja ya kuwapo nafasi hiyo ya Naibu Spika, sababu ni upotevu wa gharama wakati bunge lenyewe dogo la watu 54 tu, maana anapokuwapo naibu spika atatakiwa kupata stahiki zake zote mi sioni haja bora kuendelea na utaratibu huu, anapokosekana spika tunachagua wa muda," alisema.

Mbunge mwingine kutoka Tanzania, Dk. Abdallah Makame, alisema kuna haja kubwa ya kuwapo Naibu Spika katika bunge hilo, ili kuepuka upotevu muda wanaopoteza pale spika wao anapopata udhuru.

"Pia sioni kama itashindikana kuingiza nafasi hii sababu Jumuiya ilipoanza ilikuwa na nchi tatu na itifaki ilikuwa moja, lakini sasa itifaki zimeongezeka sababu nchi wanachama zimeongezeka na hivyo hata kazi za bunge zimeongezeka na halikuwa na naibu katibu, lakini walipoona ipo haja walipeleka mapendekezo kwa marais wao ikawekwa nafasi hii," alisema.

Kabla ya hoja hizo kutolewa na wabunge hao, Katibu wa Bunge hilo, Charles Kadonya, alimtangaza Naibu Spika aliyepigiwa kura za siri, atakayeongoza kikao chao kwa siku mbili au tatu ambazo spika hatakuwapo.

"Katika nafasi hii ilikuwa na washindani wawili ambao ni Fatuma Ndagiza (Rwanda) ambaye amepata kura 18 na Leontine Nzeyimana kutoka Burundi amepata kura 27 kati ya wapiga kura 45 walioshiriki kikao hiki kati ya 54 waliotakiwa kuwapo, hivyo huyu Leontine ndiye atakayeongoza



Wakufunzi wa wenye ulemavu wa uziwi na wasioona kutoka Chuo cha Ualimu cha Patandi, wakimsikiliza Mkurugenzi Msaidizi Elimu Maalumu na Elimu ya Watu Wazima katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (hayupo pichani), wakati akifungua warsha ya kujengewa uwezo ili kuboresha upatikanaji elimu bora kwa viziwi na wenye ulemavu mwingine, iliyoratibiwa na Shirika la Kimataifa la Sense International, Tengeru, mkoani Arusha juzi. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Serikali yaeleza jitihada zake za kusaidia wenye ulemavu

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

SERIKALI imesema imekua mstari wa mbele kusaidia na kuboresha huduma kwa watu wenye ulemavu.

Baadhi ya jitihada hizo ni kutunga sera, sheria na miongozo ili kuhakikisha kundi hilo linapata huduma stahiki.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, David Lyamongi, alisema hayo jana jijini hapa, wakati wa maonyesho ya picha za wenye ulemavu wa uti wa mgongo, waliowezeshwa kufanya shughuli za kiuchumi katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.

Alisema miongoni mwa juhudi za serikali ni kufanya utambuzi wa watu wenye ulemavu kupitia Idara ya Ustawi ya Jamii, mwongozo wa kuboresha miundombinu kwa watu wenye ulemavu, utoaji wa mikopo ya asilimia mbili kila halmashauri, kwa ajili ya vikundi vya wenye ulemavu.

"Nafahamu bado zipo changamoto nyingi wanazokutana nazo watu wenye ulemavu hasa ulemavu wa uti wa mgongo, niwatoe hofu kuwa serikali yenu inaendelea na michakato mbalimbali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), kuhakikisha mikopo mnayopata inakua na tija," alisema Lyamongi.

Mratibu wa mradi wa Jenga Maisha Kua Kiuchumi, unaowawezesha wenye ulemavu wa uti wa mgongo kiuchumi, kutoka asasi isiyo ya kiserikali ya Motivation Tanzania, Goodluck Chanika, alisema lengo la maonyesho hayo ni kuonyesha faida walizopata za kujipatia kipato, ikiwa ni pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo.

"Tumefanikia kuwafikia watu wenye ulemavu 96, ambao tumewapa elimu ya ujasiriamali na kuwawezesha mitaji ya aina ya shughuli wanazoweza kuzifanya katika hali zao, pia tumewapa baiskeli zinazowapa mwendo wa kutoka sehemu moja hadi nyingine na tumefanikiwa kutokana na ushirikiano mzuri wa serikali," alisema Chanika.

Mwenyekiti wa Asasi ya Kilimanjaro Association of Spinal Cord Injuries (KASI), Goodwill Linus, alisema kwa kushirikiana na Motivation Tanzania, wamewasaidia watu wenye ulemavu, katika nyanja mbalimbali zikiwamo za kiuchumi.

Aliongeza kuwa wanakabiliwa na changamoto ya usafiri kwa sababu vyombo vingi vya usafiri wa pamoja vimekuwa haviwapokei wenye ulemavu, huku miundombinu ya majengo mengi yakiwamo ya serikali kutokuwa rafiki kwao kuingia kupata huduma kama wananchi wengine.





# Eneo utalii wa faru wagharimu bil. 2/-

Na Godfrey Mushi, SAME

KAZI ya kujenga eneo maalumu la utalii wa faru katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi iliyopo kati ya mikoa ya Kilimanjaro na Tanga, umeigharimu Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) zaidi ya Sh. bilioni mbili.

Kamishna Msaidizi wa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, Abel Mtui, alisema mradi huo wa kukuza utalii wa faru utaisaidia kuitangaza zaidi na kuongeza mapato yake.

Jana, kamishna huyo alisema Tanapa imewekeza fedha nyingi katika mradi huo ili kuifanya Mkomazi kuwa sehemu ya vivutio vikubwa vinavyopatikana Kaskazini mwa Tanzania.

"Huu mradi wa ujenzi wa uzio wa faru na eneo maalumu la utalii wa faru, unalenga zaidi kurahisisha wageni kumuona mnyama faru kwa urahisi na karibu zaidi," alisema.

Kwa mujibu wa Mtui, Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ilianzishwa kama pori la akiba lililomegwa kutoka Pori la Akiba la Ruvu mwaka 1951. Hifadhi hiyo yenye ukubwa wa kilomita za mraba 3,234 ni miongoni mwa hifadhi za Taifa 22 zilizopo nchini kwa sasa ikiwa chini ya miteremko ya safu ya Milima ya Tao la Mashariki.

Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule, akizungumzia mradi huo alisema utalii huo wa faru utaitambulisha wilaya hiyo kimataifa hasa kutokana na aina ya faru waliopo katika nchi za Afrika ya Mashariki.

Alisema Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ni miongoni mwa chache zenye wanyama aina ya faru ikiwa ndio inayotumika kuzalisha idadi ya wanyama hao kwa ajili ya kuimarisha utalii katika hifadhi za Tanzania.



Baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, wakisubiri kufanyiwa uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ikiwamo homa ya ini na madaktari bingwa wa Hospitali ya Rufani ya KCMC na Hospitali ya Mawenzi, jana. **PICHA: GOFREY MUSHI**

# KCMC yatengeneza mafuta ya wenye ualbino

Na Godfrey Mushi, MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya KCMC imeanzisha kiwanda maalumu cha utengenezaji wa mafuta maalumu yanayowasaidia jamii ya watu wenye ualbino na matatizo ya ngozi kukabiliana na magonjwa ya ngozi na bakteria wanaoharibu rangi ya ngozi yao.

Mafuta hayo pia yana kazi kubwa ya kupunguza mionzi ya jua ambayo imekuwa ikiathiri afya ya ngozi kwa watu hao.

Akizungumzia maendeleo ya kiwanda hicho jana, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya KCMC, Dk. Sara Mazinaa, alisema kuanzishwa kwa kiwanda hicho ni sehemu ya mafanikio ya hospitali hiyo kubadili utendaji kazi wake katika utoaji huduma za afya, uchunguzi na tiba.

Ujio wa kiwanda hicho hivi sasa unaifanya KCMC kuwa hospitali yenye kiwanda kinacholenga kupunguza baadhi upatikanaji wa vifaa tiba.

"Kundi la watu wenye matatizo ya ngozi ni miongoni mwa makundi ambayo yamekuwa yakiathirika zaidi na magonjwa ya ngozi, magonjwa ambayo wakati mwingine hugeuka na kuwa sugu na kusababisha saratani ya ngozi," alisema Dk. Sara.

Mkurugenzi huyo alisema KCMC imeanza kuzalisha mafuta maalumu kwa watu wenye ulemavu wa ngozi, na tayari watu 6,500 katika mikoa 23 wameanza kunufaika na mafuta hayo ambayo yanatolewa bila malipo.

Kwa upande wake, Dk. Lulyritha Kini, ambaye ni mkuu wa idara ya magonjwa ya ngozi na zinaa wa hospitali hiyo, alisema kwa sasa Tanzania inakadiriwa na watu wenye ualbino zaidi ya 25,000.

Alisema licha ya kuwapo kwa idadi hiyo, tatizo lililopo hivi sasa ni upatikanaji wa mafuta hayo kwa kundi hilo.

Licha ya uwezo wa kiwanda hicho cha kuzalisha mafuta maalumu kwa watu wenye ualbino, bado kuna uhitaji wa serikali kuingilia kati suala la malipo ya kodi kwa malighafi zinazoagizwa toka nje kwa ajili ya kutengenezea mafuta hayo.

Meneja mradi wa uzalishaji wa mafuta hayo, Ebenezer Fabian, alisema hospitali hiyo hununua malighafi za uzalishaji wa mafuta hayo nje ya nchi kwa gharama kubwa.

# SBL yafadhili wanafunzi 10 Chuo cha Kilimo

Na Godfrey Mushi, MOSHI

WANAFUNZI 10 wanaosoma kozi ya ughani katika Chuo cha Kilimo na Ufugaji cha Kilacha, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wamepatiwa ufadhili na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL).

Wataalamu hao wapya wa kilimo watakuwa wanufaika wa pili wa ufadhili huo kupitia Programu ya Kilimo-Viwanda.

Mkurugenzi Mkuu wa SBL, Mark Ocitti, akizungumza na Nipashe jana, alisema mpango huo wa ufadhili wa masomo unalenga kuwaanda wataalamu wa kilimo ikiwa ni jitihada za kuunga mkono sera ya Rais John Magufuli ya kuandaa wataalamu kuelekea uchumi wa kati wa viwanda.

"Tumeamua safari hii kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo ya Kilimo na Ufugaji cha Kilacha, kuwaandaa vijana wa Kitanzania kuwa wataalamu katika masuala ya kilimo na ufugaji ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali za kuinua sekta ya kilimo hapa nchini," alisema Ocitti.

Chuo hicho kilianzishwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Moshi miaka 40 iliyopita.

Kwa sasa, kina wanafunzi 406 wanawake wakiwa 241.

Mkuu wa chuo hicho alisema idadi ya wanaodahiliwa kusomea kilimo na masuala ya ufugaji inaongezeka siku hadi siku, lakini tatizo kubwa linalowatesa wanachuo hao ni gharama za ada ya masomo.

Awali, Meneja Uhusiano wa SBL, Neema Temba, alisema Kilacha kwa sasa ni miongoni mwa vyuo binafsi vilivyoteuliwa na Serengeti Breweries kwa wanafunzi wake kuanza kunufaika na ufadhili wa masomo kupitia programu ya kilimo viwanda baada ya kukidhi vigezo vilivyohitajika.

Padri Jorome Silayo, ambaye ni Makamu Mkuu wa chuo hicho aliiomba serikali kufadhili wanafunzi wengine ili waweze kuongeza idadi ya wataalamu katika sekta ya kilimo.

Kampuni ya Bia ya Serengeti Breweries inatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 50 kila mwaka kutoka kwa jamii za wakulima ambazo hazina uwezo.

**"Tumeamua safari hii kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo ya Kilimo na Ufugaji cha Kilacha, kuwaandaa vijana wa Kitanzania kuwa wataalamu katika masuala ya kilimo na ufugaji ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali za kuinua sekta ya kilimo hapa nchini," alisema Ocitti.**



Ukurasa 14

**Takukuru inavyopambana na rushwa makao makuu**

Uchaguzi serikali za mitaa DRC wapigwa tena kalenda




Ukurasa 17

siasa

JUMATANO FEBRUARI 26, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 19

**Ni Agathon Rwasa dhidi ya kipenzi cha Nkurunziza**



Ukurasa 20

**Baada ya miongo kadhaa, al Bashir sasa kutinga ICC**

# Huyu ndiye Mashinji aliyeondoka

- Ameitumikia Chadema miezi 46
- Kaacha msururu wa ahadi zake

**Na Mwandishi Wetu**

ILIKUWA Machi 13 mwaka 2016 siku ya kumbukumbu isiyosahaulika kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji, baada ya kutangazwa kushika nafasi hiyo baada ya kupata baraka za Baraza Kuu la chama hicho kwa asilimia 100.

Wajumbe wa Baraza Kuu walikutana jijini Mwanza ikiwa ni miezi kadhaa tangu aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa, kujiunga na chama hicho na kubeba jukumu la kupeperusha bendera ya uliokuwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) kupitia Chadema katika nafasi ya urais , kwenye uchaguzi mkuu wa 2015.

Hata hivyo, Lowassa hakushinda nafasi hiyo kwa kuwa alipata kura milioni 6.07 sawa na asilimia 39.97 na mshindi akawa Rais John Magufuli, aliyeshinda kwa kura milioni 8.88 akijikusanyia asilimia 58.46.

Katika kikao cha Mwanza jina la Mashinji lililetwa mbele ya Baraza na Mwenyekiti wa Chadema Taifa,

**INAENDELEA UK.16**



Dk. Vincent Mashinji. **PICHA: MTANDAO**

**Mapito ya Katibu Mkuu Dk. Vincent Mashinji na nyayo zake** Ukurasa 18

# Takukuru inavyopambana na rushwa makao makuu



Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali Julius Mbung'o, akiongea na waandishi wa habari. **PICHA: MTANDAO**

**Na Renata Msungu,** DODOMA

KUONGEZEKA kwa watu jijini Dodoma kunawezaje kuhusishwa na rushwa? Je, imepungua au imeongezeka?

Ni swali ambalo linahitaj majibu hasa kwa wale wanaofuatilia na kuhoji mienendo ya suala la rushwa kwenye huduma za jamii, miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa miundombinu na hata kupata ajira kwenye sekta mbalimbali za mji unaoibua kama Dodoma.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na taasisi za kuzuia na kupamba inaonyesha rushwa imepungua kwa asilimia kubwa na Dodoma ni sehemu ya Tanzania hivyo ni dhahiri kama ilivyo mikoa mingine tatizo hilo limepungua.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Dodoma, inasema kila mara imekuwa ikiwabaini wanaokutwa na viashiria vya rushwa na kuwashughulikia.

Takukuru inasema ukiacha hilo idadi ya taarifa zinazowasilishwa na wananchi ofisi kwake ni kipimo tosha cha kuonyesha jinsi gani watu wana uelewa kuhusu ya madhara ya kuomba na kupokea rushwa .

"Kesi zimeongezeka kuripotiwa na hiki ni kiashiria kuwa watu wanapata elimu ya jinsi ya kupambana na rushwa, "anasema Mkuu wa Takukuru Dodoma, Sosthenes Kibwengo .

Anaongeza kuwa juhudi kubwa za uelimishaji wananchi zinazofanywa na Takukuru zimeleta manufaa ndiyo maana hata katika takwimu ambazo wanazitoa mara kwa mara kuna baadhi ya taasisi zimeonya kupungua kwa kiwango cha rushwa kadri siku zinavyoongezeka.

> Rushwa ya ngono watu hawaleti taarifa za kutosha kwa sababu wanaogopa, lakini sasa tumeanzisha kampeni ya vunja ukimya kataa rushwa ya ngono.

### VYOMBO VYA HABARI

"Niseme ukweli vyombo vya habari vimekuwa msaada mkubwa sana kwa Takukuru kutokana na ushirikiano na utoaji taarifa za taasisi zinazolenga kuwafahamisha wananchi ubaya wa rushwa," anasema Kibwengo.

Anataja magazeti na vipindi vya redio kuwa vimekuwa msaada mkubwa kutokana na kuchangia kufikisha elimu inayotolewa na Takukuru ya kujiepusha na vitendo vya rushwa lakini pia namna ya utoaji wa taarifa katika taasisi hiyo hasa pale kunapoonekana kuna baadhi ya watuhumiwa wana viashiria vya rushwa."

Mkuu wa Takukuru Dodoma anasema taarifa za uchunguzi zinaonyesha kuwa hivi sasa katika maeneo mbalimbali ambayo wamepita watu wana uelewa mkubwa juu ya kupambana na rushwa.

### RUSHWA INAYOSUMBUA

Kibwengo anaitaja rushwa inayosumbua kuwa ni ile ambayo mtu anatumia madaraka kinyume na sheria na hii hutendwa na wenye mamlaka wanapojaribu kushawishi mtu ampatie rushwa ili aweze kumtimizia haki yake ya msingi.

"Aina hii ya rushwa inasumbua sana kwa sababu wengi hutaka kufanyiwa kazi zao haraka hivyo hushawishika kutoa hongo na wahusika watendaji hupata fursa ya kuomba hongo ili watekeleze majukumu yao.

Kamanda Kibwengo anasema wanaipiga vita na ni aina moja ya rushwa ambayo inasumbua katika maeneo mbalimbali na ni kwa sababu watu hutaka kupita njia ya mkato ili kufanikisha mambo yao.

"Na hii aina ya rushwa inahusisha watu au kada za aina zote. Ni wa chini, juu na kati na wote wanahusika kutenda aina hii ya hongo kwa sababu ni rahisi watu kuifanya kutokana na kila mmoja kupenda kupenya kirahisi wakati wa kutafuta haki zake au zao za msingi."anasema kiongozi huyo.

Anaeleza kuwa wanajitahidi kupambana na kosa hilo na kadri siku zinavyokwenda linapungua kwa sababu Takukuru ina mamlaka ya kulisimamia na kumpeleka mtuhumiwa moja kwa moja mahakamani bila ya kupitia kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kutokana na hilo Takukuru inapambana na watu wanaohusika na aina hii ya rushwa ili kuitokomeza na kila mara wanaipigia kelele ili watu waweze kuifahamu , kuikemea na kuikabili.

"Aina hii ya rushwa haiko kwa watumishi wa umma pekee bali hata katika sekta zote za binafsi kwa sababu kila mahali huduma hizo zinahitajika kwa jamii." anasema

### MATUMIZI YA MAMLAKA

Rushwa nyingine inayosumbua ni kosa la matumizi mabaya ya mamlaka ambayo hupelekea kumtendea mtu ndivyo sivyo, anasema Kibwengo.

Kosa hili ni kinyume na kifungu cha sheria namba 31 ya kuzuia na kupambana na rushwa ambayo inakataza mtu kutumia mamlaka ya umma vibaya aliyonayo na kupelekea kukiuka kufanya haki za msingi kwa anayestahili.

Kibwengo anasema hilo nalo ni kosa korofi na hufanyika kila mahali kwa sababu watu wanapenda kutumia mamlaka vibaya ili kuwakandamiza wengine jambo ambalo halikubaliki kisheria ndio maana unaona kila mara kumekuwa na juhudi za kulipigia kelele ili watu watendewe haki hususani pale wanapohitaji huduma ambazo ni haki zao za msingi.

"Hivyo basi ni vema jamii ikaelewa zaidi juu ya upatikanaji wa haki zao za msingi na si kutumia rushwa . Hakuna sababu ya kuhonga ili uhudumiwe."

### NYARAKA ZA SERIKALI

Kosa jingine analolizungumzia ambalo halipishani sana na hayo mawili ni matumizi mabaya ya nyaraka za serikali, kwa mfano kughushi nyaraka hizo ambazo wengi wamekuwa wakijaribu kufanya hivyo, anaeleza Kibwengo.

Hata hivyo, anasema wanaishia mikononi mwa sheria kutokana na kukamatwa na kuongeza: "Wengi wanaofanya kosa hilo hufikiwa na mkono wa sheria na kupelekwa mahakamani, "anasema Kibwengo.

"Hili kosa watu hugushi kwa namna tofauti kwa mfano mwingine anaweza kujaza mafuta ya Sh. 20,000 lakini akaandika 120,000 mwingine zaidi ya hapo na hii inafanywa kulingana na uwezo wa taasisi katika utoaji wa matumizi kulingana na bajeti zao, "anasema.

Anaeleza kuwa kosa hilo ni kinyume na kifungu cha sheria namba 22 ambacho kinakataza na rushwa hii hufanywa zaidi katika miradi mbalimbali ya maendeleo inayofanywa katika maeneo tofauti.

Kibwengo anasema rushwa hii mara nyingi inawahusisha wanunuzi wa vifaa vya mradi pamoja na wauza maduka au muda mwingine mnunuzi pekee akishanunua vitu anakwenda kughushi nyaraka na kuandika zenye kiasi kikubwa ili aibishe taasisi fedha au vifaa.

Anaeleza kuwa rushwa hiyo ni ubadhirifu wa mali ya umma au ufujaji wa fedha za wananchi na kwamba Takukuru imepambana na aina hii ya rushwa katika miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa katika maeneo mbalimbali.

### NGONO

Kibwengo anasema rushwa ya ngono inatajwa katika maeneo mengi na ni moja ya rushwa ambazo zinaongoza japo wananchi hawaleti mashtaka yao kwa wingi Takururu.

Anasema kuna kificho na anahisi ni kutokana na kuogopa kwamba watadhalilika au wengine wanahofia kuchekwa na jamii kitu ambacho si kweli.

"Rushwa ya ngono watu hawaleti taarifa za kutosha kwa sababu wanaogopa, lakini sasa tumeanzisha kampeni ya vunja ukimya kataa rushwa ya ngono, "Kibwengo anasema.

# Wanasiasa wajitosa elimu Mara

## • Wamo Stephen Wassira, Muhongo, Anney

Na Sabato Kasika

MKOA wa Mara ndiko nyumbani kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere. Ni kiongozi na mwanasiasa maarufu anayeheshimika duniani hata sasa.

Pamoja na Nyerere Mara ni chimbuko la viongozi waasisi akiwamo Timothy Apio Katibu Mkuu kiongozi wa kwanza, Waziri Mkuu mstaafu Joseph Warioba pia ni mzaliwa wa Mara.

Leo hii hali ya elimu mkoani humo, haiwafurahishi wadau licha ya kwamba ulikuwa mkoa chimbuko la wasomi na viongozi wa kitaifa, elimu inadaiwa kukwamishwa na masuala mengi kama mila za ukeketaji zinazowakwamisha mabinti kusoma.

Walimu kushambuliwa na kuuawa kama ilivyotokea Tarime mwaka jana na pia utoro shuleni na uhusiano mbaya baina ya wazazi na walimu.

Ili kupata ufumbuzi wa kudumaa elimu mkoani humo, wadau wa elimu wa mkoa wanakutana kwenye kongamano maalumu la kuboresha sekta hiyo ili kuongeza ufaulu katika shule za msingi na sekondari.

Kongamano linaibuka na maazimio saba kwa ajili ya kuinua kiwango cha elimu likidokeza kuwa sababu za kuwapo mkakati huo unaobuniwa na mkuu wa mkoa huo, Adam Malima, ni baada ya matokeo yasiyoridhishwa ya mitihani ya taifa ya darasa la saba na kidato cha nne mwaka jana.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wadau wa elimu walimuomba kuitisha kongamano hilo ambalo lilifanyika juzi Jumapili likishirikisha wadau wa elimu zaidi ya 400 kutoka ndani na nje ya mkoa huo.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mara, Ephraim Simbeye, anasema, katika kongamano hilo, wametoka na maazimio saba, ambayo yalitanguliwa na ushauri wa baadhi ya wadau akiwamo, Stepehen Wasira.

"Wasira, anapendekeza walimu wapewe motisha kama njia mojawapo ya kutambua kazi wanaoifanya, kusikilizwa na kusaidiwa hasa wale wenye matatizo na kwamba suala la usimamizi wa elimu linahitaji mipango wa muda mrefu na mfupi," anasema Simbeye.

Anasema, Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk, Vincent Anney naye aliwasilisha ripoti ya utafiti alioufanya juu ya ufaulu duni katika mitihani mkoani Mara na kupendekeza kuimarishwa kwa ufundishaji na ujifunzaji.

"Dk. Anney ni mwalimu na ana shahada ya uzamivu (PhD) na anapendekeza ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo ya shule, kutolewa kwa elimu ya makuzi kwa wanafunzi shuleni na kuzingatia maadili, nidhamu kwa walimu na wanafunzi," anasema.

Simbeye anasema, mkuu wa mkoa alikuwa na msimamizi wa kongamano hilo huku Profesa Sospeter Muhongo mbunge wa Musoma Vijijini akiwa ni mchokoza mada za kufanikisha uboresheji wa elimu mkoani humo.

### YALIYOAZIMIWA

Ofisa elimu huyo anayataja maazimio ya kongamano hilo kuwa la kwanza ni uboreshaji wa miundombinu ya elimu ya aina zote katika shule za msingi na sekondari kuanzia ujenzi wa madarasa, uongezaji wa madawati na vifaa vingine vya shule.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima (mbele kushoto) na mwanasiasa Stephen Wasira pamoja na wadau wengine wa elimu wakifuatilia kongamano hilo. **PICHA ZOTE: MPIGA PICHA WETU**

> Wasira, anapendekeza walimu wapewe motisha kama njia mojawapo ya kutambua kazi wanaoifanya, kusikilizwa na kusaidiwa hasa wale wenye matatizo na kwamba suala la usimamizi wa elimu linahitaji mipango wa muda mrefu na mfupi.

"Azimio la pili ni kudhibiti utoro wa wanafunzi, ambao nao unachangia kushuka kwa elimu, na azimio la tatu ni kuanzisha utaratibu wa kutoa chakula shuleni na kuhakikisha shule zenye mashamba zinazalisha chakula ambacho kitatumiwa na wanafunzi," alisema Simbeye.

Anataja azimio la nne kuwa ni kuwapo kwa mahusiano mazuri ya shule na jamii na pia kudhibiti nidhamu ya wanafunzi, na kwamba azimio la tano ni kupambana na ukatili na mimba za wanafunzi.

Simbeye anaelezea azimio la sita walilokubaliana wadau hao kuwa ni ni ushirikishwaji wa jamii katika masuala ya elimu wakati azimio la saba ni usalama wa walimu na wanafunzi ili kuhakikisha kila upande unatimiza wajibu bila kukwazwa.

"Kongamano pia limeunda kamati ya kufuatilia maazimio hayo ambayo itaongozwa na mkuu wa mkoa huku wajumbe wake wakiwa ni wakuu wote wa wilaya za mkoa wetu," anasema.

### TATHMINI

Simbeye anasema, kamati hiyo itashirikiana na wataalamu wa elimu kufuatilia kile walichokiamua na kisha Agosti mwaka huu wadau wa elimu watakutana tena kufanya tathamini ya utekelezaji wa maazimio hayo.

Anasema, hatua ya kuitisha kongamano hilo ni kutaka kutoka waliko sasa na kwenda mbele ili mkoa wao ung'are kielimu badala ya kuendelea kurudi nyuma wakati uwezekano wa kumaliza tatizo upo.

"Kimsingi ni kwamba kwa miaka mitatu mfululizo mkoa haujafanya vizuri, na wadau wa elimu wameliona hilo na kuamua kukutana na kuweka mikakati ya kuhakikisha mkoa unakuwa juu kielimu," anasema.

Anafafanua kuwa, katika mtihani wa taifa wa darasa la saba wa mwaka jana, Mkoa wa Mara ulikuwa wa 26 kitaifa, huku kidato cha nne ukiwa wa 25 kitaifa, hali ambayo alisema, ni muhimu ifanyiwe mabadiliko.



Prof. Sospeter Muhongo (wa tatu kushoto), akiendesha kongamano hilo.

Anasema, Mkoa wa Mara una zaidi ya shule za sekondari 204 wakati za msingi zikiwa ni 847, ambazo na zote zimewekewa maazimio, ambayo hatimaye yatakuwa na matokeo mazuri.

"Wadau wameazimia kumaliza changamoto zinazoikumba sekta ya elimu mkoani Mara, hivyo nina uhakika kwa mwanzo huu tutafanikiwa, kwani wana nia ya kweli kuunyanyua mkoa wao," anasema.

### ENZI HIZO

Mbunge wa jimbo la Musoma Vijijini na mwenyekiti wa kongamano, Prof. Muhongo anasema, enzi zao wakati wanasoma, mkoa huo ulikuwa ukiongoza katika ufaulu na kutoa wanafunzi bora tofauti na sasa.

Anasema, wenyeji wa mkoa huo ndiyo wenye dhamana ya kuinua kiwango cha elimu katika mkoa wao na hatimaye kupata ufaulu mzuri ambayo itaiepusha Mara kuwa ya mwisho.

"Tunataka mkoa wetu urejee kwenye nafasi ya kwanza kama zamani, hivyo kongamano limekuja wakati muafaka na ninaamini maazimio yatakuja na majibu mazuri," Prof. Muhongo anasema.

Prof. Muhongo anasema, ubora wa elimu ni mwanafunzi aelimike na kufaulu mitihani, hivyo ni muhimu kuboresha elimu mkoani mwao huku wakidadisi na kujifunza kutoka kwingineko kwa ajili ya kuwa na elimu bora.

Naye Stephen Wasira, anasema anaguswa sana na changamoto za elimu zinazoukumba mkoa wa Mara na ametoa ushauri wake ambao anaamini utakuwa na mchango mkubwa kubadili uelekeo.

"Ni vyema kutambua kuwa elimu ndiyo msingi wa maendeleo ya mtu na ndiyo kila kitu na kwa kutambua hilo, tumeamua kuungana na ndugu zetu katika kongamano na kutoka na maazimio saba," anasema Wasira.

Wasira anasema, wamebaini changamoto nyingi zinazokwamisha maendeleo ya elimu ya kuyawekea maazimio hayo yenye lengo la kuurudisha mkoa kwenye hadhi yake ya zamani.

# Huyu ndiye Mashinji aliyeondoka

INATOKA UK.13



Dk. Mashinji akiwa na Mwenyekiti Mbowe na viongozi wengine wa Chadema mahakamani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Freeman Mbowe, ikiwa ni saa chache tangu alipompigia simu na kumweleza nia ya kumteua kwenye nafasi hiyo.

Kijana na daktari wa binadamu, hakusita, aliitikia wito na kuujongea utumishi akianza kazi ya kukitumikia chama.

Akiwa ametimiza miezi 46 na siku saba au miaka 3.8 na wiki moja anaondolewa kwenye nafasi hiyo, na Mwenyekiti Mbowe kupeleka jina la Mbunge wa Ubungo na Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Bara, John Mnyika, kushika wadhifa huo, Mnyika naye jina lake linapitishwa na Baraza Kuu.

Jumanne iliyopita Februari 18, Mashinji anatangaza kukihama chama hicho na kujiunga na CCM, kabla hajatimiza ndoto zake za kuongeza wanachama na kuing'oa CCM madarakani.

Mwaka 2016 baada ya kutajwa kwenye nafasi hiyo anaeleza jinsi Mbowe alivyompigia simu akiwa hotelini na kumweleza kuwa analipeleka jina lake kwenye Baraza Kuu kwa ajili ya kupigiwa kura ili kushika nafasi ya Katibu Mkuu.

**USHUHUDA WAKE**

Mara baada ya kupitishwa na Kamati Kuu, anasema "Sikuwahi kufikiri naweza kuwa Katibu Mkuu wa chama kikubwa kama hiki... Mwenyekiti wa Taifa, Mbowe, aliniita wakati wa chakula na kunieleza amenichagua kuwa Katibu Mkuu, nilishtuka na kuogopa sana kwa kuwa nilijua viatu vya Dk. Wilbroad Slaa ni vikubwa na sikuamini naweza kwenda na kasi yake,"ndivyo anavyoeleza.

Wakati Dk. Mashinji anapewa jukumu hilo ndiyo wakati ambao chama hicho kilikuwa kinapita katika kipindi cha mpito cha kuondokewa na Dk. Slaa aliyeamua kubaki bila chama tangu mwaka 2015 wakati wa kuelekea Uchaguzi Mkuu na kukifanya chama hicho kwenda kwenye uchaguzi mkuu bila mtendaji mkuu. Dk. Slaa ni Balozi wa Tanzania nchini Sweden.

Wakati huo, Dk. Mashinji analieleza Baraza hilo kuwa anaona yeye ni mtu mdogo sana kuvaa viatu vya Dk. Slaa lakini kwa imani iliyoonyeshwa kwake angeshikilia nafasi hiyo na kukivusha chama na bila kusita akaainisha vipaumbele vyake.

**AHADI ANAZOWEKA**

Akizungumza jinsi alivyochangia kukiinua chama anasema ndiye mwasisi wa neno mabadiliko ndani ya chama hicho.

Anakumbusha jinsi alivyokuwa mwanachama akisema wakati akiwa Muhimbili alishirikiana na wenzake wengine kuandika machapisho mbalimbali ya afya na sera ambayo waliona yanafaa kuingia kwenye utekelezaji na kuyapeleka kwa Mwenyekiti Mbowe ambaye aliwaagiza kwenda kwa Katibu Mkuu wa wakati huo.

"Tulivyofika kabla ya kupokea machapisho yetu alituhoji kama tuna kadi ya chama na kututaka kuchukua kadi, lakini hakujua kuwa uanachama ulikiwa moyoni zaidi kuliko kushika kadi, nilichukua kadi za Chadema , Machi mosi, mwaka 2011 na kuwa mwanachama ambaye nilipenda kufanyakazi kwa kujitolea zaidi," anaeleza.

> Wao wana nguvu ya mabomu sisi tuna watu. Kwani watoto wao hawakai chini shuleni? tunawaonya wanaowapa amri polisi zisizo na tija na kuwafanya waishi kwa taabu uraiani...

Anasema anakumbuka kauli ya mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, kuwa woga ni dhambi na daima hupaswi kuwa mwoga na ndipo alipotulia na kuona kuwa anaweza nafasi hiyo na kumrudia Mwenyekiti kumweleza kuwa yupo tayari kushika wadhifa huo.

Anaahidi kufanyakazi kwa bidii na hatafanya biashara kwenye chama kwa kuwa anatambua ni cha wote na lengo kubwa ni kufikia ushindi wa mwaka 2020 na kwa ambaye anaona hawezi na hakuna ushindi anaruhusiwa kushuka kwenye jahazi.

**ILANI YA CHADEMA**

Katibu huyo wa zamani anasema ameshiriki uandishi wa Ilani ya Chadema ya mwaka 2015, aidha, ameandaa sera na machapisho mbalimbali na anajua jinsi inavyoweza kutekelezwa kuanzia ukurasa wa kwanza hadi wa mwisho, hivyo kazi kubwa ni kusimamia utekelezaji wake katika halmashauri zinazoongozwa na chama hicho.

Anaagiza kila halmashauri inayoongozwa na Chadema kutekeleza ilani ya chama hicho katika sekta mbalimbali na kwamba hawakupewa halmashauri hizo kwa ajili ya 'kuuza sura' na kwamba ubora wa chama pia utapimwa hapo.

Kadhalika anataka kila kata nchini kuwa na kamati za ufuatiliaji hata kama hakuna madiwani, ili kujua utekelezaji na kero za wananchi wa eneo husika kwa wananchi kuwakilishwa vyema kwenye hiyo kamati.

Pia, anaagiza kila kata iwe na kamati ya madiwani na wananchi kutembelea miradi ya maendeleo na shughuli za kijamii kama elimu, maji na vituo vya afya au zahanati na kwamba sheria inaruhusu kuhoji masuala mbalimbali kwa watendaji wa serikali katika maeneo yao.

Anaahidi kuendesha chama kimkakati zaidi kwa kuwa na mabadiliko ya kimfumo ndani na nje ya Chadema kwani hakuna sababu ya kupanga foleni kwa muda mrefu kupiga kura halafu matokeo yachakachuliwe na kubandikwa.

"Hiki chama siyo changu wala Mbowe, ni lazima tusimike kwa wananchi, turudishe msingi wa matawi ya chama kila eneo, kazi yangu kubwa ni kukifikisha chama chini ambako ndiko kuna wanachama na wanapaswa kuamua hatma ya chama chao,"anabainisha.

Anasema lengo kuu ni kushika dola mwaka 2020 kwa falsafa ya nguvu ya umma, na kwamba wanajengea ujasiri wanachama wasiogope polisi ambao wanatumiwa na viongozi na kusahau nao wanaishi na wana ndugu uraiani.

**KATIBA MPYA**

Dokta Mashinji anawaahidi wajumbe waliokuwa wakimsikiliza kuwa suala jingine ni kudai katiba mpya kistaarabu kwa kuwa nchi siyo ya wachache na kuwa na sauti ya pamoja kuanzia kwa wanachama hadi viongozi kwa kuwa katiba ya wananchi iliandaliwa lakini ilivurugwa na bunge maalum la katiba ambalo kwa kiasi kikubwa lilikuwa na wabunge wengi kutoka Chama Cha Mapinduzi.

"Mtu akizidi kukudharau unageuka jeuri halafu akiendelea inakuwa vurugu, sisi hatutaki vurugu, wananchi tulitoa maoni yetu na kuamua lakini wachache wanatudharau. Umoja wetu utatusaidia kutoa sauti moja, tunakuja na mabadiliko ya kimkakati na siyo ghafla ghafla,"anasema.

Mashinji ambaye kwa wakati huo alikuwa na miaka 43, anasema katika kujiimarisha zaidi kupigania haki kuna ambao watarudi nyuma, pembeni lakini wengine ni lazima kusonga mbele haki itakapopatikana.

Aidha, anasema wameunda kikosi cha kimkakati ndani na nje ya chama, ni imara na kinafanyakazi zake vizuri, na kutakuwa na kikosi cha kisiasa kinachoundwa na wabunge na kuwaagiza suala la katiba mpya kuwa agenda kuu kila wanaposimama kujadili hoja yoyote.

"Wao wana nguvu ya mabomu sisi tuna watu. Kwani watoto wao hawakai chini shuleni? tunawaonya wanaowapa amri polisi zisizo na tija na kuwafanya waishi kwa taabu uraiani...Kama itafika wakati tukashindwa kuvumilia yanayotokea turushe mikono juu lakini kama uvumilivu upo tusonge mbele tuna mipango tutatekeleza," anasema na kuahidi.

Dk. Mashinji anasema ni lazima sehemu zinazoongozwa na Chadema au Ukawa ustawi wa wananchi uonekane kuanzia taifa hadi matawini ili kufikia malengo sahihi ya ujenzi wa chama na taifa.

Katibu Mkuu huyo ambaye hana maneno mengi, anasema ni vyema wanachama na viongozi kufanyakazi kwa karibu kwa kuiga mfano wa maji ambayo huenda pamoja na wanapoangukia huanguka pamoja na hakuna lawama.

"Kila mtu ambebe mwenzie na tuchukuliane, tuige mfano wa maji. Sikuwahi kuonana uso kwa uso wala kukaa muda mrefu na kuongea na Mwenyekiti Mbowe zaidi tuliwasiliana kwa simu na barua pepe na alinijibu kwa wakati na sasa ameniteua kuwa Katibu Mkuu nifanye mambo ya kiutendaji ya chama," anasema.

Aidha, anasema chama kitaendelea na operesheni mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zimewezesha kuwafikia wanachama na wananchi wengine wengi.

Katibu Mkuu anasema wanachama watambue kuwa safari ya mabadiliko bado haijahitimishwa ndiyo imeanza kwa kuwa lengo ni kukamata dola, na kwamba wanaoiga waendelee kuiga lakini hawawezi kutoa kitu sahihi ambacho kimebuniwa na wengine.



Mashinji baada ya kukihama chama hicho akikaribishwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM , Humphrey PolePole.

Aidha, anaomba ushirikiano kwa viongozi na wanachama katika kukivusha chama na kuwataka kuweka kando makundi, chuki, kukataa rushwa inayotaka kumea ambayo ni jadi na desturi kwenye vyama vingine na kwamba ndani ya chama kila mtu ni sawa na hakuna aliye zaidi ya mwenzie.

**AMETEKELEZA?**

Licha ya kiongozi huyo kuahidi mengi mbele ya baraza hilo, lakini duru za kisiasa zinaeleza kuwa yalibaki kwenye makabrasha kuliko kutekelezwa kiasi cha kuingia kwenye migogoro na viongozi wa kitaifa wa chama hicho.

Aidha, zinaeleza kuwa kuondoka kwake ni kutoridhishwa na uamuzi wa kuondolewa katika nafasi hiyo nyeti ya kukitumikia chama hicho kikuu cha upinzani.

> Ndani ya Chadema kama una sifa zote unapewa fursa na siyo kusubiri kuhonga.

**MBOWE AMSIFU**

Kwa upande wake, Mwenyekiti Mbowe anasema alimfahamu zaidi Dk. Mashinji katika mgomo wa madaktari katika kutetea maslahi ya sekta ya afya na maboresho mbalimbali, lakini zaidi alivyoanza kuandika machapisho mbalimbali ambayo kwa kiasi kikubwa yaliisaidia Chadema

"Ndani ya Chadema kama una sifa zote unapewa fursa na siyo kusubiri kuhonga. Dk. Mashinji anashangaa kwa kuwa baba yake hayupo katika medani za siasa hivyo hajapewa nafasi kwa upendeleo au kujuana, unamjua nani bali kwa sifa zake," anasema Mbowe.

Huyo ndiye Mashinji kutoka Chadema na sasa ni mwana CCM.

## Uchaguzi serikali za mitaa DRC wapigwa tena kalenda




Makao makuu ya Tume ya Uchaguzi, huko Kinshasa, nchini DRC. **PICHA: RFI.**

**KINSHASA,** DRC

UCHAGUZI wa serikali za mitaa ambao awali ulipangwa kufanyika mwaka 2019 nchini Congo, hautarajiwi pia kufanyika mwaka huu. Nchi hiyo haiko tayari kuandaa uchaguzi huo, kwa mujibu wa Ripoti ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (CENI), ambayo pamoja na mambo mengine inataja matatizo makubwa ya ukosefu wa fedha na vifaa.

Katika ripoti yake, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imebaini kwamba ni vigumu kuandaa uchaguzi wa madiwani wa manispaa na madiwani wa sekta na wakuu wa maeneo mbalimbali, katika mazingira ya sasa. Sababu ya kwanza iliyotajwa katika ripoti hiyo ni ukosefu wa vifaa.

Aidha, imetaja ujenzi wa ofisi watakazotumia madiwani 11,000 kuwa hautawezekana kwa sasa. Taasisi hizo ni wabunge katika ngazi ya chini katika maeneo yao, bila kusahau fedha za matumizi ya ofisi na mishahara ya maofisa hao.

Katika ripoti yake iliyowasilishwa bungeni, CENI imependekeza kwamba idadi ya halmashauri za manispaa ipunguzwe.

Kwa upande wake, Waziri wa Mawasiliano na Vyombo vya Habari, David-Jolino Diwampovesa Makelele, alisema hakuna uamuzi wowote unaoweza kuchukuliwa kabla ya kupata matokeo ya uchaguzi.

Waziri huyo amekumbusha nia ya Rais Félix Tshisekedi ya kuandaa uchaguzi huo wakati wa muhula wake wa miaka mitano.

Aidha, CENI imependekeza kwamba, uchaguzi huo ufanyike mwishoni mwa muhula wa rais.

Licha ya kufikiria kufanya uchaguzi Congo imekuwa na tatizo la vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa watu kutekwa nyara na wengine kuuawa katika mashambulio yanayotekelezwa na waasi wa Uganda wa ADF.

Wiki iliyopita Februari 17 huko kijijini Alungupa wilayani Beni waasi hao walivamia kijiji na raia 15 waliuawa na wengine 10 kutekwa, wakiwamo watano kutoka familia moja.

Wakazi kadhaa wa kijiji hicho pia waliporwa mali zao. Waasi waliiba ng'ombe na vitu vya thamani, kwa mujibu wa vyanzo hivyo.

Naibu msemaji wa jeshi la DRC, FARDC, Brigadia Jeneral Sylvain Ekenge, alithibitisha habari hizo.

**Radio Ufaransa**

# Mapito ya Katibu Mkuu Mashinji na nyayo zake



Dk. Vincent Mashinji akizungumza na waandishi wa habari alipokuwa Chadema.

**Na Ani Jozeni**

KUIHAMA kambi ya upinzani kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji,na maelezo ya maofisa wa juu wa sekretariati ya chama hicho kuwa hakuwa anafuata itikadi ya chama hicho huenda imewachanganya wachunguzi wa habari na wafuatiliaji wa siasa au wote wanaoutakia mema upinzani.

Kuondoka kwa watu kama hao, kubezwa kunavunja imani ya ufuasi kama huo kwa chama kinachohusika. Ni katika mazingira hayo ambako bado mashabiki na wafuasi wa chama hicho na kwa kitaaluma zaidi wachunguzi wa habari kwa jumla wanaangalia kwa makini kutakuwa na athari gani kwa ufuasi na upigaji kura kwa chama hicho baada ya wimbi la makada kuondoka.

Makada hao hawakuondoka katika mazingira yanayofanana ila tofauti, kwa mfano kuna walioondoka mwanzoni baada ya kazi ya 'kutumbua majipu' kuanza. Pia kulikuwa na mabadiliko makubwa ya sera za matumizi ya serikali na kuanza kutekelezwa miradi mikubwa ya kimkakati nchini.

Licha ya kuwa kundi hilo lilikuwa kubwa halikutafsiriwa kuwa ni kielelezo cha kutoridhishwa na chochote katika upinzani, ila ni makada ambao ni vijana wenye uchangamfu na mabadiliko.

Wakawa wameona kuwa wanaweza kuelekeza nguvu zao na ari yao katika mabadiliko yanayoendelea, wakati wale wenye historia ndefu zaidi ya kuwa na matatizo na chama tawala au serikali waliendelea kutumikia ajenda za upinzani.

Ni kuondoka kwa watu kadhaa muhimu katika kundi hilo ambako sasa kunaleta wasiwasi, kwani si vijana wenye ari, ni wakongwe wa siasa.

> Licha ya kuwa kundi hilo lilikuwa kubwa halikutafsiriwa kuwa ni kielelezo cha kutoridhishwa na chochote katika upinzani, ila ni makada ambao ni vijana wenye uchangamfu na mabadi-



Aliyekuwa mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe ambaye pamoja na Mashinji wamekimbia Chadema hivi karibuni. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Unaweza kusema kimsingi kuwa hilo ndiyo kundi la kina Edward Lowassa, Federick Sumaye, Cecil Mwambe na Dk.Mashinji. Hapa tena siyo suala la ari kwani walikwenda huko kutokana na ari kukwamishwa CCM, na wamekwama tena wakati baadhi inaelekea wana maisha ya kisiasa baadaye, kama Mwambe au Dk. Mashinji kwani 'mcheza kwao hutuzwa.' Juhudi zao Chadema zimeonekana.

Kwa upande mmoja unaweza kuangalia suala hilo kama tatizo la mtu binafsi, kwa mfano kuondoka Chadema kuwe ni kielelezo cha kustaafu rasmi kwa mawaziri wakuu wa zamani waliofuatana kwenye kiti hicho, Lowassa na Sumaye.

Licha ya kuwa waliingia katika chama kwa kufuatana, hawakuunda kundi la Lowassa katika chama kwani walikuwa na ngazi na malengo tofauti, hivyo kuondoka kwao pia kunaashiria mambo yanayotofautiana.

Mchanganuo kama huo unamgusa Dk.Mashinji kuwa suala lake liangaliwe kama kada binafsi aliyefikia ngazi ya juu ya chama, kwani hakuwa na 'makandokando' ya uongozi uliotangulia unaofahamika, anaoulinda au hakuwa na 'Team Mashinji'.

Wako wanaosema kuwa kuondoka kwa makada hao ni ishara ya udhaifu wa wazi wa kambi ya upinzani katika uchaguzi mkuu mwaka huu, hisia ambayo inabidi ifafanuliwe inaelezea kitu gani hasa.

Kwa mfano kusema kutakuwa na udhaifu mwaka huu kimsingi inatakiwa iwe ni kuainisha kuwa upinzani hautafikia kura asilimia 35 au zaidi kwa jumla, na kwa maana hiyo Chadema peke yake kufikia asilimia 25 kwa mfano.

Hoja hiyo inaweza kuwa na mashiko kwa sababu upinzani miaka yote umefanya vyema zaidi ukipata makada kutoka CCM waliokwamishwa katika kuchuja watangaza nia ili kupata mgombea; haifahamiki kama watakuja kina nani.

Kinachoonekana ni kuwa vyama vya upinzani vinatanuka zaidi wakati wa uchaguzi kwa sababu wenye ajenda za moto (kwa hisia zao) halafu wanaokwama kwenye kura za maoni za chama tawala wanaona afadhali wajitoe na kuhamia upinzani.

Hali hiyo imeleta ushindani mkubwa katika uchaguzi mkuu pale nafasi ya urais inapokuwa wazi, na haijawa rahisi kupata mgombea anayeweza kumtetemesha rais anayetafuta muhula wa pili.

Ina maana kuwa kinga kubwa ya CCM mwaka huu siyo udhaifu wa upinzani kwani wangepata watu wapya wenye ajenda za kusukuma mbele, na hata baadhi ya waliopo nyota zao zikawaka kwa mng'aro zaidi katika uchaguzi mkuu wakubalike.

Kinga muhimu zaidi ya CCM ni kuwa rais anaendelea na muhula wa pili, na siyo rahisi kwa mgombea yeyote kutazamia kupambana na rais aliyeko madarakani na afaulu, nje ya kuwepo mazingira ya mkasa ambayo hayakuwahi kutokea awali. Ina maana kuwa zile asilimia 62.5 za kura kwa CCM na asilimia 7.4 kwa upinzani zitaendelea, na siyo ajabu ziboreshwe kwa kiasi fulani,kwani kuna mlolongo wa mashahidi dhidi ya upinzani na kuipendelea CCM mwaka huu.

Bila kuchomoka mtu anayeaminika kwa mapana na marefu, kuwepo upinzani imara siyo rahisi. Kwa upande wa Visiwani inawezekana kuwe na kukata tamaa kama Maalim Seif wa ACT-Wazalendo akisimama tena, kutokana na wimbi kama hilo la mashahidi.

Kimsingi inaelekea kuwa wimbi la kuondoka kwa makada Chadema siyo katu chanzo cha udhaifu wa kina kwani upinzani muda wote unajengwa na wale ambao kwa njia moja au nyingine wanachoshwa na utendaji wa serikali au kutokana na kukwamishwa kwa matazamio yao binafsi kama watu wenye ari na siasa.

Ni wazi kuwa awamu ya tano ilifaulu kuteka hisia na ari za makada hasa vijana kutoka upinzani, lakini haijadiliwi katu kuwa imejenga pia hisia kali tena za kina katika tabaka siyo dogo la marika yote. Tatizo ni kuwa kwa vile ni katikati ya awamu, ile shauku ya kuwa na 'mtu mwingine' haipo, kwa hiyo siyo rahisi kupata 'kigogo' kutoka CCM aje na wimbi la ushawishi miongoni mwa wananchi, au hata makada.

UCHAGUZI MKUU BURUNDI:

# Ni Agathon Rwasa dhidi ya kipenzi cha Nkurunziza

Na Mashaka Mgeta



Mgombea urais wa Burundi, Agathon Rwasa. **PICHA: MTANDAO**

CHAMA cha National Congress for Liberty (CNL), kimemteua Agathon Rwasa (56) kuwa mgombea urais wake katika uchaguzi Mkuu wa Mei 20, mwaka huu nchini Burundi, akitarajiwa kutoa ushindani mkali kwa mgombea wa chama tawala cha CNDD-FDD, Evariste Ndayishimiye.

Rwasa aliwahi kuwa kiongozi wa waasi na mpinzani wa `miaka nenda rudi' wa Rais Pierre Nkurunziza anayemaliza muda wa utawala wake kwa taifa hilo dogo lililopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Hii haitakuwa mara ya kwanza kwa Rwasa kuwania nafasi hiyo, kwani alishawahi kufanya hivyo katika Uchaguzi Mkuu wa 2010 na ule wa 2015, lakini alishindwa na kuyakataa matokeo yaliyompa ushindi Nkurunziza.

Mwaka 2015, Nkurunziza aliibua taharuki iliyosababishwa na mkanganyiko wa kuhusu kuwania urais katika muhula wa tatu, lakini yeye na waliokuwa wanamuunga mkono wakipuuzia madai hayo kwa kigezo kwanza, aliingia madarakani kwa mara ya kwanza kupitia makubaliano ya kumaliza mgogoro wa kisiasa uliokuwapo na si kwa kupigiwa kura na Warundi.

Uamuzi huo wa Nkurunziza ulisababisha machafuko, mapigano, umwagaji damu na mauaji kwenye maeneo tofauti ya nchini humo.

Takwimu zilizotolewa na vyanzo tofauti zilionyesha kwamba maelfu ya watu hasa waliokuwa wakiandamana kumpinga Nkurunziza, waliuawa hasa baada ya kupigwa risasi na askari wa ulinzi wa usalama.

Kwa wakati huo, upinzani ulimshutumu Nkurunziza kwa ukiukwaji wa katiba kupitia uamuzi wa kugombea tena urais.

Kwa hali hiyo, ushindani mkubwa katika Uchaguzi Mkuu ujao unatarajiwa kuwa kati ya Rwasa na Jenerali Ndayishimiye, anayetajwa kuwa rafiki wa karibu wa Nkurunziza.

"Kadri tunavyokaribia uchaguzi mkuu, inashangaza kusikia wapo watu wanaofikiria kuhujumu uchaguzi huo," Rwasa amekaririwa akiwaambia wajumbe wa chama chake baada ya kuteuliwa kuwania kiti hicho na kuongeza, "Warundi hawatakuwa tayari kuwaruhusu wayafanye hayo."

Kwa upande wake, Umoja wa Mataifa (UN) umetahadharisha kuhusu uwezekano wa kutokea ongezeko la ukiukwaji wa haki za watu kabla ya uchaguzi huo.

Nkurunziza, alikuwa anatarajiwa zaidi kutumia fursa ya mabadiliko ya Katiba yaliyofanyika nchini humo, kuwania tena urais, na hivyo kuibua hisia za kurejea kwa machafuko kama yale ya 2015.

Bunge la nchi hiyo, lilipitisha sheria ya malipo ya 'kiinua mgongo' yanayozidi Dola 500,000 na jumba la kifahari kwa rais anayetoka madarakani.

> Inyeshe mvua ama ianguke theluji, tunayaendeleza mapambano hadi tutakapochukua mamlaka ya kuiongoza Burundi. Hilo ni deni tunalodaiwa na Warundi wanaosubiri mabadiliko.



Evariste Ndayishimiye.

Kiasi hicho cha fedha kinalalamikiwa kwa madai kuwa hakilingani na uchumi wa taifa hilo linalotajwa kuwa na asilimia 65 ya raia wake wanaoishi katika 'umasikini wa kutupwa' wakati Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP) likieleza kwamba nchi hiyo ni miongoni mwa zinazokabiliwa na uhaba wa chakula.

Wakati Rwasa akitangazwa kuwania urais, taarifa za awali zilienezwa kwamba alikuwa na mpango wa kwenda kuishi uhamishoni kufuatia kushamiri kwa vitendo vya 'mawakala' wa serikali kuwatesa wapinzani nchini humo.

"Unaniuliza kama ninakwenda uhamishoni ama kwenda kujificha? Hapana. Siendi huko. Nenda ukawaambie hakuna suala la kwenda uhamishoni, hakuna suala la kwenda kujificha. Tunachokifanya ni maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu," Rwasa aliwaambia waandishi wa habari jijini Bunjura hivi karibuni.

Rwasa alikosoa jitihada zinazofanywa kukihujumu chama chake katika uchaguzi mkuu huo, na kuwataka wanaharakati wake wasikate tamaa kutokana na hali ngumu ya kisiasa inayowakabili.

Lengo la mipango yao ni kuifuta CNL, kujaribu kumuumiza Rwasa, kuwapandikiza wapinzani ndani ya CNL kupitia uchaguzi huo," akasema.

Burundi itafanya uchaguzi mkuu wa kumchagua rais, wabunge na wajumbe wa mabaraza ya umma, kwa mujibu wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Kampeni za uchaguzi huo zimepangwa kuanza Aprili 27 na kumalizika Mei 17, mwaka huu.

"Inyeshe mvua ama ianguke theluji, tunayaendeleza mapambano hadi tutakapochukua mamlaka ya kuiongoza Burundi. Hilo ni deni tunalodaiwa na Warundi wanaosubiri mabadiliko," Rwasa amesema.

Kuhusu kuwapo matukio ya wanaharakati wa chama chake kukamatwa mara kwa mara, Rwasa anasema hali hiyo haiwatishi kwa vile matukio hayo hayawezi kufanyika kwa wanachama wake wote.

Rwasa anasema chama chake kimejiandaa kuwekeza katika kutangaza siasa za maridhiano na kuzitaka mamlaka za kwenye manispaa kuheshimu haki na uhuru wa raia wa Burundi.

Anayasema hayo alipokuwa akizungumzia matukio ya unyanyasaji katika manispaa ya Gashikanwa ambapo utawala wa eneo hilo ulifanya mkutano wa hadhara kuhusu usalama Oktoba mwaka jana, baadaye ukapingwa na wananchi.

"Ni masikitiko kuona jinsi watumishi wengi wa manispaa wanaminya haki na uhuru wa raia kujieleza pasipo kuchunguzwa," akasema.

Kwa mujibu wa shirika la Human Rights Watch, matukio ya ukiukwaji wa haki za biadamu yameshamiri nchini humo hasa baada ya kusajiliwa kwa chama cha CNL na mabadiliko ya Katiba yaliyoongeza muda wa urais kufikia miaka saba kutoka mitano ya awali.

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali.***



Wanamgambo wa 'Janjawid' wanaojipamba kwa risasi, wanadaiwa kuua watu weusi takribani 300,000 kwenye jimbo la Darfur nchini Sudan. **PICHA: MTANDAO.**

# Baada ya miongo kadhaa, al Bashir sasa kutinga ICC

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 2006 Kofi Annan, akiwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), aliionya Serikali ya Sudan na kumwambia rais wa zamani wa taifa hilo, Omar al Bashir kwamba atawajibika kutokana na mauaji ya kimbari katika jimbo la Darfur.

Miaka 14 baadaye, utabiri wa Annan huenda ukatimia baada ya serikali mpya ya Sudan, iliyoingia madarakani kwa kumuondoa Omar al-Bashir, imesema inakusudia kumfikisha kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita mjini The Hague.

Japo hatakuwapo kushuhudia utabiri wake, akiwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayemaliza muda wake, alimuonya al Bashir na serikali ya Sudan kuwa watawajibika kuchukua dhamana kwa jumla kuhusiana na uhalifu uliofanywa katika jimbo la Darfur.

Licha ya kwamba Annan alifariki dunia mwaka juzi, alisema kuwa serikali ya Khartoum imekataa kukubali msaada kutoka katika jumuiya ya kimataifa ili kuzuia mauaji, ubakaji na uharibifu wa wanavijiji katika jimbo hilo la magharibi ya nchi hiyo, lakini itabeba lawama.

Alimkumbusha Omar al-Bashir, kuwa katika mkutano wa Novemba 2003 mjini Abuja , viongozi wa Afrika ikiwamo Bashir , walikubaliana kuhusu ujumbe wa nyongeza wa umoja wa mataifa , ili kuimarisha kikosi cha sasa cha mataifa ya Afrika cha kulinda amani ambacho wakati huo kilikuwa

> Mwezi Julai mwaka 2003 mahakama ya ICC ilitangaza waranti wa pili wa kukamatwa kwa Rais Bashir kutokana na mashtaka ya uhalifu wa kivita katika jimbo la Darfur.

na wanajeshi 7,000 katika jimbo la Darfur, lakini hakuonyesha ushirikiano.

Tangu mapema 2003, wanamgambo wa Janjaweed (janjawid) wenye asili ya Kiarabu, wanaoungwa mkono na Sudan pamoja na Libya na waasi wengine walikuwa wakipigana vita ambavyo vimesababisha watu 300,000 kupoteza maisha.

Hivi karibuni serikali mpya ya Sudan, imeeleza kuwa wale wanaotafutwa na mahakama ya kimataifa ya ICC, watafika mahakamani kukabiliana na mashtaka ya mauaji ya kimbari na uhalifu wa kivita katika jimbo la Darfur, ambalo pamoja na kuuawa, wanawake walibakwa, watu kuteswa na kuacha mahangaiko mengi kwa wakazi wa Dafur.

Kwa maelezo hayo uamuzi huo unafungua njia kwa rais wa zamani kupelekwa the HagueUholanzi kujibu mashtaka ya mauaji yaliyofanyika takribani miongo miwili iliyopita.

Kadhalika, serikali ya Sudan imeendelea kusisitiza kuwa al Bashir na makundi mengine ya waasi watamkabidhi Omar al-Bashir kwa wakuu wa ICC ili kujibu mashtaka dhidi yake.

Ujumbe huo unatolewa na Waziri wa Habari, Faisal Saleh, aliyezungumza na shirika la habari la Reuters mwanzoni mwa mwaka mwezi huu.

Bashir ambaye aliondolewa madarakani na jeshi mwaka jana kutokana na maandamano ya umma, kwa miaka 17 sasa amekuwa akisakwa na ICC kwa mashitaka ya uhalifu dhidi ya binadamu na mauaji ya halaiki yanayohusiana na mgogoro wa Darfur. Hata hivyo, tangu kuangushwa kwake Aprili mwaka jana, amekuwa kizuizini mjini Khartoum, kwa mashitaka ya ufisadi na mauaji ya waandamanaji.

Mahakama ya The Hague- ICC imemfungulia mashtaka kiongozi huyo wa zamani wa Sudan pamoja na wasaidizi wake wa zamani watatu kwa makosa ya mauaji ya halaiki, uhalifu dhidi ya ubinadamu na uhalifu wa kivita katika jimbo la Darfur kufuatia mgogoro wa kikatili uliozuka mwaka 2003.

Takriban watu 300,000 waliuawa na mamilioni ya wengine waliachwa bila makazi ulipozuka mgogoro huo.

### ICC KUMSAKA

Historia ya kumsaka ilianzishwa na Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Mahakama ya ICC wakati huo Luis Moreno Ocampo, aliyesema kuwa mauaji ya halaiki bado yalikuwa yanaendelea katika jimbo la Darfur nchini Sudan na kuwa rais wa nchi hiyo Omar al-Bashir alistahili kukamatwa.

Wakati anayasema hayo alitangaza kuwa ICC ilishatoa waranti wa kukamatwa al Bashir ili afikishwe kwenye mahakama hiyo lakini aliendelea kujificha na kuihadaa jamii ya kimataifa kuhusu yaliyokuwa yakiendelea Dafur.

Luis Moreno Ocampo katika uongozi wake aliliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) wakati huo kuwa Serikali ya Sudan haishirikiani na Mahakama ya ICC au kuwachukulia hatua zozote wahusika wa vitendo vya mauaji ya halaiki.

Ocampo alisema kuwa kwa miezi sita mwaka 2003 mamia ya raia katika jimbo la Darfur waliuawa na maelfu ya wengine kulazimishwa kuhama makwao huku zaidi ya watu 2,000,000 wakiendelea kuteseka.

Mwezi Julai mwaka 2003 mahakama ya ICC ilitangaza waranti wa pili wa kukamatwa kwa Rais Bashir kutokana na mashtaka ya uhalifu wa kivita katika jimbo la Darfur.

Januari mwaka huu zaidi ya watu 20 waliuawa katika vurugu za Darfur Magharibi na taarifa kamili zilisema wananchi takribani 24, walithibitishwa kuuawa baada ya kambi ya kuhifadhi waliopoteza makazi nchini Sudan kuvamiwa.

Kabla ya hapo kambi ya Krinding, ilivamiwa mnamo Desemba 29 hadi 30 kufuatia mzozo kati ya makundi ya asili ya Kiarabu na Kiafrika.

Kudumisha amani katika jimbo la Darfur pamoja na maeneo mengine ya Sudan ni moja wapo ya changamoto kubwa zinazoikabili serikali mpya ya nchi hiyo tangu kuondoshwa madarakani raia wa zamani Omar al-Bashir, ambaye anadaiwa kuhusika na kusaidia makundi ya Janjaweed yaliyokuwa yakitimiza mashambulizi hayo.

Mgogoro mkubwa ulizuka Darfur mnamo mwaka 2003, baada ya waasi wengi wao waliokuwa si wenye asili ya Kiarabu kupambana na serikali ya mjini Khartoum.

Hadi sasa Umoja wa Mataifa unakadiria kuwa watu wapatao 300,000 wameuawa na wengine milioni 2.5 kupoteza makazi, mali na hatma ya maisha yao na kwamba kati yao watu 180,000 walipoteza makazi Darfur Magharibi.

Mapigano baina ya Waarabu dhidi ya makundi ya watu weusi na ubaguzi wa rangi na chuki dhidi ya kundi hilo ndicho kilichosababisha Sudan kugawanywa na kuwa na mataifa mawili la Sudan na Sudan Kusini. **MITANDAO**







# Aliyepewa tuzo na JPM atoboa siri mafanikio

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

ALIYEKUWA Tabibu wa Zahanati ya Uturo iliyopo katika Wilaya ya Mbarali, Wilson Chotamganga, ameeleza siri iliyoifanya zahanati hiyo kuwa ya mfano nchini kwa kuzuia vifo vya mama na mtoto kwa miaka 20.

Tabibu huyo ni yule aliyepewa tuzo maalumu ya kutambua mchango wake kwenye kukabiliana na vifo vya mama na mtoto Ikulu jijini Dar es Salaam na Rais John Magufuli, wakati alipokuwa anazungumza na madaktari.

Akizungumza na viongozi wa Mkoa wa Mbeya jana katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Chotamganga alisema kuna siri kubwa ambayo aliikuta katika vijiji vinavyohudumiwa na zahanati hiyo ikiwamo ya kuzika ndani watoto waliozaliwa wakiwa wamefariki maarufu kwa jina la 'sio riziki'.

Alisema mara ya kwanza wakati anafika katika zahanati hiyo mwaka 1993 alikuta kuna msiba wa mwanamke ambaye alifariki wakati anajifungua kwa mganga wa jadi na alipofuatilia zaidi alibaini kuwa mwanamke huyo alikuwa wa tatu ndani ya kipindi kifupi.

Alisema aliendelea kufuatilia na kubaini kuwa kulikuwa na vifo vingi vya mama na mtoto na hivyo akaamua kuanza kuchukua hatua za kukabiliana na vifo hivyo kwa kuwashirikisha wananchi wa maeneo yote ya vijiji.

"Nilitaka kujua vile vifo vya watoto wachanga na kinamama wajawazito vilikuwa vinasababishwa na nini? Walikuwa wanakufa kwa sababu ya kung'atwa na papasi ama kwa sababu ya malaria? Nilichobaini ni kwamba wengi walikuwa wanajifungulia nyumbani na kwa wakunga wa jadi," alisema Chotamganga.

Alisema baada ya kubaini mazingira hayo aliamua kuanza kutoa elimu kwa wananchi kupitia mikutano mbalimbali ya vijiji kuhusu umuhimu wa kujifungulia kwenye vituo vya afya na kuachana na wakunga wa jadi.

Chotamganga alisema wananchi wa vijiji hivyo walielewa na wakaungana naye kukabiliana na vifo hivyo kwa kuunda kamati maalumu ya wanawake makomandoo ambao walikuwa wanafuatilia afya za wajawazito wote.

"Tuliweka utaratibu wa kila mwanamke akibainika kuwa ni mjamzito, yeye na mwenza wake, wanachukuliwa na makomandoo wanaandikiwa ujumbe wanakuja zahanati kwa pamoja kwa ajili ya kufungua kadi na kupewa elimu," alisema Chotamganga.

Aliongeza kuwa waliweka adhabu ya Sh. 50,000 kwa mwanamke yeyote ambaye atajifungulia nyumbani ama kwa mkunga wa jadi na faini ya Sh. 5,000 kwa mjamzito ambaye hahudhurii kliniki hali ambayo iliwalazimu wote kujifungulia kwenye zahanati hiyo ya Uturo.

Alisema baada ya kutekelezwa vizuri kwa sheria hiyo ndogo hakujawahi kutokea kifo cha mama na mtoto tangu mwaka 1999 mpaka sasa na kwamba waliokuwa wakunga wa jadi ndio waliokuwa wanaongoza kuwahamasisha wajawazito kwenda zahanati.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariamu Mtunguja, alimpongeza Chotamganga kwa utendaji kazi wake na kwamba sifa ambayo Zahanati ya Uturo imepata kwa sasa ni sifa ya mkoa mzima wa Mbeya.

Alisema kwa sasa serikali inafanya mipango ya kuandaa muundo maalumu wa kukabiliana na vifo vya mama na mtoto kwa kutumia utaratibu wa Uturo ambao utakuwa unatumika nchi nzima.

"Nakuhakikishia kuwa kabla muundo huu haujaanza kutumika maeneo mengine nchini, sisi tutakuwa tumeshaanza kuutumia katika maeneo yote ya vituo vya kutolea huduma ili kuonyesha uhalisia wa muundo," alisema Mtunguja.

Aliwataka watumishi wengine wa afya katika mkoa huo kuiga mfano wa Chotamganga kwenye utoaji wa huduma kwa wananchi ili kuokoa maisha ya wananchi.



Aliyekuwa Tabibu wa Zahanati ya Uturo, iliyopo katika Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Wilson Chotamganga (katikati), akipongezwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, baada ya kupewa tuzo maalumu na Rais Dk. John Magufuli kwa kufanya vizuri kwenye vita ya kukabiliana na vifo vya mama na mtoto. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Matumizi Shilingi na Kwacha yaanza

**Na Grace Mwakalinga, TUNDUMA**

NCHI za Tanzania na Zambia zimeanza kutekeleza makubaliano ya urasimishaji wa matumizi ya Shilingi na Kwacha bila kubadilisha, hatua ambayo itarahisisha shughuli za kibiashara kwa wananchi wa nchi hizo mbili.

Akizungumza juzi katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe, wakati wa uzinduzi wa makubaliano hayo, Mkurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Tawi la Mbeya, Ibrahim Malagoi, alisema utaratibu huo ni utekelezaji wa makubaliano ya nchi wanachama wa Sadc, ili kurahisisha shughuli za kibiashara kwenye mipaka ya nchi hizo.

Alisema kuwa utaratibu huo utazinduliwa rasmi katika mpaka wa Tanzania na Zambia kuanzia Februari 28, mwaka huu Ijumaa na kwamba kwa sasa maofisa wa Benki Kuu za Tanzania na Zambia wapo kwenye zoezi la kutoa elimu kwa wananchi wa mipakani.

Malagoi alisema hatua hiyo imetokana na makubaliano kati ya serikali za nchi hizo mbili yaliyofanyika Septemba 21, 2018 ya kuruhusu fedha za Kwacha na Shilingi kutumika katika shughuli za kiuchumi bila kuzibadilisha katika eneo la Nakonde na Tunduma.

"Baada ya makubaliano hayo wataalamu walikaa na kutengeneza mwongozo wa namna ya kutekeleza makubaliano hayo, ambapo pia tulitakiwa kuwa na mashine ambazo zimeweza kugundua kama fedha zipi ni halali na hilo jambo tumelifanya ili kuhakikisha tunatambua alama za usalama kwenye fedha zetu," alisema.

Alisema benki hiyo imechukua hatua ya kuandaa benki nyingine za kibiashara kwa ajili ya mfumo huo kwa kuwa wao ndio wadau wakubwa, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya viongozi wa mkoa wa Songwe na wafanyabiashara wa eneo hilo kwa ajili ya utayari wa kutekeleza makubaliano hayo.

Kwa mujibu wa Malagoi, faida za urasimishaji huo ni pamoja na kuondoa gharama za ubadilishaji wa fedha ambapo wananchi wa Tanzania wanatumia shilingi upande wa Zambia na Wazambia watatumia Kwacha upande wa Tanzania bila kubadilisha.

Kwa upande wake Meneja wa Benki ya CRDB, Tawi la Tunduma, Chrispin Kombo, alisema benki yake imejipanga kwa ajili ya mfumo huo mpya na kueleza kuwa utaongeza chachu ya mzunguko wa fedha na kukuza uchumi wa wananchi wa nchi hizo mbili.

# Halmashauri zapigwa 'stop' ubia ujenzi wa mabanda

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amepiga marufuku halmashauri zote za mkoa huo kuingia ubia na wananchi kwenye ujenzi wa vibanda vya biashara kwenye masoko ya serikali na badala yake akaziagiza zijenge kwa fedha za umma na wananchi wabaki kuwa wapangaji.

Chalamila alipiga marufuku hiyo juzi wakati Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mkoa huo ilipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Soko la Tunduma Road lililopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi wilayani Mbeya.

Alisema miradi hiyo ambayo ujenzi wake hauzidi gharama ya Sh. milioni 300 inatakiwa ijengwe na halmashauri zenyewe kwa kutumia mapato ya ndani badala ya kuwapa wananchi wajenge wenyewe.

"Haya ni maeneo ya umma na masoko ni ya serikali, sasa ni marufuku kutumia fedha za wananchi kuingia kwenye ubia wa aina hii, jengeni wenyewe likikamilika waambie wananchi waje kupanga ili anayetaka apange na asiyetaka aache," alisema Chalamila.

Aliwataka viongozi wa halmashauri zote kuzingatia utaratibu huo ili miradi hiyo ijengwe kwa kasi na serikali ianze mapema kukusanya mapato tofauti na ilivyo sasa ambapo wananchi wanaanza kujilipa gharama zao kwanza.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa soko hilo, Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Wilson Nyamala, alisema vibanda vya soko hilo vinajengwa na wafanyabiashara wenyewe kwa makubaliano maalumu ya kujilipa kidogo kidogo kupitia kodi.

Alisema makubaliano waliyoingia na wafanyabiashara hao ni kujenga kila kibanda kwa Sh. milioni 1.5 na kwamba kodi ambayo itatakiwa kila mfanyabiashara alipe ni Sh. 50,000 kwa mwezi ambayo itagawanywa mara mbili.

"Nusu ya kodi itaingia halmashauri na nusu nyingine atabaki nayo mfanyabiashara kwa ajili ya kujilipa gharama za ujenzi na watakapokuwa wamerejesha gharama zote, kodi yote itakuwa inaingia halmashauri," alisema Nyamala.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, aliitaka halmashauri hiyo kusimamia ubora wa vibanda hivyo kwa maelezo kuwa kwa sasa soko hilo limejengwa ovyo.

Alisema wafanyabiashara wanajengea matope badala ya saruji na kwamba hata uezekaji limeezekwa ovyo kwa kila mmoja kuezeka kwa mfumo wake badala ya kuviweka katika mfumo mmoja.





# 'Mikoa 10 haijafanya mabaraza ya biashara'

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema mikoa 16 kati ya 26, ndio imefanya mabaraza ya biashara.

Jafo alitoa kauli hiyo katika uzinduzi wa mwongozo wa majadiliano kati ya sekta ya umma na binafsi katika ngazi ya mikoa na wilaya uliofanyika jijini hapa.

Alisema mwongozo huo ni kitendea kazi katika ngazi hizo kitakachosaidia kuendesha mabaraza hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yataleta tija.

"Takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mikoa 26 ni mikoa 16 pekee ambayo ilifanya mabaraza hayo, sasa mwongozo umeshatolewa hivyo miongoni mwa taarifa za wakuu wa mikoa zinazoletwa Tamisemi lazima taarifa ya Uendeshaji wa Mabaraza ya Biashara katika mikoa yenu iwepo," alisema.

Akizungumza baada ya kuzindua mwongozo huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema kuwa majadiliano ya mabaraza hayo yanayofanyika katika ngazi ya taifa, mikoa na wilaya na yameendelea kusaidia uchumi wa nchi kuimarika.

Alisema mabaraza ya biashara yalikuwa hayafanyiki vizuri kwa sababu watu walikuwa wanashindwa kutumia mazingira waliyonayo kujipanga kuendesha mabaraza hayo.

"Ili kuwa na utendaji unaotukuka lazima tuwe na mwongozo wa nini kifanyike, wakati gani, kwa utaratibu upi na kwa rasilimali zipi, hatuwezi kuzungumza uchumi wa viwanda wala utekelezaji wa Dira ya Maendeleo bila sekta binafsi, hivyo kuna kila haja ya kutengeneza mazingira wezeshi yatakayoifanya sekta ya umma isaidiane na ishirikiane kwa karibu na sekta binafsi ili yaliyopangwa yaweze kutekelezwa," alisema.

Naye Katibu Mtendaji wa Baraza la Biashara la Taifa, Dk. Godwill Wanga, alitoa wito kwa wadau wote kutumia majadiliano hayo kuainisha matatizo ya miradi ya pamoja kati ya sekta hizo mbili ili kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPFS), Rehema Mbogi, alisema kuwa serikali imeonyesha umakini katika masuala yanayohusu majadiliano kati ya sekta binafsi na umma katika ngazi zote.

**"Ili kuwa na utendaji unaotukuka lazima tuwe na mwongozo wa nini kifanyike, wakati gani, kwa utaratibu upi na kwa rasilimali zipi, hatuwezi kuzungumza uchumi wa viwanda wala utekelezaji wa Dira ya Maendeleo bila sekta binafsi, hivyo kuna kila haja...**

# Mongella awapasha ukweli viongozi wanawake bungeni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

RAIS wa kwanza wa Bunge la Umoja wa Afrika (AU), Dk. Getrude Mongella, amesema ni hasara kuwa na wanawake viongozi bungeni ambao wanaona aibu na kigugumizi kuzungumzia masuala ya wanawake.

Kauli hiyo aliitoa jana katika kikao cha utambulishaji wa Mtandao wa Viongozi Wanawake Afrika (AWLN), tawi la Tanzania ambao unatarajiwa kuzinduliwa leo na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, na unaratibiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya wanawake (UN Women).

Mongella ambaye ni mraghibishaji wa kijamii katika mtandao huo, alisema wanatakiwa wanawake ambao wanazungumzia masuala ya maendeleo ya wanawake na wawe wanayajua na kuyapenda.

"Ninapotaka kuangalia lile bunge siku itafikia idadi ya 50 kwa 50 sitajali wewe umetokea chama gani isipokuwa nitajali kama wewe kweli mambo tunayozungumza hapa unayajua na kuyapenda," alisema.

Aliongeza: "Kama mtu anaingia bungeni kama anakwenda kwenye Maonyesho ya Sabasaba ni heri nimpigie mwanaume, ni hasara kama tutakuwa na viongozi wanaoona aibu au kigugumizi kuzungumza maendeleo ya wanawake."

Akizungumzia kuhusu uchaguzi mkuu, alisema mwaka huu ni wa uchaguzi hivyo mtandao huo ulipaswa kuwa umefikisha mawazo kwa wanaoandika ilani za uchaguzi ili kuwa na sauti kubwa ya kusemea masuala hayo.

"Wanawake watakaogombea waende mbele. Pia tuwasaidie wasichana wetu kuwa viongozi, tuweke nguvu eneo hili ili wachukue nafasi zetu tutakapoondoka," alisema.

Aidha, alisema kunahitajika uwezeshaji wanawake kiuchumi kiuongozi na kiutawala na mtandao huo unalenga kuangalia rasilimali ya viongozi wanawake waliopo na kuwataka kutofanya kazi kwa mazoea.

"Hii kazi tumetoka nayo mbali baada ya mkutano wa Beijing, safari hii upele umepata mkunaji, mtoto anazaliwa baada ya miaka 25 ya Beijing, mtoto anayezaliwa awe king'ang'anizi, awe mpaka kieleweke, tutumie nguvu ya kuongoza jamii, tunataka kujenga chombo chenye watu wenye kiherehere, ving'ang'anizi na ambaye hataki kuwa hivyo apite aondoke," alisisitiza.

Akizungumzia kuhusu uzinduzi wa mtandao huo, mwenyekiti mwenza wa mtandao, Mary Rusimbi, alisema mtandao huo utashughulika kwenye vipaumbele sita ambavyo ni pamoja na amani na usalama wa wanawake, wanawake wanaoishi vijijini, uhamasishaji wa kijamii, viongozi vijana wanawake.

Vingine ni masuala jumuishi ya kifedha na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na wanawake katika uongozi na utawala.

Naye, Mwakilishi wa UN Women Tanzania, Hodan Addou, alisema uzinduzi wa mtandao huo utahusisha viongozi 60 wanawake waliotambuliwa na kamati tendaji ya mtandao huo mwaka jana baada ya kupitia maombi yao na pia watendaji kutoka serikalini, UN na wajumbe wa kibalozi.

Alisema jitihada na mikakati ya mtandao huo itasaidia kwenye masuala mbalimbali ikiwamo katika kukabiliana na mimba na ndoa za utotoni.



Mama na mtoto wake wakijaribu kuvuka katika Barabara ya Sido, jijini Dodoma jana, huku wakichukua tahadhari ya magari na dimbwi la maji, lililotokana na mvua zilizonyesha katika jiji hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Finland waitwa kuwekeza viwanda vya mazao misitu

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolph Mkenda, ametangaza fursa kwa wawekezaji kutoka Finland kuwekeza kwenye viwanda vinavyotumia mazao ya misitu na utalii.

Prof. Mkenda alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kupokea ugeni wa Waziri wa Maendeleo ya Ushirikiano wa Kimataifa na Biashara wa Finland, Ville Skinnari.

Alisema serikali imetangaza fursa hiyo kutokana na uzoefu wa nchi hiyo katika sekta ya misitu.

"Tumewaalika walete wawekezaji katika eneo la viwanda vya mazao ya misitu kutoka Finland, kwa sababu katika eneo hilo wanautaalamu mzuri sana," alisema.

Aidha, Prof. Mkenda aliwahakikishia Finland kuwa serikali imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ufanyaji biashara na hatua itakayokuza uchumi.

Katibu huyo alisema pia Finland wawekeze katika sekta ya utalii ambayo kwa Tanzania ina fursa kubwa katika eneo hilo.


"Mbali na utalii wa Zanzibar na ule wa ukanda wa kaskazini mwa nchi, kuna fursa kubwa katika ukanda wa kusini, tungependa kuwaona, waje, watembee na waangalie namna ya kuja kuwekeza, kwani wakiwekeza itasaidia sana katika kukuza na kuutangaza utalii katika nchi zote za Scandinavia," alisema.

Vile vile, alisema nchi hizo mbili zimekubaliana kuongeza idadi ya watalii kutoka Finland watakaotembelea Tanzania katika miaka ijayo.

"Tunashukuru kwa ushirikiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na Finland, Finland amekuwa rafiki mwema na tunaimani kuwa tutakuwa na ushirikiano zaidi ambao utasaidia kuinua uchumi wa taifa na wananchi wetu," alisema.

Naye Waziri wa Maendeleo ya Ushirikiano wa Kimataifa na Biashara wa Finland, Skinnari, alisema Tanzania na Finland zimekuwa na ushirikiano wa takriban miaka 50 katika nyanja mbalimbali na kuwa kwa sasa wanaangalia namna ya kuzidi kuimarisha ushirikiano kwa miaka mingi ijayo.

Skinnari alisema kwa upande wa viwanda, nchi yake imepiga hatua hususani katika sekta ya misitu, teknolojia ya habari(ICT) na kusisitiza kuwa ndio baadhi ya mambo ambayo wamelenga kushirikiana na Tanzania.



# Serikali yafanya utafiti vituo vya afya

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, imesema katika utekelezaji wa ugatuzi kupitia vituo vya afya, imefanya utafiti wa awali kwa vituo vyake vyote vya Unguja na Pemba ili kubaini mahitaji ya huduma za msingi ikiwamo huduma ya majisafi na salama.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Konde, Omar Seif Abeid.

Mwakilishi huyo alitaka kujua kama serikali ina mpango wa kuchimba visima katika vituo vya afya na kufunga mashine ambazo zitatatua tatizo la upatikanaji wa maji katika vituo hivyo.

Naibu Waziri Khamis alisema kupitia utafiti huo, vituo 19 kati ya 162 vimebainika vina ukosefu wa huduma ya majisafi na salama.

Alisema ofisi yake kwa kushirikiana na Mamalaka ya Majisafi na Salama Zanzibar, imeandaa mikakati ya kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo ikiwamo kuchimba visima katika maeneo ya vituo vyenye matatizo hayo pamoja na kuimarisha miundombinu ya huduma hiyo.

Alisema wizara yake inatambua kwamba vituo vyake vingi havina huduma ya ulinzi hivyo kupitia mwaka wa bajeti 2020/2021 wamepanga kuongeza idadi ya walinzi ambao watakidhi haja katika vituo vyote vya Unguja na Pemba.

"Mheshimiwa Spika, tatizo la uhaba wa bajeti uliopo ndiyo linasababisha kutokuwa na ajira za walinzi wa kutosha," alisema na kuongeza kuwa wizara yake imeweka kipaumbele kuajiri walinzi watakaokidhi mahitaji katika mwaka ujao wa fedha.



Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya Haji (kulia), akiteta jambo na Mwakilishi wa Jimbo la Nungwi, Ame Haji Ali, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri atamba uchumi kukua

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Balozi Muhamed Ramia Abdiwawa, amesema mwelekeo wa uchumi kwa mwaka 2020 unategemea kwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa mwelekeo wa hali ya uchumi, mpango wa maendeleo na bajeti kwa mwaka 2020/2021 na 2022/2023.

Alisema Serikali ya Zanzibar itaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wake na kuimarisha ustawi wa maisha ya wazanzibari kwa kufanyia kazi zaidi maeneo ya msingi ya ukuaji wa uchumi ikiwamo kuimarisha sekta ya utalii na viwanda vidogo.

Alisema pato la taifa kwa mwaka 2020 linatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 7.3 kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa uwekezaji wa mitaji kwa serikali na sekta binafsi, kuimarika zaidi kwa utalii, viwanda, kilimo, ufugaji na uvuvi.

Balozi Ramia alisema shabaha na malengo ya uchumi kwa mwaka 2020/2022 ni kasi ya ukuaji wa pato halisi la taifa kwa miaka mitatu, ikitarajiwa kuwa kati ya asilimia saba na tisa.

"Shabaha nyingine ni kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei kuwa ya wastani wa chini ya asilimia tano kwa kipindi cha miaka mitano," alisema.

Aliongeza kuwa mapato ya ndani kwa kipindi cha miaka mitatu yanakadiriwa kufikia wastani wa asilimia 26 ya pato la taifa kutoka asilimia 24.2 mwaka 2018/2019.

Alisema matumizi ya serikali kwa kipindi cha miaka mitatu yanakadiriwa kufikia wastani wa asilimia 39.4 ya pato la taifa kwa kipindi cha miaka ya 2019/2022 kutoka wastani wa asilimia 38 kwa mwaka wa 2018/2019 na kuendelea kuwapo kwa amani na utulivu.

Makamu Mwenyekiti wa kamati kuhusu mwelekeo wa hali ya uchumi, mpango wa maendeleo na bajeti kwa mwaka 2020/2021 na 2022/2023, Bahati Khamis Kombo, alisema bado kuna tatizo la kutofikia matarajio ya mapato kutokana na kukosekana kwa mapato ya nje kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Alisema kamati inaamini kuwa miongoni mwa maeneo muhimu katika kuchochea maendeleo ya Zanzibar ni pamoja na uimarishaji wa sekta ya elimu na uendeshaji wa bandari ya mafuta na gesi.

# Shein aiagiza wizara kukutana na wakulima

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameutaka uongozi wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kukutana na wakulima ili kufanikisha dhamira ya kuwapo matumizi ya mbegu bora za kilimo.

Dk. Shein alitoa agizo hilo Ikulu Zanzibar, alipopokea taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi ya wizara hiyo kwa kipindi cha Julai hadi Dsesemba mwaka jana.

Alisema pamoja na matumizi ya vyombo vya habari kuwa na mchango mkubwa katika uhamasishaji wa matumizi bora ya mbegu za kilimo, ni vyema wataalamu na watendaji wa wizara hiyo wakakutana na wakulima kwa kuzingatia uzito wa jambo hilo.

Alisema uhamasishaji wa matumizi ya mbegu bora ni jambo zito na linalohitaji kupewa umuhimu na kuwa endelevu ili kuleta matokeo chanya katika kilimo, hasa cha mpunga.

Aliitaka wizara hiyo kuwa na mipango mizuri ya mafunzo kwa watendaji wake ili kuondokana na matatizo mbalimbali na kuwa na mipango mbadala katika kuyapatia ufumbuzi.

Alisema ni vyema kukawa na utaratibu maalum utakaotekelezwa kwa awamu tofauti kulingana na bajeti.

Dk. Shein aliipongeza wizara hiyo kwa juhudi za kuwaendeleza kielimu watendaji wake kwa lengo la kukuza uwezo wao.

Aliutaka uongozi wa wizara kukaa pamoja na watendaji wa Halmashauri za Wilaya na kuangalia namna ya kuwapo usimamizi mzuri katika uendelezaji wa masoko yalioko kwa kuwa na mipango bora katika upangaji wa bidhaa zao.

Pia aliutaka uongozi wa wizara hiyo kutuma waraka serikalini na kuelezea ukubwa wa vikwazo vinavyojitokeza katika ushughulikiaji wa kilimo cha mpunga kinachotegemea mvua.

Alisema kuwapo kwa taarifa za kuchelewa kuanza kazi za kilimo hicho, kwa madai ya wakulima kuchelewa kutuma fedha za kuchangia gharama za ukulima kwa mategemeo ya fedha hizo kulipwa na wabunge au wawakilishi, hakuendani na azma na dhamira ya serikali katika uimarishaji wa kilimo cha mpunga.

Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, aliutaka uongozi wa wizara hiyo kuhakikisha kila mara unatoa msukumo na misaada kwa wakulima, wafugaji na wavuvi nchini kote, ili kupata mafanikio zaidi katika shughuli zao.

Alisema katika siku za hivi karibuni kumeanza kujitokeza mizozo kati ya wakulima na wafugaji katika baadhi ya maeneo, hivyo ni vyema kuliangalia suala hilo kwa makini ili kuepusha athari hapo baadaye.

Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, alisema katika kipindi hicho, wizara imefanikiwa kupata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mpango kazi.

# Wawili wafa ajali ya bodaboda, lori

**Na Steven William, MUHEZA**

VIJANA wawili waliokuwa wakitumia usafiri wa pikipiki, maarufu bodaboda, wamefariki dunia baada ya kugongwa na lori aina ya Scania lenye namba za usajili T 382 AVW lililokuwa linatoka Tanga mjini.

Tukio hilo limetokea juzi jioni katika Kijiji cha Mkanyageni, Kata ya Ngomeni wilayani Muheza mkoani Tanga katika barabara kuu ya kutoka Tanga mjini kwenda Segera.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza, Richard Muwe, alidai vijana hao ni wakazi wa Tarafa ya Amani wilayani Muheza.

Muwe alidai vijana hao; Eustice Majo, aliyekuwa dereva wa pikipiki hiyo na abiria wake, Halfan Tupa, walikuwa walikuwa wakitoka Tanga mjini.

Alidai kuwa vijana hao walipofika katika eneo hilo, wakati wanapanda mlima kuelekea Kijiji cha Mkanyageni, ghafla lilitokea basi dogo aina ya Coster lenye namba za usajili T 933 DLG ambalo lilikuwa linalipita lori hilo, likawagonga na kusababisha kupoteza mwelekeo na kuingia katika uvungu wa tela la lori kisha kukanyagwa kichwani.

Alidai Jeshi la Polisi wilayani Muheza lilifika eneo la tukio na kuichukua miili ya vijana hao na kuipeleka chumba cha kuhifadhi maiti cha hospitali teule ya wilaya hiyo.



Wakazi wa Tabata Kisukuru, jijini Dar es Salaam, wakijitolea kujenga barabara ya mtaa wao, kwa kiwango cha zege, baada ya kuharibiwa vibaya na mvua. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wakulima viungo wataka bodi yao

**Na Faustine Feliciane, aliyekuwa MOROGORO**

WAKULIMA wa mazao ya viungo wanaolima kwa njia ya asili mkoani Morogoro, wameiomba serikali kuunda bodi ya kusimamia bidhaa zao kama ilivyokuwa kwenye mazao mengine.

Wakizungumza na waandishi wa habari ambao walitembelea Kituo cha Utafiti wa Kilimo Endelevu (SAT) mkoani humo, walisema kuundwa kwa bodi hiyo kutasaidia kuongeza faida kwenye mazao yao kama ilivyo kwenye mazao mengine kama pamba, korosho na kahawa.

Wakulima hao walisema licha ya kupatiwa mafunzo ya kilimo hai na wao kujikita katika kilimo cha viungo mchanganyiko, bado wanakabiliwa na tatizo la kukosa soko la uhakika.

Mmoja wa wakulima hao kutoka Kijiji cha Lubondo, Pendo Ndeme, alilishukuru shirika hilo kwa kazi kubwa linayoifanya kuwapa elimu wakulima na wafugaji, ili jamii hizo zishirikiane kimaendeleo.

Aliiomba serikali kuwaangalia kwa jicho la karibu wakulima wa mazao ya viungo kwa kuwaundia bodi yao.

"Hii itatuongezea tija sisi wakulima, na pia itatufanya tuone sasa mazao yetu yanatambulika, wenzetu wa SAT wametusaidi kupata elimu na kulima kilimo chenye tija kwetu," alisema.

Aliongeza kuwa mazao yao yanafanya vizuri lakini tatizo kubwa ni ukosefu wa masoko ya uhakika ya kuuza bidhaa zao kwa wingi.

"Tunaiomba serikali iangalie upya katika eneo hili kwani kama wakituwezesha na sisi kuwa na bodi yetu ya kutusimamia kama ilivyo kwenye eneo la pamba ambalo wana bodi yao, ni wazi kwamba tutapata tija na wakulima watapata faida kutokana na mazao haya ya viungo.

"Kuna idadi kubwa ya wakulima ambao wanalima viungo mbalimbali nchini. Nafikiri ni wakati mwafaka sasa nao kuwa na bodi yao inayowasimamia," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa SAT, Janeth Maro, alisema chuo chao kilianza mwaka 2015 kikijikita katika elimu ya kilimo hai na kufanya utafiti kuhusu kilimo hicho kwa kushirikiana na taasisi nyingine kama Chuo Kikuu Sokoine cha Kilimo (SUA).

Alisema pamekuwapo na mwitikio mkubwa kwa wananchi na wengine wamehamasika katika kulima mazao mbalimbali yakiwamo mazao ya viungo, lakini tatizo kubwa ni kukosekana kwa soko la uhakika.

"Sisi kama kituo cha mafunzo na utafiti, tumekuwa tukishiriki katika kuwatafutia masoko, lakini kuhakikisha wanakidhi viwango kwa maana bidhaa zao. Hapa kikubwa serikali kuona namna ya kusapoti wakulima hawa kupata soko," alishauri.

**"Kuna idadi kubwa ya wakulima ambao wanalima viungo mbalimbali nchini. Nafikiri ni wakati mwafaka sasa nao kuwa na bodi yao inayowasimamia," alisema.**

# Matumizi nishati mbadala yamwibua Zungu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amezungumzia umuhimu wa matumizi ya nishati mbadala ya gesi ambayo ni rafiki kwa mazingira ukilinganisha na mkaa na kuwataka

Watanzania kugeukia matumizi ya gesi ili kulinda mazingira. Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Circle Gas, Volker Schultz, ofisini kwake jijini Dar es Salaam juzi, Zungu alisema elimu na uhamasishaji zaidi unahitajika kuhusu matumizi mbadala ya nishati.

"Tanzania kama nchi inahamasisha matumizi ya nishati mbadala kama suluhisho pekee la kulinda misitu na mazingira kwa ujumla. Tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali kushirikiana na wadau wa mazingira," alisema.

Alisema Schultz alimtembelea kumwelezea mpango wa kampuni yake kuhamasisha matumizi ya gesi katika majiji ili kupunguza ukataji miti ovyo ambao umekuwa ukiathiri mazingira.

"Kwa sasa matumizi ya mkaa yamekuwa makubwa kutokana na ongezeko la watu, ukataji wa miti umeongezeka na mpaka sasa kwa tafiti zilizopo zaidi ya tani milioni mbili za mkaa zimekuwa zikitumika kwa mwaka kama nishati ya kupikia majumbani, hali hiyo imeleta athari kubwa za kimazingira," alisema Zungu.

Alisema mpango huo ambao utekelezaji wake haujaanza, unalenga kuhudumia majiji makubwa na kwa Tanzania utaanza na jijini Dar esSalaam na kuenea katika majiji engine kutokana na mafanikio yatakayopatikana.

Aliongeza kuwa mpango huo utakapokamilika, mtumiaji hatalazimika kulipa gharama za jiko wala mita papo kwa hapo, badala yake gharama hizo zitalipwa ndani ya kipindi cha miezi 18, huku akilipia gharama za gesi kulingana na matumizi yake. Kwa upande wake, Schultz alisema lengo la kampuni yake ni kuona na kuhakikisha watu wengi katika maeneo ya majiji wanatumia nishati hiyo ya gesi kwa ustawi wa mazingira na afya zao.

"Tunakusudia kutoa huduma hii kwa majiji kama Dar es Salaam na Nairobi ambayo yamekuwa na matumizi makubwa ya mkaa hali ambayo inachangia uwepo wa mabadiliko ya tabia nchi," alisema Schultz na kuongeza kuwa mpango huo utakuwa rafiki kwa mazingira na ustawi wa uchumi.

## HABARI KIMATAIFA

# WHO: Dunia ijiandae kwa janga la Corona

**BEIJING,** China

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema dunia inapaswa kujiandaa kwa uwezekano wa janga la virusi vya corona

Linasema ni mapema sana kuita milipuko wa virusi hivyo janga lakini nchi zinapaswa kuwa katika awamu ya maandalizi.

Limeeleza kuwa janga ni pale maambukizi ya ugonjwa huo yanaposambaa kwa urahisi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine katika maeneo mengi ya dunia.

**Itaahirisha mkutano wa mwaka wa taifa uliotarajiwa kufanyika mwezi ujao ili kuendelea na juhudi za kupambana dhidi ya virusi vya corona.**

Matukio zaidi ya virusi ambavyo husababisha ugonjwa Covid-19, vinaendelea kujitokeza, huku milipuko ya ugonjwa huo ikibainika katika mataifa ya Korea Kusini, Italia na Iran.

Hata hivyo, maambukizi mengi yanapatikana nchini China, chanzo cha asili ya virusi, ambako watu zaidi ya 77,000 wamepata maradhi hayo na zaidi ya 2,600 wamefariki.

Zaidi ya matukio 1,200 yamethibitishwa katika nchi 30 na kumekuwa na vifo zaidi ya 20. Italia iliripoti vifo vya watu wanne siku ya jumatatu na kuifanya idadi ya vifo nchini humo kufikia watu saba.

Masoko ya hisa yalishuka kote duniani kwasababu ya hofu ya athari za kiuchumi

China ilisema itaahirisha mkutano wa mwaka wa taifa uliotarajiwa kufanyika mwezi ujao ili kuendelea na juhudi za kupambana dhidi ya virusi vya corona.

Mkutano huo unaochukua uamuzi wa chama tawala cha Kikomunisti, umekua ukikutana kila mwaka tangu 1978.

Uwiano wa watu waliofariki kutokana na Covid-19 vinaonekana kuwa kati ya asilimia moja hadi mbili ingawa WHO inaonya kwamba kiwango cha vifo bado hakijafahamika.

Jumatatu Iraq, Afghanistan, Kuwait, Oman na Bahrain ziliripoti matukio ya kwanza vyote vikiwahusisha watu waliokua wamewasili kutoka Iran.

Maofisa wa Bahrain walisema mgonjwa aliyeathiriwa na virusi hivyo alikua ni dereva wa basi la shule, na shule kadhaa zimefungwa kutokana na tukio hilo. **BBC**

# Trump ammwagia sifa Modi ziarani India

**NEWDELH,** India

RAIS wa Marekani, Donald Trump na Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi, wameoneshana ukarimu kwa kumwagiana sifa mbele ya umati wa raia wa India, wakihakikishiana kuendeleza uhusiano mzuri kati ya mataifa hayo.

Hatua hiyo imekuja baada ya Rais Trump kuwasili nchini humo na kuhutubia katika uwanja wa mchezo wa kriketi uliohudhuriwa na maelfu ya watu mjini Ahmedabad.

Rais Trump alimwagia sifa kwa uongozi wa modi akisema kwa mara ya kwanza katika historia, kila kijiji cha India kina umeme na raia wengi wameunganishwa na huduma ya mtandao.

Alisema kuwa kasi ya ujenzi wa barabara kuu nchini humo imeongezeka mara mbili kuelekea kaya milioni 70 zaidi.

Rais Trump alitoa hotuba hiyo mbele ya takribani raia 100,000 waliokuwa wakimshangilia katika uwanja wa mchezo wa kriketi wa mji anakotokea waziri mkuu Narendra Modi.

Rais Trump alihutubia kwenye umati mkubwa ambao haijawahi kushuhudiwa na waziri mkuu huyo katika maisha yake ya siasa.

Rais Trump alianza hotuba yake kwa kutangaza kuwa Marekani inaipenda na kuiheshimu India na kuwa nchi yake itaendelea kuwa rafiki mwaminifu kwa watu wa India.

Rais huyo wa Marekani amezuru India wakati kukiwa na mvutano wa kibiashara kati ya mataifa hayo mawili, India ikiwa nchi ya tano kwa uchumi mkubwa duniani.

Mvutano huo uliibuka baada ya utawala wa Rais Trump kuongeza ushuru kwa bidhaa za chuma na alminium kutoka India.

Katika ziara yake ya Inchini humo, Rais Trump alihaidi makubaliano mazuri ya biashara na kuipatia nchi hiyo silaha bora zaidi za kijeshi duniani.

Rais Trump alihitimisha ziara yake jana katika Mji wa New Delhi alipozungumza na Modi. **DW**



Mwanasiasa wa Uganda, Bobi Wine (katikati), akiwa amekabiliwa na polisi walipokuwa wakijaribu kuzuia mikutano yake. **PICHA: AFP**

# Rais wa zamani Misri afariki dunia

**CAIRO,** Misri

RAIS wa zamani wa Misri, Hosni Mubarak, amefariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika hospitali jijini Cairo akiwa na miaka 91

Mubarak alidumu madarakani kwa miongo mitatu kabla ya kung'atuliwa na jeshi baada ya kufanyika kwa maandamano makubwa ya raia.

Mubarak alikutwa na hatia ya kula njama katika mauaji ya waandamanaji wakati wa mapinduzi na kuwekwa kizuizini.

Hata hivyo, hatia hiyo iliondolewa na akaachiwa huru Machi, 2017.Kifo chake kimethibitishwa na Televisheni ya Taifa ya Misri jana.

Mapema jana tovuti ya Al-Watan iliripoti kuwa kiongozi huyo alifariki kwenye hospitali moja ya jeshi. Mubarak alifanyiwa upasuaji mwishoni mwa Januari.

Mtoto wake wa kiume, Alaa alisema siku ya Jumamosi kuwa baba yake yupo mahututi.

Baada ya kuzaliwa mwaka 1928, Mubarak aliingia jeshi kama kijana na kuendelea kuchukua jukumu muhimu katika vita kati ya Israel na Waarabu mwaka 1973.

Alikuwa rais chini ya muongo mmoja baadaye baada ya kutokea kwa mauaji ya Rais Anwar Sadat. Alikuwa na jukumu muhimu katika mchakato wa amani wa Israel - Palestina.

Lakini licha ya kiasi kikubwa cha msaada wa kijeshi ambayo Misri ilipokea wakati alipokuwa madarakani, ukosefu wa ajira, ufukara, na ufisadi uliendelea kuimarika.

Mwaka mmoja baada ya Mubarak kupinduliwa, Mohammed Morsi mwanasiasa Muislamu alishinda uchaguzi wa kwanza wa kidemokrasia nchini Misri.

Morsi naye alitimuliwa madarakani na jeshi mwaka 2013 na kufariki mwaka 2019 akiwa jela.

Mubarak alifungwa kifungo cha maisha kufuatia vifo vya waandamanaji 900 ambao waliuawa na vikosi vya usalama wakati wa maandamano ya mwaka 2011.

Mashtaka hayo baadaye yalifutiliwa mbali na Mubaraka kuachiliwa mwaka 2017. Mgogoro ulizuka mnamo Januari, 2011, baada ya maandamano kama hayo kutokea nchini Tunisia na kusaidia kupinduliwa kwa rais wa taifa hilo. Mubarak alilazimishwa kujiuzulu siku 18 baadaye. **BBC**

# Watu 13 wauawa katika mapigano akiwamo polisi

**BUJUMBURA,** Burundi

WATU 12 waliobeba silaha wameripotiwa kuuawa katika mapigano na vikosi vya kulinda usalama vya serikali ya Burundi, yaliotokea jumapili katika mji mkuu wa Burundi, Bujumbura.

Kiongozi wa wilaya ya Nyabiraba, Ferdinand Simbananiye aliwawaambia waandishi wa habari kwamba kundi lenye wapiganaji 14 lisilojulikana lilishambulia wilaya yake Jumapili, watu 12 miongoni mwao waliuawa, katika makabiliano na jeshi la polisi.

Kiongozi huyo ameongeza kuwa askari polisi mmoja pia aliuawa katika mapigano hayo, huku wapiganaji wawili wakikamatwa wakiwa na silaha sita. Hata hivyo hakuna kundi lolote lililodai kuhusika na shambulio hilo.

Taarifa zinasema kuwa wakazi wa wilaya hiyo iliyopo mkoa wa Bujumbura vijijini, hasa wafuasi wa chama cha upinzani cha CNL wana wasiwasi mkubwa baada ya kutokea mapigano hayo.

Wafuasi wa chama cha CNL kinachoongozwa na Naibu Spika wa Bunge, Agathon Rwasa, wamekuwa wakilalamika kwamba wanakamatwa kiholela na polisi, ikiwashutumu kuhusika katika harakati za kuvuruga usalama. **VOA**

# Wataka asilimia 10 bajeti ya kilimo

**Na Jumbe Ismailly,** MKALAMA

SERIKALI kupitia Wizara ya Kilimo imeshauriwa kuangalia uwezekano wa kuongeza bajeti ya kilimo kutoka asilimia saba ya sasa hadi 10 ili kuwasaidia wakulima kuondokana na umaskini.

Akichangia jana taarifa za kamati za Kudumu za Halmashauri, Diwani wa Mwanga, Mohamed Juma, alisema endapo wakulima wataendelea na kilimo cha sasa huku wakinunua pembejeo kwa bei za juu, kuna uwezekano miongoni mwao kuendelea kuwa maskini.

Kwa mujibu wa diwani huyo, ili kuwawezesha wakulima kuingia kwenye soko huria bila vikwazo vyovyote kikanda, kimataifa au sheria, ni wakati mwafaka kwa serikali kuwaandaa wakulima ili waingie kwenye soko hilo huria.

"Tuko kwenye utandawazi na soko huria hasa kwenye kilimo na soko huria maana yake ni uhuru wa bidhaa kwenda popote pale bila kuwapo vikwazo vya kimataifa, kikanda au sheria. Lazima tuwaandae wakulima wetu waingie katika soko huria na kama hatutawaandaa, tutaendelea kuwa watazamaji kwenye soko hili," alisema.

Diwani huyo pia alielezea namna ya kuwaandaa wakulima kuwa ni kuwawezesha kupata pembejeo za kilimo kwa bei nafuu au kwa bei zenye ruzuku kwa sababu katika nchi za Ulaya ambazo ziko pamoja katika soko huria, wana ruzuku katika kilimo.

"Sasa kama sisi wakulima wetu hawana ruzuku, wananunua mbolea kwa bei ghali, wananunua viuatilifu bei ghali na wananunua pembejeo zingine kwa bei ghali, hawataweza kuingia katika soko huria. Matokeo yake watazalisha kidogo kwa sababu wameshindwa kununua mbolea, wameshindwa kulima vizuri kwa hiyo wanazalisha kidogo kwenye ekari lakini kwa gharama kubwa, alifafanua Mohamed.

Kutokana na hali hiyo, alishauri katika bajeti ijayo, kuangalia uwezekano huo kwa kuwa asilimia 90 ya wakazi wa Wilaya ya Mkalama ni wakulima.

"Kwa hivyo tutafute njia na njia mojawapo ni uzalishaji wa mbegu za mahindi, alizeti na mbegu zingine hata za vitunguu wawezeshwe wakulima ili wazalishe wenyewe. Kwa mfano mbegu ya mahindi kilo moja inauzwa kwa Sh. 5,500," alibainisha.

Akitoa taarifa ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2018/19, Ofisa Mipango wa Wilaya ya Mkalama, Joyce Emanuel, alisema katika kipindi hicho, waliongeza matumizi ya pembejeo na kanuni bora za kilimo kutoka watu wanne kati ya 10 mwaka 2016/17 hadi watu wanane kati ya 10 mwaka 2018/19.

Kwa upande wa sekta ya mifugo, aliweka wazi kuwa walitoa chanjo ya mifugo kwa asilimia 85, kukarabati josho la mifugo katika kata za Gumanga, Nkinto na Nkalankala kwa kushirikiana na wananchi.

Akifunga mkutano maalumu wa halmashauri wa kujadili rasimu ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2020/21, Mwenyekiti wa Halmashauri, James Mkwega, alitoa wito kwa madiwani, wataalamu kwa kushirikiana na viongozi CCM kwenda kujipanga kwa ajili ya kusimamia ukusanyaji wa mapato yanayotokana na vitunguu, zao ambalo msimu wake umeshaanza.




Mkuu wa Biashara wa Zantel, Aneth Muga, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, wakati wa uzinduzi wa kifurushi cha Bonga Mpakabasi, kinachowawezesha wateja wa Zantel, kupiga simu kwenda mitandao yote kwa gharama nafuu. Kushoto ni Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Mussa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi yajengea yatima visima vya maji

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Time To Help imefanikisha ujenzi wa visima viwili vya maji kwenye taasisi ya watoto yatima na shule ya sekondari hivyo kuwaondolea kero ya maji ya muda mrefu.

Uzinduzi huo ulifanyika jana mjini Bagamoyo na kushuhudiwa na wafanyakazi wa kujitolea kutoka Uholanzi ambao walifadhili ujenzi wa visima hivyo kwa kushirikiana na shule za Feza.

Mbunge wa Bagamoyo (CCM), Dk. Shukuru Kawambwa, pia alishuhudia uzinduzi wa visima hivyo na ukarabati wa kituo cha kulelea yatima.

Ofisa Uhusiano wa Time To Help, Mbwana Kitendo, alisema wanajisikia faraja kuona ndoto ya kuwapatia maji wahitaji hao imekamilika.

Alisema taasisi hiyo imekamilisha ujenzi wa kisima kwenye Shule ya Sekondari Boko Mtambani na kituo cha kulelea yatima cha Amazing Steps Orphanage kilichoko Bagamoyo mkoani Pwani.

Kitendo alisema mbali na kujenga kisima cha maji kwenye kituo hicho pia wamekifanyia ukarabati mkubwa wa madarasa na ofisi za walimu zilizokuwa kwenye hali mbaya.

Alisema Time To Help ni taasisi ya kujitolea iliyoanzishwa na shule za Feza kwa ajili ya kusaidia jamii katika nyanja mbalimbali kama maji kupitia ujenzi wa visima.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, taasisi hiyo imekuwa ikikarabati shule mbalimbali zilizokuwa kwenye hali mbaya, kuwapa madawati na kuwajengea maktaba, vitabu na kuwapatia kompyuta.

Alisema hivi karibuni taasisi hiyo iliandaa matembezi ya hisani ya kilomita mbili kwa ajili ya kuhamasisha jamii kuwajali watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali kaulimbiu ikiwa "Watoto Wote Wana Haki ya Kuthaminiwa Utu Wao Kama Watu Wengine'.

Kitendo alisema mwaka huu taasisi hiyo imepanga kuwakatia bima ya afya watoto 1,000 na kwamba kipaumbele chao kitakuwa kwa wanaolelewa katika vituo vya yatima.

Alisema taasisi hiyo imeona ni muhimu kuwakatia bima ya afya ili kuwaondolea usumbufu wanapoumwa kama sehemu yao ya mchango kwa jamii kwa kuwa watoto hao wanahitaji upendo na faraja kutoka kwa jamii.

## Vituo vya afya vyapigwa jeki

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetoa vifaa mbalimbali vikiwamo vya kujifungulia wajawazito katika vituo vya afya Mlimba Halmashauri ya Mji Ifakara mkoani Morogoro na Mwandoya Halmashuari ya Wilaya Meatu mkoani Simiyu.

Aidha, benki hiyo imetoa msaada wa meza 100 na viti 100 katika shule za sekondari Mlabani na Lumemo katika Halmashuari ya Mji wa Ifakara ambapo vimegharimu kiasi cha Sh. milioni tano, huku vifaa vya afya vikigharimu Sh. milioni 15.

Vifaa hivyo vilitolewa mwishoni mwa wiki, ambapo katika kituo cha afya Mwandoya mkoani Simiyu, benki hiyo imetoa vitanda saba na magodoro yake vikiwamo viwili kwa ajili ya kujifungulia wajawazito. Vingine ni mashuka 25, pamoja na vifaa vya kusaidia mjamzito aliyejifungua kwa njia ya upasuaji, na katika Kituo cha Afya Mlimba ni vitanda vitano, kujifungulia wajawazito, mashuka 25 na magodoro matano.

Akizungumza wakati wa hafla ya kupokea vifaa hivyo, Mganga Mfawidhi Kituo cha Afya Mwandoya, Dk. Julius Matongo, alisema kuwa benki hiyo imewanusuru wanawake ambao walikuwa wakipanga foleni kujifungua kutokana na kuwa vitanda vichache.

"Kituo chetu kilikuwa na vitanda viwili na tumekuwa na idadi kubwa ya wajawazito wanaokuja kujifungua, walikuwa wakipanga foleni kutokana na uhaba wa vitanda hivi tuliokuwa nao, lakini leo hii kwa msaada huu ambao tumepokea vitanda viwili tatizo halitakuwapo tena," alisema Dk. Matongo.

Mkuu wa Wilaya ya Meatu, Dk. Joseph Chilongani, akipokea vifaa hivyo aliishukuru NMB kwa msaada huo huku akiwataka watumishi wa kituo hicho na wananchi kuvitunza na kutumia katika kazi iliyolengwa.

Aidha, Dk. Chilongani aliwasisitiza wananchi kutumia benki hiyo kwani faida yake inaonekana kusaidiwa katika shughuli za maendeleo ikiwamo elimu na afya.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**HULE YA CHEKECHEA INAKODISHWA**
hule ya Chekechea inakodishwa u ubia, pia yaweza kubadilishwa a kuwa kituo cha Elimu au kituo na Afya . Ipo Mbezi Luis. Kwa nawasiliano: **0712 480 836 / 0765 38 779.**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


**LOSS REGISTRATION CERTFICATE**

MICRO COMMUNITY DEVELOPMENT FOUNDATION TANZANIA HAS LOST REGISTRATION CERTFICATE NO 2667, ORGINAL TIN CERTFICATE AND ATHER DOCUMENT INFORMATION ABOUT TONEAREST POLICE STATION FOR REF NO **ARU/ARU/RB/72276/2020**
JAGMINDERPAL SINGH SAGHERA
DIRECTOR

156475

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**Michael John Kisingi** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 621 AZQ aina ya SANLG. Chassis number LBRSPJB56F9037749. Engine number SL57FMI*15959395*.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KOR/RB/777/2020**

115647302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO**

Mimi **MAKA KIDELIO NKYA** wa TANGA, nikiwa na akili timamu nimefika mbele ya Hakimu/Wakili na kutamka yafuatayo:

1. Kwamba, Mimi ni Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu HAMIS KARONDA
2. Kwamba, Marehemu HAMIS KARONDA alikuwa mmiliki wa kiwanja Na. 3 kitalu 101 kilichopo barabara ya 15 – Tanga.
3. Kwamba, kwa bahati mbaya hati ya kiwanja hicho imepotea, na tumefanya jitihada ya kuitafuta bila mafanikio.
4. Kwamba, kwa kiapo hiki naiomba ofisi yako iweze kunipatia hati nyingine kwa jina la Marehemu ambalo ni HAMIS KARONDA.

UTHIBITISHO: Nathibitisha kuwa yote niliyotamka hapo juu ni kweli, kweli tupu kwa kadri nijuavyo kwa sheria ya viapo.

Imethibitishwa hapa Tanga na MAKA KIDELIO NKYA.

115647402

**KUPOTEA KWA CHETI**



**Thadeo Lingamila** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0116-0160** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1999 katika shule ya Sekondari Kantalamba..

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: KBA/RB/6776/2010**

156459

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**ARUSHA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi No: 36/2020**

**Ombi la RAMADHANI MOHAMED kuteuliwa**

Msimamizi wa mirathi marehemu HAWA MOHAMED wa Pangani Arusha

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathiya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesiwakitaka mnamo tarehe 20/03/2020 kabla huyomwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 20/02/2020

215646402

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA- MWANZA**
**SHAURI NA 363 LA 2019**

**RICHMOND R.MUTWALA………MUOMBAJI**

**DHIDI YA**
**KHALID BASHIR……………………………MDAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

1. KWA: KHALID BASHIR

Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ ombi dhidi yako katika baraza la ardhi na nyumba mkoa wa mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 12.03.2020 katika chumba cha baraza, barabara ya posta jengo liko mkabala na mahakama kuu ya biashara, Tanzania.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.
KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika, baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na chapa ya Baraza leo tarehe 14/02/2020.

MURIRYA N.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
MWANZA

115646902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No; 60/2020
Ombi la ZAINABU MUSSA WAZIRI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SOPHIA THADEI BRUNO.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 25/02/2020.

115646802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;46/2020**

Ombi la GEORGE SALIEL MINJA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ELINEEMA ANDREA KIMAMBO.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 25/02/2020.

215646602

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11
(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
Katika Mahakama ya mwanzo
DODOMA MJINI
Usimamizi wa mirathi Na. 17/2020
Ombi la JOYCE NATHANIEL PYUZA kuteuliwa
Msimamizi wa mirathi ya Marehemu JAMES DOMINICK FELIX
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhuthuria kesi wakitaka mnamo tarehe 25/3/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

156456

**JAMHURI YAMUUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAM KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**
**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 38/2018**
**(Asilia Shauri la Maombi No 10/2016 Mahakama Kuu ya Tanzania Mbeya)**
**TAFISA GENERAL ENTEERPRISES LTD………MWOMBAJI**
**DHIDI YA**

1. DIAMOND TRUST BANK LTD
2. SUMA JKT AUCTION MART…………………WAJIBU MAOMBI

Kwa: (1). SUMA JKT AUCTION MART
(2). BRIG. GENERAL CHARO YATERI
THE EXECUTIVE DIRECTOR, SUMA JKT HOLDING COMPANY OF 2nd RESPONDENT.
(3). CAPT. FARIJALLAH MKOJERA
THE MANAGING DIRECTOR OF SUMA JKT AUCTION MART.
POPOTE MLIPO – TANZANIA

**KUITWA SHAURINI**

Mnaamriwa na Mahakam hii Muhudhurie hapa Mahakam Kuu Kanda ya Mbeya tarehe 15/4/2020 siku ya Jumatano saa 3:00 asubuhi, ambapo shauri limepangwa kwa maelekezo (kutajwa.)
ELEWA KWAMBA Mkikosa kufika siku hiyo shauri litapangwa kusikilizwa bila ninyi kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa mahakama leo hii tarehe 24 mwezi Februari, mwaka 2020.

215646302


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Nipashe
MWANGA WA JAMII

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei***

***Poa Tupigie 0782253676***


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# LEWANDOWSKI KIDUCHU ATUE MAN UTD

**MUNICH,** Ujerumani

ROBERT Lewandowski amesema ilibaki kidogo asajiliwa na Manchester United mwaka 2012, lakini klabu yake ya wakati huo, Borussia Dortmund haikuwa tayari kumuuza.

Kutokana na hilo, Kocha wa Man United wakati huo, Sir Alex Ferguson aliamua kwenda kuvamia Arsenal kumnasa straika Robin van Persie.

Straika huyo wa Bayern Munich, Lewandowski alisema alizungumza na Ferguson kuhusiano na mpango wa kutua huko Old Trafford, lakini Dortmund ilikaza na kugoma kumuuza.

Lewandowski, 31, alisema: "Nilizungumza na Ferguson miaka miwili baada ya kuichezea Dortmund na nilikuwa tayari kabisa kwenda kujiunga na Manchester United. Na ile ilikuwa kwa sababu ya Ferguson na kwa sababu ya Manchester United.

"Borussia Dortmund ilisema: 'hapana, haiwezekani.' Wakati ule akili yangu ilikuwa kuhama tu, kwa sababu ukweli unapopokea simu ya Sir Alex Ferguson na wewe ni mchezaji kijana, hakuna kitu ambacho unaweza kukataa. Ilikuwa siku yangu muhimu."

# Inter Milan yawafungia kazi Martial, Aubameyang

**MILAN,** Italia

INTER Milan itamsajili mmoja kati ya Anthony Martial wa Manchester United au Pierre-Emerick Aubameyang wa Arsenal iwapo itampoteza straika wake Lautaro Martinez, ambaye anasakwa na Barcelona.

Barcelona inamtazama Martinez kama mrithi wa muda mrefu wa Luis Suarez na miamba hiyo ya Nou Camp iko tayari kulipa pauni milioni 125 kumsajili wakati wa dirisha kuu la usajili la majira ya kiangazi dau ambalo Inter Milan haiwezi kulikataa.

Ndiyo maana miamba hiyo ya San Siro imeanza kujiandaa kisaikolojia na tayari imeanza kuangalia wachezaji wa kuziba pengo lake huku majina ya Martial na Aubameyang (pichani) yakitajwa zaidi pale Inter Milan.

Tangu achukue mikoba ya kuinoa Inter Milan, kocha Antonio Conte amesajili mastaa kadhaa kutoka Ligi Kuu England akiwanasa Romelu Lukaku, Alexis Sanchez, Christian Eriksen, Ashley Young na Victor Moses.

Kikosi cha Conte kimeendelea kuuwasha moto katika Ligi Kuu ya Italia (Serie A).







# *Wilder ataja sababu kuchapwa na Fury*

**LAS VEGAS,** Marekani

BONDIA wa Marekani, Deontay Wilder (pichani) amelaumu vazi alilovaa na kuingia nalo ndani ya ulingo wa ndondi kama sababu iliyomfanya kupoteza taji lake la WBC katika uzani mzito zaidi duniani kwa Muingereza Tyson Fury.

Raia huyo wa Marekani mwenye umri wa miaka 34, alisema kwamba vazi hilo lilikuwa zito sana hatua iliyomfanya kukosa nguvu miguuni katika pigano hilo.

Fury mwenye umri wa miaka 34, alionyesha umahiri wake ili kushinda taji katika mji wa Las Vegas Jumamosi wakati kona ya Wilder iliposalimu amri kwa kutupa kitambaa cheupe wakati pigano hilo lilipokuwa limefika raundi ya saba.

Wilder pia aliviambia vyombo vya habari vya Marekani kwamba ataheshimu kifungo cha pigano la tatu la marudio dhidi ya Fury.

Fury hakuniumiza hata kidogo, lakini ukweli ni kwamba vazi nililovaa lilikuwa na uzito wa kilo 18.1 na ulikuwa mwezi wa kumbukumbu wa historia ya watu weusi.

Fury alibebwa katika ulingo wa ndondi kwa kujitumia kiti cha enzi na pia alikuwa amevalia taji la mfalme.

HABARI MICHEZO

# De Bruyne ataka kubeba ubingwa Uefa

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester City, Kevin de Bruyne, amewaambia wachezaji wenzake watahesabika kuwa wamefeli kama hawatabeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Licha ya kutumia fedha nyingi kuwekeza kwenye kikosi hicho, Man City hatua kubwa zaidi iliyowahi kufika kwenye michuano hiyo ya Ulaya ni nusu fainali, ilipofika miaka minnne iliyopita.

Kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola leo Jumatano kitashuka uwanjani kumenyana na Real Madrid kwenye mtoano wa hatua ya 16-bora kwenye Uwanja wa Bernabeu.

Na kama Uefa adhabu yao itasimama palepale, basi hii itakuwa michuano ya mwisho kwa Man City kushiriki na baada ya hapo itasubiri kwa misimu miwili mingine kufuatia kufungiwa kushiriki michuano hiyo kwa misimu miwili kutokana na kukumbwa na hatia kwenye usawa wa matumizi ya pesa katika usajili.

Kiungo De Bruyne mwenye umri wa miaka 28, alisema: "Ni Madrid na ndio iliyobeba mara nyingi Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lakini, nadhani tutakwenda kwenye mechi hiyo na kujaribu kucheza soka letu, kushambulia na kuipa presha.

"Kama hatutashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, kila mtu atasema tumefeli katika muda wetu tuliotamba. Kwa sababu hicho ndicho kitu ambacho bado hatujakibeba."






# FERNANDES AANZA TAMBO MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Bruno Fernandes, aliyesajiliwa hivi karibuni amesema ndoto zake ni kuwa gwiji hapo Old Trafford baada ya kufunga bao lake la kwanza wakati timu yake hiyo mpya ilipoichapa Watford 3-0 kwenye Ligi Kuu England.

Kiungo huyo Mreno alisema "nimekuja hapa kuwashika" baada ya kuonyesha kiwango bora kabisa ndani ya uwanja tangu alipojiunga na miamba hiyo.

Bruno mwenye umri wa miaka 25, aliyenaswa kwa pauni milioni 55, bao lake la kwanza Man United amefunga kwa mkwaju wa penalti wakati kikosi hicho kikiwa kwenye kampeni kabambe ya kuifukuzia nne-bora.

"Hiki ndicho ninachotaka kufanya, ndicho ninachohitaji kufanya kwenye klabu hii," alisema.

"Kila mtu anafahamu wazi tunataka nafasi ya kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Nipo hapa kuwezesha hilo na timu kushinda mechi zake."

Bruno alitengenezea pia bao la Mason Greenwood huku akihusika pia kwenye bao la pili lililofungwa na Anthony Martial. Kikosi hicho cha Man United kwa sasa kipo nyuma kwa pointi tatu kuikamatia Chelsea kwenye nne-bora.

# *Liverpool yabakiza pointi 12 kubeba Epl*

**LONDON,** England

KOCHA Jurgen Klopp amewaongoza majogoo wa Jiji la Livepool kuweka historia ya kuibuka na ushindi katika michezo 18 mfululizo baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya wagonga nyundo wa London, West Ham United.

Kipindi cha pili cha mchezo huo wakiwa nyumbani Anfield kilitosha kupindua matokeo kutoka kuongozwa kwa mabao 2-1 dhidi ya West Ham United na matokeo kuwa ushindi kwa Liverpool wa mabao 3-2.

Kwa sasa wanahitaji pointi 12 tu kutawazwa kuwa mabingwa wapya wa Ligi Kuu England katika michezo 11 iliyosalia, Liverpool wameibuka na ushindi katika michezo 26 kati ya 27 waliyocheza hadi sasa.

Ushindi dhidi ya West Ham United, unamaana kuwa wameifikia rekodi ya Manchester City ya kuibuka na ushindi katika michezo mingi zaidi (18) ya Epl mfululizo, walifanya hivyo msimu wa 2017-18.

Ikiwa Liverpool wataendelea kucheza kwenye kiwango chao, basi wanaweza kutwaa ubingwa wa Epl katika mchezo dhidi ya Crystal Palace, Machi 20, lakini Klopp anaamini ili wakamilikishe hilo wachezaji wake hawapaswi kubweteka.

"Sikuwa hata na matarajio kuwa tutaivunja au kuifikia (rekodi)," alisema Klopp, ambaye alishuhudia Mohamed Salah na Sadio Mane wakiiokoa siku yake mbele ya West Ham.

"Tumefanya na siamini kama imewezekana kiukweli kabisa. Kila ambacho kimekuwa kikitokea ni juhudi za kila mmoja kwenye klabu."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# JAMIE CARRAGHER AMWANIKA SALAH

Kama utatazama washambuliaji watatu wa Liverpool na kuwauliza mashabiki yupi...

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah ndiye mfungaji kinara wa Liverpool kwenye Ligi Kuu England akiwa na mabao 15 msimu huu na kamwe hataweza kufikisha mabao 47 aliyofunga msimu uliopita, lakini Jamie Carragher anaamini mshambuliaji huyo hakubaliki sana mashabiki wa klabu hiyo.

**Salah alifunga bao lake la 15 kwenye Ligi Kuu msimu huu wakati Liverpool ikishinda 3-2 dhidi ya West Ham juzi usiku.**

"Nadhani Mo Salah anaonekana kama mchezaji wa kiwango cha juu duniani na wale wa nje, lakini na mashabiki wa Liverpool hajakubalika kidogo," Carragher alisema.

"Hakika nenda kutoka msimu wa kwanza na kile anachokifanya sasa, kumekuwa na kutozama kidogo. Lakini hatafunga mabao 47 msimu huu.

Akizungumzia mashabiki wa Liverpool na kutazama mitandao ya kijamii, alisema: "Nadhani Liverpool inayo wachezaji sita wa daraja la juu duniani. Nadhani wanaye kipa, Trent Alexander-Arnold, Virgil van Dijk, Sadio Mane, Roberto Firmino na Salah.

"Nadhani kama ukiwauliza mashabiki wa Liverpool endapo watachukua kiasi kikubwa cha fedha kwa wengine watano, wote watasema hapana, haijalishi ni kiasi gani cha fedha.

"Hakuna namna wangemuuza Alisson ama Van Dijk. Lakini kama utawapa ofa ya pauni milioni 130 kwa Salah, wanaweza kulifikiria hilo.

"Ndiyo maana ninasema hakubaliki sana."

Carragher amebainisha sababu mbili kwa nini sifa ya Salah kati ya mashabiki haiwezi kuwa juu kama ilivyo rekodi yake ya mabao anayostahili kuwa nayo.

"Ni mshambuliaji wa pembeni ambaye anacheza taratibu hiyo ikiwa na maana anatazamwa anapopokea mpira," aliongeza Carragher. "Mara zote anajitazama njiani mwenyewe.

"Lakini si imara kama Mane na si mjanja kama Firmino wakati mpira unapomjia. Kwa hiyo, yeye hupoteza mpira sana katika hali kama hizo. Inaweza kusumbua kumtazama Salah.

"Pia kuna hofu kwamba kuna ubinafsi upande wake. Tuliona hilo likitokea na Mane mapema mwanzoni mwa msimu. Wakati Salah akiwa katika nafasi kila anachofikiri ni endapo anaweza kufunga.

"Wakati huo, hilo linachanganya."

Hata hivyo, Carragher anaamini usumbufu huo lazima utazamwe kwa sababu ya picha kubwa ambayo inaashiria umuhimu wa Salah kwa Liverpool. "Nimecheza na wachezaji wa pembeni Anfield ambao hawakuwa wafungaji. Walikuwa wanamaliza msimu kwa kufunga bao moja kwa sababu walikuwa wakikimbia tu pembeni ya mstari na kukumbana na mabeki wa pembeni kwa kuwakimbilia.

"Salah anapoteza mpira, lakini anafunga mabao.

"Salah ana pasi za mwisho nyingi pia. Ni Lionel Messi pekee mwenye pasi za mwisho nyingi kuliko Salah katika ligi tano bora Ulaya tangu amejiunga na Liverpool.

"Kitu kikubwa ninachokipenda kwake, kamwe hakumbwi na majeraha. Unaona Liverpool inacheza na yupo pale kwa wiki nzima, mechi 97 amecheza kati ya 102 (kwa sasa 98 kati ya 103).

"Kama utatazama dakika kwa bao, kunaweza kuwa na wengine. Lakini kama mimi ni kocha ninamtaka mtu anayecheza kila wiki, asiyekosa mchezo na anayepata matokeo.

## ZISIKUPITE

### AUBAMEYANG NJIAPANDA

ARSENAL inaweza kulazimika kumuuza mshambuliaji wake Pierre-Emerick Aubameyang, 30, kama itashindwa kukubaliana mshahara katika mkataba mpya, wakati huu mkataba wake ukimalizika mwaka 2021. ***(Star)***

### SANCHO KUZITOSA UTD, LIVER

WINGA wa England, Jadon Sancho, 19, anaweza kubaki Dortmund zaidi ya msimu huu licha ya kuhusishwa na kujiunga na Chelsea, Liverpool ama Manchester United katika dirisha la majira ya joto. ***(Ruhr Nachrichten - in German)***

### KUACHANA NA COUTINHO

MKURUGENZI Mkuu wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge bado hajashawishika na Mbrazil Philippe Coutinho, 27. Klabu hiyo ya Ujerumani ina kipengele kinachoiruhusu kumnunua kiungo huyo jumla mwishoni mwa msimu. ***(Bild, via Mail)***

### MATIC KUSEPA MAN UNITED

KIUNGO wa Manchester United, Nemanja Matic, 31, anatarajiwa kuondoka wakati mkataba wake utakapomalizika majira haya ya kiangazi, na wakala wake tayari anamtafutia mwelekeo mbadala, lakini AC Milan haionyeshi kuvutiwa naye kutokana na mshahara mkubwa anaohitaji Mserbia huyo. ***(Calciomercato)***

### ARSENAL NAYO KWA MATUIDI

MANCHESTER United inavutiwa na beki wa Juventus, Blaise Matuidi, 32, huku Arsenal nayo ikijiunga katika mbio za kuisaka saini ya Mfaransa huyo. ***(Calciomercato via Express)***

### MOURINHO AMTAKA WILLIAN

KOCHA wa Tottenham, Joe Mourinho anavutiwa na huduma ya Mbrazil Willian, 31, baada ya kufanya na winga huyo wa Chelsea wakati akiinoa klabu hiyo ya Stamford Bridge. ***(Star)***

### AZIKALISHA ROMA, UNITED

ROMA na Manchester United zimeendelea kuzungumza kuhusu kuubadili mkataba wa mkopo wa beki Muingereza, Chris Smalling, 30, kuwa wa kudumu. ***(Star)***

### LIVER YANUSA DAU LA WERNER

MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig, Mjerumani Timo Werner, 23, anayehusishwa na Liverpool, mkataba wake una kipengele kinachomruhusu kuuvunja kwa pauni milioni 25 pamoja na uhakika wa bonasi inayofafana na kiasi hicho, kuliko kama awali ilivyokuwa ikiaminika kuwa pauni milioni 50. ***(Sport1 - in German)***

### XHAKA AFUNGUKA BIFU LAKE

KIUNGO wa Arsenal, Mswisi Granit Xhaka, 27, amesema alihofu kwamba asingeichezea tena klabu hiyo baada ya kutibuana na mashabiki jambo lililomsababishia kupoteza unahodha - na wasiwasi kama anaweza kupewa jukumu hilo tena. ***(Evening Standard)***

### LEICESTER KUMFUNGA FUCHS

LEICESTER City inazingatia kumpa ofa ya mkataba mpya Christian Fuchs, 33, wakati beki huyo raia wa Austria mkataba wake ukielekea ukingoni. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

## Possi avifunda vyama vya michezo

**Na Saada Akida**

KAIMU Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Ally Possi, amewataka viongozi wa vyama vya michezo kuzingatia mambo muhimu ambayo ni mhimili mkubwa wa kuendeleza michezo nchini.

Aidha, aliyataja mambo hayo kuwa utawala bora, kupiga vita matumizi ya dawa za kulevya na kupambana na kupiga vita suala la rushwa michezoni.

Possi aliyasema hayo jana katika mafunzo ya viongozi wa vyama vya michezo ya siku mmoja yaliyoandaliwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT).

Kuhusu utawala bora, alisema viongozi wanatakiwa kuwa wa wazi katika suala la kifedha kwenye mapato na matumizi ya vyama husika.

"Hatuwezi kusonga mbele kama viongozi wasipokuwa wawazi katika suala la fedha, chama kitaongozwa kwa utawala bora hapo hata wadhamini watajitokeza kusaidia," alisema.

Alisema wadhamini hawawezi kujitokeza kudhamini michezo endapo viongozi wasipokuwa wa wazi na kusema kweli.

"Pia kuepusha migogoro katika chama husika, hivyo viongozi tunatakiwa kuwa waadilifu na tuache kugombana wenyewe kwa wenyewe ndani ya vyama vyetu," alisema.

## Miembeni wajivunia usajili dirisha dogo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZINAR

TIMU ya Miembeni inajivunia usajili wake wa dirisha dogo ambao umezidi kuipaisha katika mzunguko huu wa pili wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja baada ya kutopoteza michezo yote mitatu iliyocheza raundi hii ya lala salama.

Miembeni ambayo bado inaendelea kuugulia maumivu ya kufungiwa kwa kocha wao kwa takriban miezi sita na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imeendeleza wimbi la ushindi mwembamba baada ya kushinda bao 1-0 dhidi ya Mundu katika mchezo wa ligi hiyo uliopigwa juzi kwenye Dimba la Mau.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa timu hiyo, Mbarouk Hanga, alisema malengo makubwa waliyonayo ni kuitoa timu hiyo katika nafasi ya chini waliyokuwapo hivi sasa na kuhakikisha inafika katika nafasi za juu na kujinusuru na wimbi la kushuka daraja.

Alisema matokeo wanayoyapata hivi sasa yametokana na kufanya usajili mzuri katika dirisha dogo ambapo wamesajili wachezaji ambao wanaweza kuhimili vishindo vya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja yenye upinzani mkali.

Kwa sasa Miembeni ina alama 14 na imepanda hadi nafasi ya 10 ikitokea mkiani mwa ligi hiyo yenye timu 13.

# SIMBA, YANGA ZAITIWA MWAMNYETO COASTAL

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Coastal Union, umezitaka Simba ama Yanga kuweka dau la kushawishi mezani kama moja kati ya timu hizo inahitaji huduma ya beki wao wa kati, Bakari Mwamnyeto.

Mwamnyeto amekuwa akihusishwa na klabu hizo kongwe hapa nchini na tetesi zimekuwa zikieleza kuwa tayari amemalizana na uongozi wa Simba na atajiunga na vinara hao wa Ligi Kuu msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Coastal, Hemed Ally 'Aurora', alisema beki huyo ana mkataba wa mwaka mmoja na klabu yao, hivyo hawatamzuia kuondoka endapo mazungumzo na timu inayomhitaji yafikiwa.

**Alisema awali Yanga na Simba walifika kuhitaji huduma ya nyota huyo lakini ilishindikana kutokana na kushindwana dau walilokuwa wakilitaka.**

"Kwa uwezo wa beki wetu, tuna imani msimu ujao hatutakuwa naye hivyo tumeanza mchakato wa kutafuta mbadala wake ndani na nje ya Coastal," alisema Aurora.

Alisema hawana sababu ya kumzuia nyota wao huyo, endapo timu inayomtaka itaenda na dau zuri litakaosaidia kusajili nyota wengine.

"Suala la kwamba tayari amesajiliwa na Simba na kusubiriwa amalize msimu, hizo taarifa si za kweli, kama nilivyosema awali mchezaji wetu bado ana mkataba wa mwaka mmoja kutumikia Coastal," alisema Aurora.

TUPO VIZURI...



Viungo wa Simba, Mbrazil Gerson Fraga 'Vieira' (kulia) na Jonas Mkude wakichuana mazoezini katika Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga jana, asubuhi, kabla ya jioni kuvaana na Stand United kwenye mechi ya hatua ya 16-Bora ya Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), maarufu FA Cup. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Polisi waifuata Singida kwa tahadhari*

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuifurumusha Ruvu Shooting kwa mabao 3-1, timu ya Polisi Tanzania itaanza safari ya kuifuata Singida United kesho tayari kwa mechi yao ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Liti zamani Namfua.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Malale Hamsini, alisema kikosi chake kinaendelea vizuri na mazoezi na wachezaji wake wote wapo fiti kuelekea mechi hiyo isipokuwa Baraka Majogolo ambaye anasumbuliwa na jino.

"Singida ipo mkiani, lakini tukikutana nayo itatukamia vikali, hilo tunalifahamu, hivyo tunatakiwa tuingie uwanjani kwa tahadhari kubwa ndio maana tunawahi kuondoka ili wachezaji wapate muda wa kupumzika kuelekea katika mchezo huo," alisema Malale.

Hata hivyo, alisema mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani na kusema mpaka leo mchana atajua wachezaji wangapi wanaondoka kuelekea mkoani humo na wangapi watabaki.

"Sina wasiwasi na mchezo huo ambao naamini utakuwa na ushindani mkubwa, kwa upande wetu tumejipanga vizuri kila idara kuhakikisha hatupotezi mchezo huo japokuwa tutakuwa ugenini, tutaendeleza ushindani wetu kama tulivyofanya kwenye michezo iliyopita," alisema.

Aliongeza Ligi Kuu msimu huu ina ushindani mkubwa na kwamba kila timu imejizatiti vizuri hali inayosababisha soka la Tanzania lizidi kukua na wachezaji wetu kupata nafasi ya kwenda kufanya majaribio nje ya nchi ya kucheza soka la kulipwa.

"Ushindani uliopo kwa sasa unaleta chachu ya maendeleo ya soka Tanzania, vile vile unasaidia wachezaji wetu kujitangaza nje ya nchi kupitia kwa mawakala mbalimbali wanaolifuatilia soka letu, hivyo kuwasaidia kupata nafasi ya kucheza soka la kulipwa," alisema.

Polisi Tanzania kwa sasa ipo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 37 baada ya mechi 24 huku Singida United ikiburuza mkia na pointi zake 12.

# Michezo

Jumatano Februari 26, 2020

Nipashe




Carragher amwanika Salah UKURASA 30

CHA TATU...




Beki wa pembeni wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold akimzidi akili kipa wa West Ham, Lukasz Fabianski kwa kuucheza mpira ambao ulimpita na kuzamishwa kimyani na Sadio Mane aliyeiandikia timu yake bao la tatu baada ya kukuta lango likiwa wazi kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga: Ligi bingwa Simba, hesabu FA

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga umeweka wazi kuwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara kwa sasa ni ndoto kutokana na mahasimu wao, Simba kuwaacha mbali kwa pointi, na badala yake wanaelekeza nguvu zao kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF) maarufu Kombe la FA.

Yanga kwa sasa ina pointi 41 katika nafasi ya nne baada ya mechi 22, ikiwa ni alama 21 nyuma ya vinara Simba na nne nyuma ya Azam FC iliyopo nafasi ya pili. Hata hivyo, Simba na Azam zipo mechi mbili mbele, lakini katika nafasi ya tatu kuna Namungo FC yenye alama 43 baada ya mechi 23.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa klabu hiyo, Boniface Mkwasa, alisema dalili ya kutwaa ubingwa haipo na kwamba kwa sasa wanajipanga kwa ajili ya kutwaa Kombe la Shirikisho ambapo leo wanashuka dimbani kuumana na timu ya Gwambina FC kutoka mkoani Mwanza.

"Kupata ubingwa kwetu si rahisi, kwa sasa nguvu zote tunazielekeza kwenye michuano hiyo ambayo naamini tukipambana tuna uwezo wa kutwaa kombe hilo, tumekaa na wachezaji wetu kila mmoja ana morali ya kutwaa kombe hilo, kikubwa ni kuongeza juhudi na ziada," alisema Mkwasa huku akiwataka mashabiki wao wasikatishwe tamaa na matokeo ya sare nne walizozipata mfululizo katika michezo yao ya Ligi Kuu iliyopita na kudai kwa sasa wayasahau.

Wakati Yanga wakianika mikakati yao, Kocha wa Gwambina FC, Flugence Novatus pamoja na uongozi wa timu hiyo ya Ligi Daraja la Kwanza mkoani Mwanza umesema hawamhofii mchezaji wa mahasimu wao, Bernard Morrison kwa kusema angekuwa mchezaji mzuri angeipa matokeo mazuri timu yake hiyo. Novatus alisema hawatakuwa na huruma pindi watakapokutana na mahasimu wao na kuwataka watarajie mchezo wenye presha kubwa kutokana na kuwa na wachezaji wenye uwezo mkubwa licha ya kutokuwa kwenye Ligi Kuu.

# SIMBA YATAKATA FA

## ●●● Dilunga aitanguliza robo fainali, waahidi makombe yote mawili msimu huu, Namungo nayo...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya mikwaju ya penalti ya Hassan Dilunga, jana yalipeleka Simba kwenye hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu FA Cup, kwa kuitoa Stand United kwa mikwaju ya penalti 3-2, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga.

**Dilunga alifunga bao la kwanza kwa mkwaju wa penalti dakika ya 50, kabla ya Stand United kusawazisha, pia alifunga penalti nyingine baada ya dakika 90 kumalizika na changamoto ya matuta kuchukua hatua yake.**

Ilikuwa ni penalti ya tano, ambayo iliifanya Simba kusonga mbele, baada ya ile ya mwisho ya Stand United kugonga nguzo na kutoka nje.

Penalti zingine za Simba zilizotinga wavuni zilipigwa na Claotus Chama na Deo Kanda, huku zile za Meddie Kagere na Ibrahim Ajibu zikiota mbawa.

Baada ya mechi hiyo kuanza, dakika ya nane tu ya mchezo, Shiza Kichuya alimlamba chenga beki wa timu hiyo na kuingia ndani, kabla ya kuachika shuti lililotoka nje kidogo ya lango.

Stand United ilijibu shambulio hilo dakika ya 20, wakati Juma Fakhi aliposahauliwa na mabeki wa Simba, akaupata mpira kwenye winga ya kushoto na kuingia ndani kidogo, kabla ya kuachia shuti kubwa lililotoka nje ya lango.

Mchezaji huyo huyo alikosa bao dakika ya 37, alipoupata mpira akiwa ndani ya eneo la hatari la Simba, lakini shuti lake lilidakwa na kipa Beno Kalolanya.

Dakika mbili baadaye Meddie Kagere aliukosa mpira wa kuunganisha, kufuatia krosi safi kutoka kwa Kichuya.

Bao la kusawazisha la Stand lilifungwa na Miraji Salehe dakika ya 50 kutokana na makosa ya beki wa kati wa Simba Tairone Santos kushindwa kupiga mpira haraka, ukamgonga Zamogoni Pangapanga ambaye aliuchukua na kuukokota, kabla ya kupiga krosi safi iliyomkuta mfungaji.

Hata hivyo, Miraji alikuwa ni mmoja wa wachezaji waliokosa mikwaju ya penalti, pamoja na mwenzake Majid Kimbondile.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Dilunga alisema malengo yao msimu huu ni kutwaa mataji yote mawili, FA Cup na Ligi Kuu Bara.

Kwa sasa Simba ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiongoza kwa pointi 15 zaidi kutoka timu inayoshika nafasi ya pili, Azam FC yenye alama 45.

Timu zingine zilizotinga hatua ya robo fainali ni Namungo FC ambayo jana ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, iliichapa Mbeya City mabao 2-1, Panama ikakung'utwa mabao 2-5 na Sahare All Stars kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, na kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Ndanda ilitumia vema uwanja wa nyumbani kwa kuichapa Kitayosa FC mabao 3-1.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >